SIRI PART 3

JASUSI/GAIDI

SEASON 5

MTUNZI: PATRICK.CK



HADITHI HII NI MALI YA MWANDISHI NA HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA KWA HIYO HAIRUHUSIWI KUCHAPISHA, AU KUITUMIA KWA NAMNA NYINGINE HADITHI HII BILA RUHUSA YA MWANDISHI.HATUA KALI ITACHUKULIWA KWA YEYOTE ATAKAYEKIUKA MASHARTI HAYA..

SIMULIZI NYINGINE ZA MTUNZI PATRICK.CK

1.MISS TANZANIA
2.I WAS WRONG
3.TEN CHAPTERS
4.I DO
5.SERENA
6.BEFORE I DIE
7.BEYOND PAIN
8.PENIELA
9.QUEEN MONICA
10.THE FOOTBALL
11.I DIED TO SAVE PRESIDENT
12.KIAPO CHA JASUSI
13.KIKOSI CHA SIRI
14.SIRI

MAWASILIANO
0764294499

ILIPOISHIA SEHEMU ILIYOPITA

VICTORIA – SHELI SHELI

Saa nane za usiku mlango wa chumba walimo akina Mathew ukafunguliwa wakaingia walinzi wanne.Tayari akina Mathew alikuwa wamepitiwa na usingizi.Mathew akaamshwa na kutolewa mle ndani akapelekwa katika chumba Fulani ambako alimkuta Jeffrey.

“Abu Zalawi tumekuondoa usingizini lakini ni kwa jambo la muhimu” akasema Jeffrey

“Tumepewa maelekezo kwamba wewe na wale wanasayansi kesho mtapelekwa Marekani kwa ndege maalum” akasema Jeffrey na kumpa Mathew maelekezo ya namna mpango utakavyokuwa

“Abu Zalawi sisi tumemaliza kwa upande wetu ahsante sana kwa ushirikiano wako .Nakutakia kila la heri katika jukumu zito ulilopewa” akasema Jeffrey

“Nashukuru sana Jeffrey na ninawaahidi kwamba nitafanya kila niwezalo kuhakikisha ninafanikisha kupata kile nilichotumwa nikafanye nchini Iran” akasema Mathew na kuagana na Jeffrey akarejeshwa tena katika kile chumba chao

“Hawa jamaa walikuwa wanataka nini? akauliza Yasser baada ya Mathew kurejea

“Bado wanaendelea kunihoji wakidhani labda nimebadili msimamo wangu.Wameniambia nitafakari hadi kesho kabla

sijakutana na mateso ambayo sijawahi kuyaona” akadanganya Mathew

“Abu Zalawi chochote unachokifahamu usiwaeleze hawa jamaa.Hata ukiwaeleza chochote hawatakuacha salama.Usifanye nao makubaliano yoyote makatili hawa” akasema Yasser

“Niko tayari kufa lakini si kuwaeleza chochote Marekani.Msihofu ndugu zangu hawawezi kupata chochote kutoka kwangu” akasema Mathew wakampongeza kisha kila

mmoja akaenda kulala katika godoro lake

“Mpaka hapa nilipofika nimefanya vizuri.Hawa jamaa tayari wameniamini na hicho ndicho hasa kitu kikubwa kwani hawa ndio watakaonisaidia niaminiwe na mamlaka za Iran.Ninaingia katika sehemu ngumu sana ya misheni hii.Namuomba Mungu anisimamie” akawaza Mathew

****

Saa mbili za asubuhi mlango wa chumba ulifunguliwa akina Mathew wakaamriwa kusimama halafu kila mmoja akafungwa pingu na kuvishwa mfuko kichwani kisha wakatolewa ndani ya kile chumba

“Mnakwenda kutuua?akauliza Yasser lakini hakuna aliyemjibu

“Tungeomba mtupatie nafasi ya dakika chache tusali kabla ya kuuawa” akasema Sajid Hassim

Waliingizwa katika gari mlango ukafungwa wakaondoka.Ndani ya lile gari ambalo hawakulijua ni la aina gani kulikuwa na watu wanne wenye silaha wakiwalinda.

Baada ya dakika kadhaa gari lile likasimama mlango wa nyuma ukafunguliwa wakashushwa halafu taratibu walianza kupandishwa ngazi na kuingia katika ndege.Kila mmoja akakalishwa katika kiti chake na kufungwa pingu miguu na mikono zilizounganishwa na mnyororo mrefu.Dakika chache baadae

ndege ikapaa na ilipokaa sawa angani mifuko waliyofunikiwa kichwani ikatolewa.Ndani ya ndege kulikuwa na walinzi wanne waliokuwa na silaha.

Ndege iliendelea kupasua anga huku akina Mathew wakikirimiwa kwa vinywaji na vitafunwa

“Kazi inaanzia hapa” akawaza Mathew na kumuita mmoja wa walinzi akamwambia anahitaji akajisaidie.Mlinzi Yule akafungua mahala minyororo ile ilipofungwa kisha akampeleka Mathew

chooni.Akamfungulia mlango Mathe akaingia kisha mlinzi Yule akasimama kwa nje akimsubiri.Mathew akapapasa mahala alipoelekezwa akakuta kuna funguo ya kufungulia zile pingu.Haraka haraka akafungua pingu za mikono halafu akafungua za miguu akawa huru.Akasimama pembeni ya mlango

Zilipita dakika tano Yule mlinzi akagonga mlango na kumuuliza Mathew kama amekwisha maliza kujisaidia.Mara akasikia sauti ya muanguko wa kitu

akafungua mlango haraka haraka kuchungulia lakini kitendo cha kuchungulia akajikuta akipigwa kichwa kizito halafu akadakwa na kuvutwa ndani.Mathew akamuongeza kichwa kingine na ngumu za mfululizo Yule mlinzi akaanguka chini

“Sihitaji kumchunguza kama bado ana fahamu.Ninaiamini mikono yangu,haijawahi kukosea” akawaza Mathew akamsachi Yule jamaa na kuchukua bunduki yake pamoja na bastora akavaa fulana ya

kujikinga na risasi aliyokuwa ameivaa Yule mlinzi.Akamfunga Yule mlinzi kwa pingu halafu akafungua mlango taratibu akachungulia nje hakukuwa na mtu maeneo yale ya karibu akatoka na kuanza kutembea kwa kunyata.Alijitokeza katika chumba walimokuwamo wale wanasayansi ambao wote walipatwa na mstuko mkubwa baada ya kumuona Mathew akiwa na bunduki na bastora.Haraka haraka akamfuata Yasser akamfungua pingu za mikono na miguu

akawa huru akampa bunduki halafu akamfungua Muharrem Idris na kumtaka aendelee kuwafungua wenzake.Mathew akanyata kuelekea katika chumba ambacho walinzi wale walikuwa wamekaa wakizungumza huku wakipata kinywaji.Hawakuwa na wasiwasi wowote wakiamini mwenzao alikuwa katika chumba cha wafungwa akiendelea na zamu ya ulinzi.Mathew akachungulia katika kioo akawaona namna walivyokaa halafu taratibu akakishika kitasa akakinyonga

kikafunguka na kwa kasi ya umeme akajitoma ndani ya kile chumba cha walinzi.Walipatwa na mstuko mkubwa

“Wote simameni taratibu huku kila mmoja mikono yake ikiwa juu !! Mathew akaamuru.Taratibu walinzi wale wakaanza kuinuka taratibu na ghafla mlinzi mmoja akashusha mkono akataka kuchomoa bastora yake lakini kabla hajaifikia risasi zikasikika na Yule mlinzi akaanguka chini.Nyuma ya Mathew alikuwa amesimama

Yasser akiwa na bunduki inayofuka moshi.Ndiye aliyemmaliza Yule mlinzi

Walinzi wale wakachukuliwa wote na kufungwa pingu .

“Tunatakiwa kuidhibiti ndege na kuibadili uelekeo wake ! akasema Mathew

“Abu Zalawi kuna jambo ambalo hatukuwa tumekueleza.Sisi wote hapa ni wanajeshi na miongoni mwetu Abdul Razaq ni rubani wa ndege hivyo hakuna kitu cha kusubiri twende haraka tukawadhibiti wale marubani !

akasema Yasser kisha wakatoka katika chumba kile wakaanza kunyata kuelekea katika chumba cha marubani.Mlango wa chumba cha marubani ulikuwa umefungwa kwa ndani.Bila kupoteza muda Yasser akamimina risasi katika kitasa na kukisambaratisha Mathew akaurukia teke mlango ukafunguka wakaingia ndani ya chumba kile cha marubani .Mathew akawataka wasimame na watoke katika viti vyao marubani wale wakatii kisha Abdu Razaq na Tayeb Burhan

wakashika hatamu na kuanza kuiongoza ndege .Kitu cha kwanza walichokifanya ni kuzima kifaa kinachowezesha ndege kuonekana na kufuatiliwa katika rada.

“Abdu badili uelekeo wa ndege tunakwenda nyumbani ! akasema Yasser kwa furaha kubwa.

“Mafuta yaliyopo yanaweza kutufikisha Iran?Mathew akauliza

“Ndiyo.Mafuta yanatosha kutufikisha nyumbani.Ahsante Abu Zalawi” akajibu Abdu Razaq

“Vipi kuhusu mimi?Nitakubaliwa kuingia Iran kutokana na historia yangu ya ugaidi?akauliza Mathew

“Abu Zalawi wewe ni shujaa na unastahili sifa kubwa.Ni wewe uliyesababisha haya yote yakawezekana.Ni wewe uliyesababisha leo hii tunarejea tena nyumbani.Utapokelewa kwa mikono miwili Abu Zalawi usihofu” akasema Yasser na kumkumbatia Mathew kwa furaha kubwa kisha akaungana

na wenzake kuimba kwa furaha wimbo wa taifa la Iran.

ENDELEA.....

Tangu kulipopambazuka,tayari SNSA walianza kufuatilia kilichokuwa kinaendelea katika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere.Hii ni baada ya kuhisi kuwa Sattar Sayf Al Din ambaye anatumwa Tanzania kusambaza virusi angeweza kushukia katika uwanja huo.Tayari walikwisha jiunga na mfumo wa ulinzi wa uwanjani hapo na walikuwa

wanafuatilia kamera zote kufahamu kilichokuwa kinaendelea.Uwanja wa Julius Nyerere bado ulikuendelea kufungwa na ulikuwa chini ya uangalizi wa vikosi vya jeshi la Tanzania.

Asubuhi hii jiji la Dar es salaam lilikuwa shwari na hakukuripotiwa matukio yoyote ya vurugu.Maduka na masoko yalianza kufunguliwa ili kuwawezesha wananchi kujipatia mahitaji muhimu,wananchi wengine waliokuwa wamekimbilia katika makambi maalum

yaliyotengwa kwa ajili ya kuwahifadhi watu waliokimbia mapigano,walianza kurejea katika majumba yao kufanya usafi na kuhifadhi mali zao.Taratibu hali ya maisha katika jiji la Dar es salaam ilianza kurejea kuwa ya kawaida lakini bado doria za vikosi vya ulinzi na usalama ziliendelea katika mitaa mbali mbali ya jiji ili kuhakikisha hakuna vurugu zozote zinazoendelea kutokea.

Saa moja na dakika kumi na saba,Gosu Gosu na Nawal waliwasili ofisi kuu SNSA na

moja kwa moja wakaelekea ofisini kwa Ruby na kumkuta akiendelea na kazi

“Tayari kazi imekwisha anza.Tumeanza kufuatilia kila kinachoendelea uwanjani hapo toka saa kumi na mbili za asubuhi na mpaka sasa hakuna chochote tulichokipata.Zimetua helkopta mbili za jeshi na ndege moja ya jeshi la Tanzania.Tunaendelea kufuatilia kwani kama nilivyosema jana kuna uwezekano mkubwa Sattar Sayf Al Din akaingia hapa

nchini kuanzia saa sita za mchana wa leo” akasema Ruby

“Nina mashaka kidogo.Ni vipi kama Sattar atatumia ndege ya kawaida ya abiria na akaenda kutua katika uwanja wa kimataifa wa Kilimanjaro au hata Nairobi halafu akaja Dar es salaam kwa gari ? Akauliza Gosu Gosu

“Hilo haliwezekani” akasema Nawal

“Kirusi hicho ni hatari sana na hawawezi kutumia ndege ya abiria kusafirishia.Lazima watatumia ndege maalum kuhakikisha

kinafika kikiwa salama hivyo kwa vyovyote vile lazima watatumia uwanja huu wa Julius Nyerere" akasema Nawal

"Tuendelee kufuatilia na kama hatutapata chochote tutatafuta namna nyingine ya kuweza kumpata Sattar lakini kwa siku ya leo kwa namna yoyote ile lazima tuhakikishe tumekipata kirusi hicho" akasema Ruby wakaendelea kufuatilia kamera zile za uwanja wa ndege wa Julius Nyerere katika runinga kubwa wakiwa ofisini kwa Ruby

“Nawal unaonaje ukimpigia simu Habiba Jawad ukamuuliza kama amepata taarifa zozote za kuhusu Sattar Sayf Al Din pamoja na Mathew? Akauliza Ruby na kumpatia Nawal simu akampigia Habiba Jawad

“Mama Habiba”akasema Nawal baada ya Habiba kupokea simu

“Nawal unaendeleaje? Akauliza Habiba

“Niko salama kabisa mama.Kwa ujumla jiji la Dar es salaam liko salama.Hakuna matukio ya vurugu japo

hakuna uhakika kama vurugu zimekwisha au vipi lakini hadi sasa jiji ni salama kabisa.Kuna taarifa yoyote mpya huko?Nawal akauliza

“Kwa sasa bado sijapata taarifa yoyote mpya.Bado taarifa niliyonayo ni ile ile kwamba Sattar Sayf Al Din amekwisha ondoka Marekani akielekea Tanzania.Kuna mipango yoyote mnayo ya kujua mahala atakapofikia huyu mtu? Akauliza Habiba

“Ndiyo mama.Kwa sasa tunaendelea kufuatilia katika uwanja wa ndege wa kimataifa

wa Julius Nyerere hapa Dar es salaam ambako tuna uhakika ndiko atatua.Tunategemea kuanzia saa sita mchana wa leo awe amewasili hapa Dar es salaam kutokana na muda alioondoka Marekani.Nitakujulisha kile tutakachokipata” akasema Nawal

“Nawal narudia tena kukusisitiza kwamba kwa namna yoyote ile lazima muhakikishe Sattar anakamatwa kirusi hakisambazwi nchini Tanzania.Umenielewa Nawal?

“Nimekuelewa mama,tunafanya kila tuwezalo.Kuna taarifa zooze umepata kuhusu Mathew Mulumbi? Nawal akauliza

“Hapana.Bado sijapata taarifa zozote.Msihofu kuhusu Mathew atakuwa salama japo atakumbana na magumu mengi lakini ninao uhakika mkubwa atayashinda yote na atamaliza misheni yake.Tuendelee kumuombea ili awe salama.Kwa sasa jielekezeni zaidi katika kirusi hicho na mimi kila nikipata taarifa yoyote ambayo naamini

inaweza kuwa na msaada kwenu nitawajulisha haraka sana” akasema Habiba

“Mama wewe unafahamiana na viongozi wote wakuu wa IS.Kwa nini usiwasiliane nao wakueleze mahala alipo Assad ili iturahishishie kumpata Sattar Sayf Al Din endapo hatatumia uwanja wa ndege wa Julius Nyerere?akauliza Nawal

“Mimi ni mfadhili wao tu na si sehemu yao ya uongozi hivyo kuna mambo mengine ambayo hawawezi kuniambia.Hata hivyo

nitajitahidi kutafuta taarifa za namna ya kuweza kumpata huyo Assad na nikifanikiwa nitawajulisha” akasema Habiba na kuagana na Nawal

“Kama mlivyosikia hakuna jipya kutoka kwa Habiba.Tuendelee na mipango yetu tuliyoipanga” akasema Nawal

WASHINGTON DC – MAREKANI

Taarifa za kupotea kwa ndege iliyowabeba Mathew Mulumbi mtuhumiwa wa Ugaidi aliyelipua ubalozi wa Marekani nchini Tanzania,pamoja na raia sita wa Iran waliokuwa wanashikiliwa Mateka na Marekani kwa muda mrefu,zilipokelewa kwa mstuko nchini Marekani.Haraka haraka juhudi za kuitafuta ndege hiyo zikaanza.Kitu cha kwanza

walichokihisi ni kwamba yawezekana ndege hiyo imeanguka katika bahari ya Hindi.

Taarifa hiyo ya kupotea kwa ndege,zikamfikia Rais William Washington wa Marekani ambaye bila kupoteza muda akampigia simu makamu wake Mark Piller

“Mheshimiwa Rais” akasema Mark Piller baada ya kupokea simu

“Mark nimejulishwa kuhusu kupotea kwa ndege yetu iliyokuwa inamleta

mtuhumiwa wa shambulio la ugaidi katika ubalozi wetu jijini Dar es salaam.Kuna chochote unaweza ukaniambia kuhusiana na tukio hilo? Akauliza Rais William

“Ndiyo mheshimiwa Rais. Ndege hiyo haijapotea bali kwa sasa imebadili uelekeo na kuelekea chini Iran. Hii ni katika ule mpango niliokueleza kwamba tunataka kumtumia Abu Zalawi kuingia nchini Iran.Usihofu mheshimiwa Rais kila kitu kimepangwa kwa umakini mkubwa sana” akasema Mark Piller

“Mark una uhakika hiki mnachokifanya kitafanikiwa? akauliza Rais William

“Naomba uniamini mheshimiwa Rais.Mpango huu utafanikiwa na utakuwa na manufaa makubwa sana kwetu.Usiwe na hofu mheshimiwa Rais tuko makini sanana tumejipanga vizuri” akajibu Mark

“Mark jitahidini sana kufanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba jambo hili haligeuki na kuwa mzigo kwetu.Endapo huyo gaidi mnayemtumia akigundulika

mtakuwa mmeivua nguo nchi yetu”

“Usiwe na shaka mheshimiwa Rais.Tunaamini Abu Zalawi ataifanya vyema kazi anayotumwa kwenda kuifanya kule Iran” akajibu Mark Piller

“Vipi kuhusu kile kirusi? Tayari kimefika Tanzania? Akauliza Rais William

“Kwa taarifa nilizonazo ni kwamba Sattar Sayf Al Din anakaribia kufika Tanzania na atakapofika tutajulishwa na watu wetu kule.Kila kitu

kitakwenda sawa mheshimiwa Rais”

“Mark narudia tena kutoa angalizo kwamba kila hatua za tahadhari lazima zichukuliwe kuwalinda watu wetu kule Tanzania.Sitaki kupoteza hata raia mmoja wa Marekani katika suala hili” akasema Rais William

“Mheshimiwa Rais naendelea kukusisitiza kwamba hutakiwi kuonyesha kama unafahamu chochote kuhusiana na haya mambo niliyokueleza.Yote unayoyafahamu endelea

kuyafanya siri kubwa ambayo hata mke wako asiifahamu”akasema Mark Piller

“Nitafanya hivyo Mark” akajibu Rais William na kuagana na Mark Piller ambaye naye alimpigia simu David Walker kiongozi wa kikundi kile ambacho kimejipa jina la The great 20 au kwa kifupi G20.

“David nimetoka kuzungumza na Rais muda mfupi uliopita kuhusiana na kupotea kwa ndege yetu”

“Anasemaje Rais? Akauliza David

“Hafahamu chochote.Yeye na wenzake wanachoamini ni kwamba yawezekana ndege imeangukia baharini”

“Safi sana.Mark mpango unakwenda vizuri sana na hivi tuzungumzavyo tayari ndege hiyo inaelekea Iran.Tunafuatilia na tunaendelea kukujulisha kila kitakachojiri” akasema David Walker na kuagana na Mark kwani alikuwa na safari ya kuelekea kwa Jason Washington mkurugenzi wa

CIA.Hakupoteza muda akatoka kuelekea katika gari lake akaondoka kuelekea nyumbani kwa mkurugenzi wa CIA.Tayari mida hiyo ilikaribia saa kumi za usiku kwa saa za Marekani.

David alifika nyumbani kwa Jason Washington akakaribishwa ndani na walinzi wa Jason.Alipelekwa moja kwa moja katika ofisi ya Jason akaingia na kumkuta akizungumza na mtu simuni.Jason akamfanyia ishara aketi na asubiri amalize mazungumzo na Yule mtu

simuni.Baada ya dakika moja Jason akaagana na Yule aliyekuwa akizungumza naye simuni akamgeukia David

“Karibu David” akasema Jason

“Jason nikuonapo katika sura hiyo najua kuna jambo haliko sawa” akasema David

“Ni kweli David.Jana kijana wangu alichukua gari la mama yake bila ruhusa akaenda nalo katika sherehe ya kuzaliwa mmoja wa marafiki zake na wakati wakirudi amegonga gari lingine” akasema Jason

“Ameumia? David akauliza

“Hapana hajaumia” akajibu Jason

“Usijali Jason hayo ni mambo ya kawaida kwa vijana wetu yatakwisha tu.Kitu kikubwa hajaumia katika ajali hiyo” akasema David Walker

“Tuachane na hayo David.Twende moja kwa moja katika kile kilichokuleta hapa alfajiri hii” akasema Jason

“Jason kuna jambo limenileta hapa tulijadili mimi na wewe ambalo ni la muhimu sana katika ule mpango wetu unaoendelea”

“Ndiyo David.Jambo gani hilo? Kwanza kabla ya yote nataka niwape hongera sana kwa namna mlivyo ratibu mpango huu kiasi cha kutotiliwa shaka hata kidogo kama ni mpango uliotengenezwa.Hivi sasa tayari utafutaji wa ndege hiyo iliyopotea umeanza na wote wanaamini yawezekana ikawa imepata hitilafu ikaanguka na kuzama katika bahari ya Hindi.Una jambo gani muhimu la kuongezea katika mpango huu David? Akauliza Jason

“Mpango kama unavyoona unakwenda vizuri sana na tuna uhakika mkubwa kwamba Abu Zalawi ataingia nchini Iran.Hata hivyo kuna jambo ninalifikiria la muhimu sana ambalo hatukulitilia maanani hapo kabla”

“Ndiyo nakusikiliza David” akasema Jason

“Uhakika wa Abu Zalawi kuingia nchini Iran ni mkubwa.Hatukutegeneza mpango wowote wa kumsaidia Abu Zalawi akiwa nchini Iran.Akiwa kule kuna mambo ambayo atayahitaji kama vile

mawasiliano,usafiri nk hivyo lazima awepo mtu wa kumsaidia kuyapata haya kwa siri bila mtu huyo kujulikana” akasema David

“Hilo ni wazo zuri sana David lakini hatuna watu wetu kule Tehran.Endapo tungekuwa na watu wetu kule ingekuwa rahisi kumpa Abu Zalawi msaada muda wowote atakaouhitaji”akasema Jason

“Ni kweli sisi hatuna watu wetu Tehran lakini tunao wenzetu wa Mossad.Wao wana majasusi wao nchini Iran.Tunaweza kuzungumza

nao ili majasusi hao waweze kumsaidia Abu Zalawi.Abu ni mgeni wa jiji la Tehran na kama angeweza kumpata mwenyeji ambaye angemsaidia katika kufanikisha baadhi ya mambo ingemrahisishia sana shughuli yake.Unaonaje wazo hilo la kuwaomba msaada Mossad? akauliza David.Jason akainamisha kichwa akafikiri kidogo halafu akasema

“Ninakubaliana na wazo lako David lakini sina uhakika kama Mossad wanaweza kukubali kutusaidia katika operesheni hii.Kuna msuguano

ulitokea hapa kati kati baina yetu hivyo basi mahusiano yetu na Mossad si mazuri kwa sasa” akasema Jason

“Jason kwa namna yoyote ile lazima tumsaidie Abu Zalawi kule Iran.Hatuna majasusi wetu Iran na hatuwezi kuingiza majasusi wetu kule lakini Israel ambao ni washirika wetu wakubwa wana majasusi wao Iran ambao tunaweza kuwatumia kumpa msaada Abu Zalawi ili aweze kukamilisha jukumu tulilomtuma kule” akasema David

“David kuna jambo lilitokea na kuzorotesha mahusiano yetu na Mossad.Kuna wakati walihitaji kufahamu mahala alipo Ammar Nazari na wakaomba msaaada kwetu lakini sikuwa tayari kuwasaidia kuwapa taarifa za mahala alipo Ammar Nazari kwa kuwa tulikuwa na mtu wetu katika kundi hilo aliyekuw akatika operesheni maalum.Baada ya kuwakatalia kuwapa taarifa za mahala alipo Ammar,Mossad walifanya jitihada zao wenyewe na kufanikiwa kufahamu mahala

anapojificha Ammar na wakamuua kwa bomu.Toka wakati huo mahusiano yetu nao si mazuri” akasema Jason

“Pamoja na mashirikiano kutokuwa mazuri lakini si vibaya kama tukiwajaribu.Endapo watakataa kutusaidia tutaangalia washirika wetu wengine.Tunao washirika kadhaa wanaoweza kutusaidia lakini tunapenda kufanya kazi na Mossad kwa kuwa majasusi wake wana umahiri mkubwa sana.Jaribu kuwasiliana na mkurugenzi wa Mossad ili

tuone kama wanaweza kutusaidia” akashauri David.Kwa kufuata ushauri wa David,Jason akachukua simu na kumpigia Moshe Levine mkurugenzi wa Mossad

“Jason habari za siku?akauliza Moshe Levine mkurugenzi wa Mossad baada ya kupokea simu

“Huku tunaendelea vyema kabisa”akajibu Jason

“Nafuarhi kusikia hivyo.Poleni kwa shambulio la Dar es salaam” akasema Moshe

“Ahsante Moshe.Samahani kwa kupiga muda huu lakini nimekupigia kukuomba msaada wako.Nafahamu hatuna mashirikiano mazuri kwa siku za hivi karibuni lakini CIA na Mossad tumekuwa marafiki na kushirikiana kwa muda mrefu hivyo nashauri tusahau yale yaliyopita na tuanze tena mashirikiano mapya baina yetu” akasema Jason

“Nini unahitaji Jason? Akauliza Moshe

“Nafahamu unao watu wako jijini Tehran”

“Ndiyo ninao watu watu wangu Tehran” akasema Jason

“Nahitaji msaada wako Moshe.Kuna operesheni kubwa sana tunaiendesha kule Tehran.Kuna mtu wetu tumemtuma huko katika misheni ya muhimu sana.Ninahitaji watu wako kule Tehran wamsaidie huyo mtu wetu aweze kufanikisha misheni yake” akasema Jason

“Jason unaweza ukanifafanulia ni operesheni gani inaendelea huko Iran? Akauliza Moshe na Jason akamueleza Moshe kuhusiana

na misheni ile wanayotaka kuifanya nchini Iran.

“Jason kwanza nashukuru kwa kuniamini na kunieleza kuhusiana na mpango wenu unaoendelea nchini Iran.Mossad tuna watu wetu Tehran na hakuna tatizo katika kumsaidia huyo mtu wenu kufanikisha misheni mliyomtuma kwani misheni hiyo ni muhimu pia kwa taifa la Israel kwani tumekuwa tukipokea vitisho vingi kutoka Iran.Hata hivyo kuna tatizo”akasema Moshe

“Tatizo gani Moshe? akauliza Jason

“Sina hakika kama huyu mtu mnayemtumia katika operesheni hiyo Abu Zalawi mnamfahamu vyema” akasema Moshe.Jason akamtazama David

“Kuna nini kuhusu Abu Zalawi? Akauliza Jason

“Huyu mtu mnamfahamu vyema?

“Moshe unaonyesha wasi wasi mkubwa.Unamfahamu Abu Zalawi? Akauliza Jason

“Ndiyo Jason.Ninamfahamu Abu

Zalawi kiundani ndiyo maana ninasema kuna tatizo” akajibu Moshe na Jason akashusha pumzi

“Kabla sijawaeleza chochote, ilikuaje mkachagua kumtuma Abu Zalawi kazi hii nyeti? Akauliza Moshe

“Tulihitaji mtu ambaye ni Gaidi kwa ajili ya kazi hii na tulipompata Abu Zalawi ilitulazimu kwanza kujiridhisha kama anafaa tukampa mtihani akaufaulu vizuri ndipo tulipomtuma kwenda Iran.Kuna tatizo gani

kuhusu huyu mtu?akauliza Jason

“Nina wasiwasi mnamtumia mtu ambaye hamumfahamu vyema na ndiyo maana nasema lipo tatizo.Abu Zalawi si gaidi kama mlivyojulishwa”akasema Moshe Levine

“Si gaidi? Ki vipi Moshe? Akauliza Jason akionekana kustuka kidogo

“Jina lake halisi ni Mathew Mulumbi.Ni jasusi anatokea Tanzania” akasema Moshe na nusura simu imponyoke Jason kwa mstuko alioupata

“Sijakuelewa Moshe unachokizungumza” akasema Jason

“Huyu mtu mnayemfahamu kama Abu Zalawi jina lake halisi ni Mathew Mulumbi na ni jasusi anayetokea Tanzania” akasema Moshe Levine na kumsimulia Jason kila kitu kuhusu Mathew Mulumbi toka alivyovamia ubalozi wa Israel jijini Nairobi na kumtorosha Edger kaka na hadi walivyofanikiwa kumkamata na kumfunga kwa miaka mitatu nchini

Israel.Jason akahisi kuanza kuloa jasho.Moshe akaendelea

“Kwa muda mrefu tumekuwa tukimtafuta mfadhili mkuu wa vikundi vya wanamgambo wanaopambana na Israel ambaye anafahamika kama Habiba Jawad.Mathew naye alikuwa katika mpango huo akatushawishi tuungane naye katika kumsaka Habiba na ndipo tulipokuja na mpango wa kumuunganisha Mathew na Ammar Nazari kiongozi wa kundi la Ammar Nazari Brigades aliyekuwa anashikiliwa gerezani na

ambaye kundi lake lilikuwa linafadhiliwa na Habiba.Hapo ndipo jina la Abu Zalawi lilipoanza.Hili ni jina ambalo tulimpa alitumie kwa ajili ya kujenga ukaribu na Ammar Nazari na vile vile tukamuweka katika mtandao wetu kama mtu tunayemtafuta.Mathew alifanikiwa kumtorosha Abu Zalawi gerezani na kujiunga naye na baada ya hapo hatukuwahi kupata mrejesho wowote kutoka kwake hadi tulipofanikiwa kumuua Ammar.Mathew aliibuka tena na tayari alikwisha onana na

Habiba Jawad ambaye alimtuma kuja Israel kumchukua mwanae Edger Kaka tuliyekuwa tunamshikilia.Tulimkabidhi mwili wa Edger Kaka akapotea na hatukupata tena mrejesho kutoka kwake hadi tulipopata taarifa kuwa amehusika katika shambulio la bomu katika ubalozi wa Marekani jijini Dar es salaam.Yawezekana hayo yote hamkuwa mkiyafahamu kuhusu huyu jamaa mnayemtumia katika hiyo misheni yenu muhimu sana”

akasema Moshe.Jason akavuta pumzi ndefu kisha akasema

“Moshe umetufumbua macho.Ni kweli hatukuwa na taarifa zozote za kuhusiana na huyu mtu.Tunachokifahamu sisi ni kwamba anaitwa Abu Zalawi raia wa Saudi Arabia.Nimestuka kusikia kwamba jina lake ni Mathew Mulumbi na ni raia wa Tanzania.Moshe ahsante sana kwa taarifa hii ambayo imenichanganya sana.Ninaomba nikupigie baadae kidogo” akasema Jason

na kukata simu akatazamana na David

“David nini hiki kinachoendelea? akauliza Jason na kumpa David maelezo yote aliyopewa na Moshe Levine mkurugenzi wa Mossad.

“Kweli hii ni taarifa ya kustusha mno.Hakuna mtu yeyote aliyefahamu kitu kama hiki.Tumeletewa huyu mtu na Habiba ambaye tunamuamini na tumeshirikiana naye kwa muda na akatupa taarifa zake kuwa ni gaidi na anaitwa Abu Zalawi.Tunamuamini Habiba

Jawad hivyo hakuna aliyekuwa na wasiwasi hata kidogo kuhusiana na mtu aliyetuletea” akasema David Walker ukapita ukimya mfupi halafu Jason akasema

“Habiba ametuchezea mchezo mbaya sana ! akasema Jason kwa hasira

“Ni jambo la kustusha mno”

“Baada ya kulifahamu jambo hili nini tunafanya David? akauliza Jason

“Imekuwa bahati mbaya sana tumelifahamu jambo hili katikati ya misheni na wakati

ambao tayari Abu anaelekea Iran na hatuna namna tena ya kuweza kumzuia asiendelee na misheni hii.Jason kwa sasa sina hakika kama kuna kitu tunachoweza kukifanya.Tumuache tu aendelee na misheni yetu tena kama ni jasusi itakuwa vizuri zaidi kwani atafanya kazi kwa ufanisi mkubwa sana” akasema David Walker

“David,mtu huyu kama alivyosema Moshe tumekosea sana kumpa misheni kubwa kama hii.Tulipaswa kumchimba Abu Zalawi

mapema na kumfahamu kiundani kabla ya kumtuma kazi.Tulikosea mno” akasema Jason

“Ni kweli Jason.Nikiri tulikosea sana kutokufanya uchunguzi wa kina kuhusu Abu Zalawi kabla ya kumkabidhi misheni hii lakini hii ilisababishwa na imani kubwa tuliyo nayo kwa Habiba Jawad.Tuliamini mtu aliyetuletea hana tatizo lolote kwani amekuwa akitusaidia kupata watu kwa ajili ya shughuli mbali mbali na hakujawahi kutokea tatizo

lolote hadi sasa.Ushauri wangu tumuache Abu Zalawi aendelee na misheni hii kwani tayari amekwisha piga hatua kubwa” akasema David Walker

“Hapana David hatuwezi kumuacha akaendelea na misheni hii na wala misheni yenyewe haipaswi kuendelea.Tunasimamisha kila kitu ! akasema Jason na kumfanya David apatwe na mshangao

“Jason wewe ni mkuu wangu na ndiye mwenye maamuzi ya mwisho kuhusiana na misheni zote

tunazozifanya lakini katika hili siwezi kukubaliana nawe hata kidogo.Tumekwisha tumia gharama kubwa sana kwa ajili ya kuandaa operesheni hii na tayari tumefika nusu yake hatuwezi kuishia hapa.Lazima tuendelee hadi pale tutakapotimiza lengo letu.Kumbuka damu za watu zimemwagika kwa sababu ya misheni hii,hatuwezi kuishia hapa! Tumekaribia sana kufika pale ambapo tumekuwa tunapatafuta kwa miaka mingi” akasema David

“David nakubaliana nawe kwamba imetugharimu fedha na damu kuandaa misheni hii lakini hatuwezi kuendelea nayo tena.Madhara yake ni makubwa sana kama ikiendelea ukilinganisha na gharama ambazo tumetumia.Huyu jamaa ambaye tayari tumefahamu anaitwa Mathew Mulumbi ni mtanzania.Hamuoni hatari iliyopo kuendelea kumtumia? Ni vipi kama tayari anafahamu mambo tuliyoyafanya kule Tanzania? Sikuwepo wakati mkizungumza naye lakini

nataka nifahamu kutoka kwako kwani ni wewe uliyeongoza mahojiano naye kuna chochote mlimwambia kuhusiana na kile tulichokifanya Tanzania? Akauliza Jason na David akaanza kukumbuka.

“Eneo la Afrika Mashariki hivi sasa liko katika machafuko makubwa sana ya kidini.Kinachoendelea kule ni moja ya mipango yetu na kwa kuwatumia IS tumeweza kufanikisha kuibuka kwa machafuko makubwa sana ya kidini ambayo yamepelekea

Marekani kupeleka vikosi vyake.Hapa unaweza ukaona ni namna gani Marekani inafaidika kutokana na makundi ya kigaidi.Tumewatumia IS kutengeneza vurugu zile na sasa Marekani inafaidika kwa mafuta mengi kutoka Uganda.Meli za Marekani zimepanga foleni zinapishana kujaza mafuta ,akiba yetu ya mafuta inaongezeka.Hii yote ni kazi ya timu hii unayoiona humu ndani na ni mfano wa mafanikio makubwa ambayo

yanapatikana kwa kuwatumia magaidi”

Sura ya David walker ikabadilika baada ya kumbu kumbu hii kumjia.

“Kuna kitu umekikumbuka David?akauliza Jason

“Ndiyo Jason.Kuna kitu nimekikumbuka.Katika mazungumzo yetu tulimueleza Abu Zalawi kila kitu tunachokifanya bila kumficha tukiamini yeye ni gaidi na ni raia wa Saudi Arabia.Hatukujua kama ni jasusi tena raia wa Tanzania.Tulifanya kosa”

akasema David na ukimya ukapita

“Mlimweleza chochote kuhusiana na mpango wa kusambaza kirusi Tanzania? Akauliza Jason

“Hapana mpango huo umekuja baada ya yeye kuondoka Marekani.Hafahamu chochote kuhusu mpango huo lakini anachokifahamu ni kuwa,sisi tukiwatumia magaidi wa IS tumechochea vurugu za kidini zilizotokea Tanzania kwa lengo la kujipatia mafuta.Nilikuwa mjinga sana kumweleza jambo

hili ! akasema David kwa masikitiko

“David nadhani sasa umeona wewe mwenyewe kwa nini ninasema misheni hii lazima isimamishwe haraka sana bila kujali utekelezaji wake umefika hatua gani.Abu Zalawi au Mathew Mulumbi kama anavyojulikana hapaswi kuendelea na misheni hii.Tayari anafahamu kuwa ni sisi tulio nyuma ya machafuko yale yaliyotokea Tanzania lakini bado akakubali kufanya kazi tuliyomtuma akaifanye hudhani kuna kitu huyu jamaa

anapanga kukifanya? Kwa mujibu wa Moshe huyu ni mmoja wa majasusi hatari kabisa na kwa miaka mitatu alikuwa katika mateso makali na hakuwahi kufungua mdomo wake kusema chochote.Japokuwa amekubali kuifanya kazi yetu kama vile hakuna chochote kilichotokea lakini hatuwezi kujua moyoni mwake nini anakiwaza.Tumefanya kosa kubwa sana David" akasema Jason

"Yote haya ameyataka Habiba Jawad.Yeye ndiye

aliyemleta huyu mtu na akatuaminisha kwamba ni mtu sahihi anayeweza kuifanya operesheni hiyo kwa ukamilifu.Kwa nini akamchagua Abu Zalawi? Hapo ndipo tunapaswa kuanzia” akasema David

“Unadhani Habiba Jawad alimfahamu Abu Zalawi ni nani lakini bado makusidi kabisa akaa mua kumleta kwetu tumtumie? Akauliza Jason

“Ninahisi hivyo.Alimleta kwetu mtu ambaye naamini alimfahamu fika ni nani na

ninahisi alifanya hivyo kwa sababu maalum ambayo hatuijui”

“Tumeshirikiana na Habiba Jawa kwa muda mrefu toka mume wake alipofariki na tumemuwezesha kuwa na utajiri mkubwa mno,unadhani anaweza kuwa na mpango wowote wa siri dhidi yetu? Akauliza Jason

“Tutamfanyia uchunguzi kulifahamu hilo lakini kwa sasa ni kutafakari kuhusu hatua za haraka za kuchukua kuhusiana na misheni hii na

huyu jamaa Abu Zalawi” akasema David

“Kama nilivyosema awali kwamba kwa namna yoyote ile Abu Zalawi hapaswi kuendelea na misheni hii nyeti”akasema Jason

“Hivi sasa naamini Abu atakuwa njiani akielekea Iran.Ndege aliyomo imepotea haionekani na hatuna namna ya kuweza kumpata hadi atakapokuwa ameingia Iran,ndiyo maana nilishauri kwamba aendelee na misheni yake kama kawaida na kama tukif……”

“David huyu mtu hapaswi kuendelea na misheni yetu yoyote.Huyu mtu ni bomu na siku moja atatulipukia.Tayari anafahamu sisi ndiyo sababu ya mamia ya watu kupoteza maisha Tanzania na yawezekana miongoni mwa waliofariki ni ndugu zake,unadhani akisikia tena kitakachotokea Tanzania baada ya kirusi kusambazwa nini atatufanya? Ni wazi anaweza akageuka na kuwa adui yetu mkubwa.Huyu mtu tayari amekuwa mzigo kwetu na kitu pekee ambacho

tunapaswa kukifanya kwa sasa ni kutafuta namna ya kumuua kabla hajaanza kufanya chochote nchini Iran” akasema Jason

“Tuliwaomba msaada Mossad ili majasusi wao walioko nchini Iran wamsaidie Abu Zalawi tunaweza kubadili badala ya kumsaidia mpango uwe ni kumuua” akasema David

“Nadhani itatulazimu kufanya hivyo.Japo nakubali tumefika hatua nzuri lakini mtu tuliyemtumia si mtu sahihi na hatuwezi kuendelea

naye.Tunapaswa kummaliza haraka sana kisha tutaanza kujipanga tena upya namna nyingine.Vile vile tumchunguze Habiba Jawad tujue kama alimfahamu Abu Zalawi ni nani lakini bado akamleta kwetu ili tumtumie.Tuchunguze mahusiano yao.Habiba anapaswa ahojiwe kwa kina kuhusiana na huyu jamaa” akasema Jason halafu akachukua simu na kumpigia Moshe Levine mkurugenzi wa Mossad

“Moshe nimekupigia tena kuomba msaada wako.Kwanza ninakushukuru kwa kutufumbua macho kuhusu Abu Zalawi.Hatukuwa tukimfahamu ni nani huyu mtu na baada ya kumfahamu tumeamua kukatisha misheni tuliyomtuma akaifanye Iran” akasema Jason Washington

“Ni maamuzi mazuri mmeyafanya Jason,kwani huyu jamaa si mtu sahihi kwa misheni hii na hata sisi mpaka leo hii tunajilaumu mno kwa kuamua kushirikiana naye.Ameturejesha nyuma

mno katika jitihada zetu za kumsaka Habiba Jawad.Tulidiriki hata kumuachia Ammar Nazari ambaye ni mtu hatari sana kwa Israel tukitegemea kupata matokeo lakini hatujapata chochote mpaka sasa.Huyu mtu anatakiwa aondolewe haraka iwezekanavyo ! akasema Moshe Levine

“Ndiyo maana nimekupigia Moshe ili kukuomba tushirikiane tuweze kuumuondoa Abu Zalawi haraka sana kabla hajafanya

chochote nchini Iran” akasema Jason

“Nina watu wangu jijini Tehran ambao wakatekelea mpango huo wa kumuua Abu Zalawi lakini kuna kitu tutakihitaji kutoka kwenu CIA” akasema Moshe Levine

“Nini unakihitaji Moshe? Akauliza Jason

“Ninataka kupata taarifa za mahala alipo Habiba Jawad”akasema Moshe

“Habiba Jawad? Akauliza Jason kwa mshangao

“Ndiyo.Tutahitaji kujua mahala alipo” akajibu Moshe

“Hatuna taarifa zozote za kumuhusu Habiba Jawad” akasema Jason

“Jason nimewaambia hivyo kwa sababu nafahamu mnazo taarifa za kumuhusu Habiba Jawad.Tunafahamu Abu Zalawi amekutana na Habiba Jawad na kama mmeweza kukutana na Abu Zalawi mkamtuma katika misheni yenu lazima mnafahamu alipo Habiba Jawad.Tunamuhitaji sana Habiba Jawad hivyo tupeni taarifa za mahala alipo na sisi tuwatumie watu wetu

kumuondoa Abu Zalawi” akasema Moshe Levine.

“Moshe nitakupigia baadae kidogo tuzungumze kuhusu suala hili” akasema Jason Washington na kukata simu akapiga meza kwa hasira

“Aaaaghh !! akasema kwa hasira

“Mossad wanataka tuwape taarifa za Habiba Jawad ndipo watusaidie kumuonda Abu Zalawi! Akasema Jason

“Wamefahamuje kama tunafahamu alipo Habiba Jawad?akauliza David

“Ni kwa sababu ya Abu Zalawi.Wanafahamu amekuwa akishirikiana na Habiba Jawad hivyo basi kitendo cha sisi kumtumia katika misheni yetu kinawafanya waamini kwamba tunafahamu mahala alipo Habiba Jawad.David jambo hili linazidi kuwa kubwa” akasema Jason

“Jason kwa namna yoyote ile hatuwezi kuwapa Mossad taarifa za Habiba Jawad.Hawapaswi kufahamu kama tumekuwa tukishirikiana naye.Hii ni siri yetu kubwa ambayo hata Rais wetu haijui

hivyo hatuwezi kuianika kwa mtu mwingine yeyote hasa hasa Mossad” akasema David

“Lakini tunahitaji kumuondoa Abu Zalawi haraka sana na ni Mossad pekee wanaoweza kutusaidia katika hilo kwani tayari wanao majasusi wao jijini Tehran.David tukubali Mossad wametubana katika kona.Tunahitaji kuzungumza nao vizuri katika jambo hili.Tukichelewa tunaweza kumkosa Abu Zalawi kwani tayari tumekiwsha mtengenezea mazingira

mazuri ya kuweza kupokelewa bila tatizo nchini Iran na anaweza akageuka kuwa mwiba kwetu na kutuchoma.Hatupaswi kumpa nafasi lazima tuhakikishe anauawa haraka sana ikiwezekana kabla hajakanyaga ardhi ya Iran.Sidhani kama kuna haja ya kubishana na Mossad.Hakuna sababu ya kumficha Habiba Jawad kwani ni yeye ndiye aliyesababisha haya yote yakatokea" akasema Jason

“Habiba ni mtu anayefahamu mambo yetu mengi kwani tumeanza kushirikiana naye kwa muda mrefu.Ni mtu ambaye hatuwezi kumtoa kirahisi kwa Mossad.Lakini kwa kuwa na sisi tunahitaji msaada wao basi tunaweza kufanya kitu kimoja.Tukubaliane nao kwamba wamuue Abu Zalawi na sisi tumuue Habiba Jawad.Tunao uwezo wa kumpata Habiba na kumuua hivyo tufanye kazi hiyo sisi wenyewe ili wasije wakagundua mashirikiano

yetu na Habiba” akasema David.

“Hilo ni wazo zuri David” akasema Jason kwa sauti ndogo kisha ukimya ukapita

“Lakini kwa nini tumuue Habiba Jawad? Amekuwa nasi kwa muda mrefu na ametusaidia mambo mengi.Je hatumuhitaji tena? Akauliza David

“Habiba Jawad ndiye aliyetufikisha hapa tulipofika.Ametufanya tukaingia katika misheni ambayo ni sawa na kujifunga kitanzi shingoni sisi wenyewe

baada ya kumleta kwetu Abu Zalawi ambaye si gaidi bali ni jasusi.Naamini hakufanya hivi kwa bahati mbaya nahisi kuna jambo wanalipanga kati yake na Abu Zalawi hivyo lazima tuwaondoe wote mara moja ili tuendelee kuwa salama.Nakuhakikishia David bila kuwaondoa watu hawa wawili hatutakuwa salama.Usihofu kuhusu utajiri tuliomuwezesha Habiba,tutatafuta mtu mwingine wa kumuwezesha na akatufanyia kazi nzuri kuliko hata Habiba" akasema Jason

lakini David alionekana kuzama katika lindi la mawazo.

“Jason nadhani suala hili lifike kwanza kwa G20 ili yafanyike maamuzi.Hili jambo ni kubwa mno hatuwezi kufanya maamuzi sisi wawili pekee wakati tunao wenzetu wengine.Ikiwezekana kura inaweza kupigwa kuamua jambo hili.Nitawakusanya ndani ya muda mfupi asubuhi ya leo kisha nitaliwasilisha kwao jambo hili watalitafakari na kulifanyia maamuzi na pengine wanaweza wakawa na

mawazo mengine mazuri zaidi” akasema David

“Sawa David nenda kakutane na wajumbe hao mzungumze na jibu lipatikane haraka sana ili tujue namna ya kulishughulikia jambo hili”akasema Jason na David akaondoka kwenda kufanya maandalizi ya kukutana na wajumbe wa kikundi chao cha G20 kwa ajili ya kulijadili suala lile nyeti lililojitokeza

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Bado macho ya SNSA yalielekezwa katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere wakiendelea kufuatilia kila kinachoendelea pale uwanjani.Ilipofika saa sita na dakika saba yakasikika maongezi kati ya rubani wa ndege na waongoza ndege wa uwanja wa Julius Nyerere.Ilikuwa ni ndege ya jeshi la Marekani ikiomba kutua katika uwanja huo ikiwa imeleta mahitaji mbalimbali

kwa ajili ya vikosi vya jeshi la Marekani vilivyoko Tanzania.

Dakika chache baadae ndege ya jeshi la Marekani ikatua.

“Yawezekana ndege iliyoleta kirusi ni hii kwani imefika kwa muda ule ule ambao tulitarajia ndege iliyombeba Sattar ingewasili” akasema Gosu Gosu

“Tuendelee kufuatilia tutajua kama ni hii” akasema Ruby akionekana kuwa na wasiwasi

Dakika chache toka kuwasili kwa ndege ile

ukawasili msafara wa magari ya vikosi vya jeshi la Marekani vilivyopo Tanzania na kazi ya upakuzi wa mizigo katika ndege ile ikaanza.

“Inaonekana ni mizigo ya kawaida inayohusiana na wanajeshi” akasema Gosu Gosu

“Tuendelee kuchunguza” akasema Ruby wakati mizigo ikipakuliwa kutoka ndegeni na kuingizwa katika magari

“Hakuna dalili zozote za kuwepo Sattar au kirusi katika ndege hii ya mizigo” akasema Gosu Gosu lakini hakuna

aliyemjibu watu wote waliyaelekeza macho yao katika kamera wakifuatilia kile kilichokuwa kinaendelea pale uwanjani.Mizigo iliyokuwa katika ndege ile ilimalizika na magari yakajipanga kwa ajili ya kuondoka.Kiongozi wa msafara ule akatoa maelekezo na magari yakaanza kuondoka.

“Hakuna kirusi katika ndege hii.Hawa watu wametuc……” Akasema Gosu Gosu na Nawal akamkatisha

“Subiri kwanza Gosu Gosu.Kuna magari manne

yamebaki uwanjani.Mnadhani kwa nini yamebaki? Akauliza Nawal

“Ni kwa sababu bado kuna kitu wanakisubiri.Yawezekana wanamsubiri Sattar Sayf Al Din” akasema Nawal

“Nawal yuko sahihi.Hawa jamaa wanaonekana kuna kitu wanakisubiri.Tuendelee kuwafuatilia tujue kile wanachokisubiri” akasema Ruby

“Lakini mbona hakuna dalili zozote za kuwepo Assad Ismail hapa uwanjani?Tulielezwa kwamba

yeye ndiye atampokea Sattar Sayf Al Din” akasema Gosu Gosu

“Relax Gosu Gosu” akasema Ruby

Magari manne ya vikosi vya jeshi la Marekani yaliendelea kubaki pale uwanjani na kwa namna walivyokaa walionekana kuna kitu wanakisubiri.

Dakika ishirini baadae yakasikika mazungumzo kati ya waongoza ndege wa uwanja wa Julius Nyerere na Rubani aliyekuwa akiomba kutua katika uwanja huo wa ndege

“Hii lazima itakuwa yenyewe ! akasema Nawal

Dakika chache baadae ndege ikatua na magari yale ya jeshi la Marekani yaliyokuwa yamebaki yakisubiri yakaanza kuijongelea ndege ile.

“Hii si ndege ya jeshi la Marekani.Hii ni ndege inayotumiwa na CIA kupeleka maafisa wake sehemu mbali mbali duniani”akasema Nawal baada ya ndege ile kutua.

“Hii inatupa uhakika kwamba ndege hii yawezekana ndiyo imeleta kirusi”akasema Ruby

Magari yale yalisogelea ndege ile ambayo mlango wake ulifunguliwa na baadhi ya maafisa wa jeshi wakaingia ndani.Baada ya muda wakatoka wakiwa wameongozana na mtu mmoja aliyebeba masanduku mawili.Wote mle ndani sura zao zikaonyesha mabadiliko baada ya kumshuhudia Yule mtu aliyekuwa amebeba masanduku mawili akiwa ameongozana na maafisa wa jeshi la Marekani kuwa ni Sattar Sayf Al Din

“Hatimaye kirusi kimefika Tanzania” akasema Nawal

Sattar Sayf Al Din aliongozwa hadi katika mojawapo ya magari yale na kuondoka pale uwanjani.

“Nini kinafuata baada ya kujiridhisha kuwa Sattar ameingia nchini na muda wowote wanaweza wakasambaza kirusi?akauliza Gosu Gosu

“Huyu Sattar Sayf Al Din ni mtu ambaye lazima watamchunga sana kwani amebeba kitu hatari mno hivyo basi nina uhakika

watampeleka katika sehemu maalum watamlinda hadi watakapomkabidhi kwa Assad Ismail kwa ajili ya kuanza kazi ya usambazaji wa kirusi” akasema Nawal

“Sattar yuko katika mikono ya vikosi vya Marekani na yawezekana akapelekwa katika kambi yao akahifadhiwa huko na itatuwia ugumu kwetu kuweza kumpata.Lazima tuje na mpango kabambe wa kutuwezesha kuingia katika kambi ya jeshi la Marekani na hatimaye kumfikia Sattar na

kuchukua kirusi” akasema Ruby

“Nina wazo” akasema Nawal

“Ninyi mna mawasiliano ya karibu na Rais wa Tanzania? Akauliza Nawal

“Ndiyo tuna ukaribu mkubwa na Rais” akajibu Ruby

“Vizuri.Basi italazimu kumshirikisha Rais katika jambo hili” akasema Nawal

“Hapana hatuwezi kumshirikisha Rais katika hatua hii.Ni mapema mno.Tutamjulisha Rais baada

ya kukipata kirusi” akasema Ruby

“Ruby nisikilizeni” akasema Nawal

“Tayari tuna uhakika kwamba Sattar Sayf Al Din ameingia hapa nchini na tumemuona akiwa na masanduku mawili ambayo tunaamini kirusi kimo ndani yake.Ili tuweze kujua nyendo zote za Sattar na mipango yake yote ya kukisambaza kirusi hicho ikiwa ni pamoja na kujua mahala alipo Assad Ismail lazima kuingia katika vikosi vya Marekani .Kwa ninyi

itakuwa vigumu kwa sababu si wamarekani lakini mimi ni mmarekani hivyo inaweza kuwa rahisi kwangu.Tufanye hivi,tuonane na Rais na aelezwe kila kitu kuhusiana na kirusi hicho na kitu ambacho tutamtaka akifanye ni kumuita kamanda wa vikosi vya Marekani vilivyoko hapa nchini na atanikabidhi mimi kwake akidai kwamba nimeokolewa na vikosi vya Tanzania kutoka katika mikono ya watekaji.Nitajitambulisha kama mpiga picha wa

kujitegemea niliyekuja kutembea Tanzania na nikajikuta nimekwama katikati ya machafuko nikatekwa hadi nilipookolewa na vikosi vya jeshi la Tanzania nikapelekwa Dar es salaam.Nikisha kabidhiwa kwao naamini watanipeleka katika kambi yao ambako nitaanza kufanya uchunguzi kuhusiana na mahala alipo Sattar na kujua mipango yote ya kuhusiana na usambazaji wa kirusi huku nikiendelea kuwasiliana nanyi” akasema Nawal

“Nawal huo ni mpango wa hatari sana” akasema Ruby

“Ni kweli ni mpango wa hatari sana lakini lazima tuufanye kwani ndio pekee utakaotuwezesha kukifuatilia kirusi na kuzuia mpango wa kukisambaza” akasema Nawal

“Gosu Gosu una ushauri gani?Ruby akauliza

“Mimi naona wazo la Nawal ni zuri tulifanyie kazi ili aweze kuingia katika kambi ya vikosi vya Marekani kumfuatilia Sattar,lakini nina hofu endapo Rais akifahamu kuwa Marekani wako nyuma

ya haya yote yanayoendelea hapa nchini anaweza akapandwa na hasira na kuvitaka vikosi vya Marekani vindoke haraka sana na hivyo tukashindwa kukamilisha operesheni yetu” akasema Gosu Gosu

“Anachokisema Gosu Gosu ni kitu cha kweli.Tunapaswa kuwa makini sana tunapoamua kumueleza Rais kuhusu jambo hili.Nashauri tumuombe Rais akukutanishe na mkuu wa vikosi vya Marekani hapa nchini bila kumueleza chochote

kuhusiana na operesheni wanayoiendesha Marekani hapa nchini hadi hapo tutakapokuwa tumepata taarifa za kutosha” akasema Ruby wakajadiliana kwa muda wakakubaliana halafu Ruby akampigia simu Dr Fabian Kelelo akamuomba waonane kwa ajili ya suala muhimu na Dr Fabian akamtaka aende ikulu.

Kutoka ofisi kuu za SNSA hadi ikulu si mbali hivyo iliwachukua dakika kama kumi kufika ikulu

“Ruby karibu sana.Mnaendeleaje huko katika idara yenu?akauliza Dr Fabian baada ya akina Ruby kuwasili

“Tunaendelea vyema mheshimiwa Rais” akasema Ruby na kunyamaza kidogo halafu akasema

“Mheshimiwa Rais huyu anaitwa Chloe Bennet anatokea Marekani” akasema Ruby na Nawal akasimama akaenda kumpa mkono Rais

“Karibu sana Tanzania Chloe” akasema Dr Fabian

“Ahsante sana mheshimiwa Rais” akasema Nawal

“Mheshimiwa Rais Chloe yuko hapa kwa jambo mahsusi.Kuna misheni muhimu anasaidiana nasi” akasema Ruby

“Naweza kufahamu ni misheni gani inayoendelea kati yenu na Chloe? Akauliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais ninaomba nisikwambie kwa sasa hadi hapo tutakapokuwa tumeikamilisha misheni hiyo”

“Ruby hapo ndipo huwa unaniudhi.Kila mara ninapokuuliza kinachoendelea SNSA jibu lako limekuwa hilo hilo moja kwamba huwezi kunieleza kwa sasa hadi hapo baadae?Kwa nini hutaki kuniweka wazi mambo gani yanayoendelea SNSA? Kuna ugumu gani kunieleza kile mnachokifuatilia? Don’t you trust me? Akauliza Dr Fabian kwa sauti ya ukali kidogo

“Ninakuamini mheshimiwa Rais” akajibu Ruby

“Kama unaniamini kwa nini unasita kunieleza ukweli wa kile kinachoendelea SNSA?Kwa nini unafanya siri?akaendelea kuuliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais ninakuomba unipe muda kidogo tu halafu nitakuja kwako na kukueleza kila kitu.Ni mambo mazito kidogo.Kwa mchana huu nimekuja kwako kuomba msaada” akasema Ruby.Dr Fabian akachukua kitambaa akafuta jasho usoni halafu akasema

“Ruby naomba nikuweke wazi kwamba sijapendezwa na tabia hii ya kunificha mambo yanayoendelea katika idara yako.Usisahau kwamba mimi ndiye mkuu wa SNSA hivyo napaswa kufahamu kila kinachoendelea katika idara hiyo.Nini unataka nikusaidie?akauliza Dr Fabian

“Ninahitaji huyu mwenzangu haa Chloe aunganishwe na vikosi vya jeshi la Marekani vilivyoko hapa nchini.kuna misheni ya muhimu sana tunataka kuifanya”akasema Ruby

“Ruby unanipa wakati mgumu sana.Hutaki kunieleza chochote kinachoendelea na wakati huo huo unataka nimuunganishe mwenzako na vikosi vya Marekani vilivyoko hapa nchini.Kuna nini mnataka kukichunguza? Akauliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais naomba uniwie radhi tena katika jambo hilo” akasema Ruby na Rais akagonga meza kwa hasira

“Ruby nimechoka nawe.Ninawezaje kukusaidia bila kujua kile mnachotaka

kukifanya kwa vikosi vya Marekani vilivyoko hapa nchini.Unachotaka nikifanye kinaweza kuharibu mahusiano mazuri yaliyopo baina yetu na Marekani.Tunauheshimu sana mchango wao mkubwa walioutoa.Mara tu vurugu zilipoibuka ni Marekani waliotuma vikosi vyao kwa haraka sana kuja nchini kushirikiana na vikosi vyetu.Unaponitaka nishirikiane nanyi kuweka pandikizi katika vikosi vya Marekani lazima unipe sababu ya msingi ya kufanya hivyo na

kama utaendelea na majibu yako ya kunieleza baadae sintakuwa na msaada kwako.Nitakuachia ufanye kazi zako wewe mwenyewe ! akafoka Dr Fabian

“Ruby kuna nini?akauliza Nawal ambaye hakufahamu kile walichokuwa wakikizungumza Dr Fabian na Ruby.

“Rais anahitaji kufahamu dhumuni la kutaka uingie katika vikosi vya Marekani” akasema Ruby

“Hakuna namna Ruby mueleze ukweli” akasema

Nawal.Ruby akafungua mkoba wake akatoa faili akalifunua na kutoa picha moja akampatia Rais

“Anaitwa Sattar Sayf Al Din.Huyu anatokea kundi la kigaidi la IS na yuko hapa nchini” akasema Nawal na kufungua picha za video akamuonyesha Rais namna Sattar alivyokuwa akishuka katika ndege

“Sijakuelewa Ruby.Umesema huyu mtu anatokea kundi la IS lakini hapa ninamuona akishuka katika ndege akiwa

ameongozana na maafisa kutoka jeshi la Marekani.Sielewi kinachoendelea hapa ! akasema Dr Fabian

“Ndiyo maana nikakuomba mheshimiwa Rais nipe muda kwani jambo hili ni kubwa na yawezekana nikikueleza leo hii usinielewe” akasema Ruby

“Make me understand ! akasema kwa ukali Dr Fabian halafu ukapita ukimya mfupi

“I’m sorry Ruby nimeshindwa kujizuia kukasirika lakini ninahitaji

sana kujua kile kinachoendelea hivi sasa.Kama huyu mtu ni gaidi kwa nini yuko na vikosi vya Marekani? Amekamatwa? Akauliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais mtu huyu kama nilivyokueleza ni gaidi na amekuja hapa nchini kwa ajili ya kutekeleza shambulio la kigaidi.Mheshimiwa Rais masanduku mawili uliyomuona ameyabeba wakati akishuka ndegeni yana kirusi ambacho amekuja kukisambaza hapa nchini”

“Kirusi? ! DrFabian akastuka

“Ndiyo mheshimiwa Rais”

“Kirusi cha aina gani hicho? Akauliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais naomba na mimi nizungumze kidogo.Kama Ruby alivyonitambulisha kwako ninaitwa Chloe Bennet ninatokea shirika la ujasusi la Marekani CIA.Tulipata taarifa za kuwepo kwa shambulio la kirusi hapa nchini Tanzania ambalo linategemewa kufanywa na kikundi cha kigaidi cha IS.Mtu ambaye

umeonyeshwa na Ruby muda mfupi uliopita ni kweli amekuja hapa nchini kwa ajili ya kutekeleza shambulio hilo.Kwa ufupi tu ni kwamba kirusi hicho ambacho kinatazamiwa kusambazwa ni kirusi hatari cha maangamizi makubwa na kinachoua ndani ya muda mfupi na husambaa kwa njia ya hewa.Mheshimiwa Rais mimi na wenzangu akina Ruby tunataka kuzuia shambulio hilo lisitokee lakini kwa bahati mbaya mtu ambaye amekuja kufanya shambulio hilo anapata hifadhi katika

kambi ya vikosi vya jeshi la Marekani ndiyo maana tumekuja kwako kuomba msaada wako ninataka uniunganishe na kamanda mkuu wa vikosi vya Marekani vilivyoko hapa nchini ili niweze kuingia katika kambi hiyo kufanya uchunguzi huku nikiwasiliana na wenzangu na kujua mipango yote inayopangwa kuhusiana na usambazaji wa kirusi hicho" akasema Nawal

"Mnazidi kunichanganya.Nataka kujua nani hasa anayetaka

kusambaza kirusi hicho?Ni gaidi huyu mliyenionyesha au ni wanajeshi wa Marekani? Akauliza Dr Fabian

“Kirusi kimepangwa kusambazwa na Sattar ambaye ni gaidi kutoka kundi la kigaidi la IS lakini anapata msaada kutoka kwa vikosi vya Marekani vilivyoko hapa nchini na ndiyo maana umeona katika video tulizochukua kutoka uwanja wa ndege wa Julius Nyerere Sattar akipokewa na maafisa kutoka vikosi vya jeshi la

Marekani walioko hapa nchini” akajibu Nawal

“Nini hasa sababu ya kutaka kusambaza virusi hivyo?akauliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais suala hili ni pana sana na ndiyo maana ninaendelea kusisitiza nipe muda nitakuja kwako na maelezo kamili ya kila kinachoendelea hapa nchini lakini kwa leo ninataka unisaidie hicho tulichokuomba.Ninataka kumpandikiza Chloe katika kambi ya vikosi vya Marekani ili aweze kuchunguza na kujua

mahala alipo Sattar na kirusi alichokuja nacho” akasema Ruby

“Ruby ninashindwa nifan…..” akasema Dr Fabian lakini Ruby akamkatisha

“Mheshimiwa Rais ninaomba uniamini katika hili.Najua kuna mambo mengi bado uko gizani na nitakuja hapa kwako kukueleza kila kitu lakini naomba kama hujawahi kuniamini basi niamini katika hili.Nchi iko katika hatari kubwa na ndiyo maana mimi na wenzangu tumeamua kufanya jambo hili la hatari

kubwa kwa ajili ya kuiepusha nchi na hatari iliyopo.Tunakuomba sana msaada wako mheshimiwa Rais” akasema Ruby

“Nini unataka nikifanye?akauliza Dr Fabian baada ya kutafakari kwa muda,Ruby akamuelekeza namna walivyoupanga mpango ule na kitu gani anatakiwa kufanya Dr Fabian.

Baada ya kupewa maelekezo ya kile anachotakiwa kukifanya bila kupoteza muda Dr Fabian akachukua simu akampigia

simu waziri wa ulinzi na kumpa maelekezo kwamba anamuhitaji mkuu wa vikosi vya Marekani vilivyoko nchini Tanzania haraka sana pale ikulu ana mazungumzo naye.

DAKIKA ISHIRINI BAADAE

Helkopta ya jeshi la Marekani iliyombeba Jeneral William Marshall mkuu wa vikosi vya jeshi la Marekani vilivyoko nchini Tanzania,ilitua katika viwanja vya ikulu jijini Dare s salaam.Hii ni kufuatia ombi la

Rais la kutaka kuonana na mkuu huyo.

Jenerali William akashuka katika helkopta akapokewa na walinzi wa Rais wakamuongoza kuelekea ndani kwa ajili ya kukutana na Rais.Akiwa amevaa sare za jeshi la Marekani alikaribishwa sebuleni na baada ya dakika kadhaa rais Dr Fabian akajitokeza akiwa ameongozana na Nawal.William akasimama na kutoa salamu ya kijeshi kwa Rais kisha Rais akampa mkono na kumkaribisha.

“Ahsante sana kwa kufika kwa haraka Jenerali William baada ya kupokea wito wangu” akasema Dr Fabian

“Nimeelekezwa na waziri wa ulinzi wa Tanzania ambaye tunawasiliana mara kwa mara kwamba unanihitaji mara moja hivyo nikalazimika kuacha kila nilichokuwa nakifanya nije nikusikilize mheshimiwa Rais” akasema Jenerali William

“Karibu sana Jenerali William.Kwanza kabisa ninataka kujua maendeleo ya vikosi vya Marekani hapa

nchini.Mnaendeleaje na majukumu yenu?

“Tunaendelea vizuri sana mheshimiwa Rais tukishirikiana na vikosi vya Tanzania na kwa kiasi kikubwa ninaweza kusema kwamba tumefanikiwa kudhibiti vurugu.Kwa sasa tunaendelea na doria za ardhini na angani kuhakikisha hakuna tena makundi yoyote yanayoleta uvunjifu wa amani” akasema William

“Tunawashukuru sana William kwa kazi kubwa mliyoifanya ya kuhakikisha

amani inarejea nchini.Hata hivyo kuna jambo lingine nimekuitia hapa mchana huu” akasema DrFabian na kumgeukia Nawal

“Anaitwa Chloe Bennet ni raia wa Marekani ambaye anajishughulisha na upigaji wa picha na wakati machafuko yalipoanza alikuwa katika mbuga ya Serengeti akipiga picha na akajikuta akinasa kati kati ya mapigano.Alitekwa na kundi la vijana akashikiliwa yeye na wenzake wanne raia wa Kenya hadi jana walipokombolewa na vikosi

vya jeshi na kuletwa hapa Dar es salaam.Nimekuita ili nimkabidhi kwako uhakikishe usalama wake kwa wakati huu ambapo hakuna ubalozi.Nilitaka kumsafirisha kurejea Marekani lakini Chloe akaniomba aendelee kubaki Tanzania kwani anategemea kuendelea na zoezi lake la upigaji wa picha pale vurugu zitakapokuwa zimemalizika.Ninamkabidhi kwako uhakikishe anakuwa salama na pale vurugu zitakapokuwa zimemalizika

basi ataendelea na kazi zake” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais ninakushukuru sana kwa msaada mkubwa uliomsaidia huyu mwenzetu nakuahidi atakuwa salama katika usimamizi wangu hadi pale vurugu zitakapokoma kabisa” akasema William

“Chloe nakutakia mapumziko mema na pale utakapokuwa tayari kwenda kuendelea na shughuli zako za upigaji picha njoo uniage tafadhali na ninakuhakikishia kwamba vifaa vyako vyote

vilivyopotea nitavigharamia utapata vipya” akasema Dr Fabian Nawal akasimama akamfuata

“Nakushukuru sana mheshimiwa Rais kwa msaada mkubwa ulionipatia.Ninakuhakikishia kwamba nitakapokuwa tayari kwenda kuendelea na shughuli zangu nitakuja kukuaga” akasema Nawal akimshukuru Rais halafu akaenda kusalimiana na William Rais akawaaga wakaondoka kuelekea katika helkopta ya jeshi la Marekani wakaingia

helkopta ikapaa na kuondoka maeneo ya ikulu.Dr Fabian akamfuata Ruby aliyekuwa katika sebule nyingine

“Tayari nimetekeleza ulivyoniomba na mwenzako amekwisha ondoka na mkuu wa vikosi vya Marekani vilivyoko hapa Tanzania.Ruby mna uhakika na hiki mnachotaka kukifanya?Akauliza Dr Fabian

“Ninakushukuru sana mheshimiwa Rais kwa kutusaidia jambo hili.Hii ni njia pekee ya kutuwezesha kuingia katika kambi ya jeshi

la Marekani na kumfuatilia Sattar na kuzuia mpango wa kusambaza kirusi hapa Tanzania" akasema Ruby

"Ruby nataka kufahamu kwa kina kuhusiana na hiki kirusi.Mna hakika kweli kuna kirusi kinataka kusambazwa hapa nchini? Akauliza Dr Fabian

"Kirusi kipo kweli mheshimiwa Rais na tunaendelea kukifuatilia ili kuzuia mpango wa kukisambaza" akajibu Ruby

"Ruby hili si jambo la kufanyia mchezo.Kama una

uhakika kuna kirusi hatari ambacho kinaweza kusababisha maangamizi makubwa hapa nchini tunatakiwa kuanza kujiandaa ili pale mpango wenu wa kuzuia kisisambazwe ukishindwa kufanikiwa tuwe na uhakika wa kuwakinga watu wetu” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais kwa sasa suala hili litabaki siri yetu na hatakiwi mtu mwingine yeyote kufahamu kwani inaweza kuzuka taharuki kubwa na kuvuruga uchunguzi wetu.Ninakuhakikishia

mheshimiwa Rais kwamba tutafanya kila lililo ndani ya uwezo wetu kuhakikisha kirusi hicho hakisambazwi hapa Tanzania" akasema Ruby

"Ruby ninataka kufahamu je vikosi vya Marekani vinahusika katika jambo hili? Akauliza Dr Fabian

"Mheshimiwa Rais kama nilivyokueleza awali kwamba hili ni jambo pana lakini nitakuja kukueleza kila kitu.Naomba nipe muda ninakuahidi nitakuja nikiwa na maelezo ya kutosha kuhusiana na jambo hili" akasema Ruby

lakini Dr Fabian akaonekana bado ana wasiwasi mwingi.Baada ya ukimya mfupi akasema

“Ruby umenitaka nikuamini katika suala hili na mimi ninalazimika kufanya hivyo lakini tambua ya kwamba maisha ya watanzania yako mikononi mwako hivyo kwa namna yoyote ile mpango huo wa kusambaza kirusi katika ardhi yetu haupaswi kufanikiwa.Umenielewa Ruby?akauliza Dr Fabian

“Nimekuelewa mheshimiwa Rais”akajibu

Ruby huku Dr Fabian akimtazama kwa wasiwasi

“Ruby please swear to me that you won’t let them win ! akasema Dr Fabian.Ruby akavuta pumzi ndefu na kusema

“Mr President I swear I wont let them win ! akasema Ruby

“Ahsante sana kwa kunihakikishia hilo Ruby.Narudia tena kukusisitiza kwamba maisha ya watanzania yapo mikononi mwako.Kama kuna msaada wowote utauhitaji muda

wowote hata kama ni vikosi vya jeshi nitaarifu na mimi nitakusaidia”

“Ahsante sana mheshimiwa Rais nitafanya hivyo” akasema Ruby kisha akaagana na Dr Fabian akaondoka kurejea katika ofisi zao

****

Helkopta iliyowabeba akina Nawal ilitua katika kambi ya jeshi ya vikosi vya Marekani iliyopo kandoni mwa bahari.Kulikuwa na kambi

mbili za vikosi vya Marekani jijini Dar es salaam,kambi moja kubwa ikiwa katika uwanja wa Uhuru ambako ndiko vifaa vyote vilikuwa vinahifadhiwa na kambi nyingine ilikuwa ufukweni mwa bahari ya Hindi.

Jenerali William alianza kushuka katika helkopta halafu akafuatiwa na Nawal wakaongozana kuelekea katika kontena lenye rangi nyeupe ambalo lilikuwa linatumiwa kama ofisi ya Jenerali William.Ndani ya kontena lile

kulikuwa na ubaridi wa kutosha kutokana na kiyoyozi.

“Chloe karibu sana.Hii ni ofisi yangu” akasema Jenerali William na kumkaribisha Nawal katika chumba cha kupumzikia.

“Pole sana Chloe kwa masahibu yote yaliyokukuta”

“Ahsante sana Jeneral nimekwisha poa” akajibu Nawal na mara wakaingia watu wawili na Jenerali William akamtambulisha Nawal kwao halafu akamuomba aendelee kupumzika kwani alikuwa na

mazungumzo na watu wale walioingia mle ofisini.Jenerali William alitoka na wale wanajeshi wawili Nawal naye akasimama na kutoka ndani ya kile chumba akachungulia nje akamuona Jenerali William na wale jamaa wakielekea sehemu nyingine.Haraka haraka akarejea katika kile chumba cha mapumziko na kuchukua simu aliyopewa SNSA akampigia Ruby

“Nawal ! akasema Ruby baada ya kupokea simu

“Ruby tayari nimekwisha ingia katika kambi yao iliyoko

ufukweni mwa bahari.Kwa sasa niko katika ofisi ya Jenerali Wiliam Marshall” akasema Nawal

“Safi sana Nawal.Una nafasi ya kufanya chochote kwa muda huu?

“Jeneral William ametoka na sifahamu atachukua muda gani kurejea,ninataka kutega kamera”

“Sawa Nawal.Hakikisha unategа kamera na kifaa cha kunasa sauti katika ofisi hiyo ili tuweze kunasa mazungumzo na kufuatilia kila

kinachoendelea hapo ofisini” akasema Ruby

“Ninataka nijitahidi nitumie nafasi hii ndogo niweze kutekeleza hilo” akasema Nawal na kukata simu akafungua begi lake dogo la mgongoni alilokuwa nalo akatoa vifaa fulani ambavyo ni kamera ya siri na kifaa kingine cha kunasa maongezi.Akaenda tena kuchungulia katika dirisha kama kuna mtu anaelekea upande ule lakini hakukuwa na mtu yeyote aliyekuwa anaelekea pande zile.Haraka haraka akaelekea

katika mlango uliokuwa umefungwa akausogelea akiwa amevaa glovu mkononi akakiminya kitasa mlango ukafunguka akaingia ndani ya ofisi.Mezani kulikuwa na kibao Gen.William Marshall.

“Hii ndiyo ofisi yake” akawaza Nawal kisha akatega kifaa cha kunasa mazungumzo chini ya meza,halafu akatega na kamera ya siri katika kabati la vitabu.Wakati akiendelea na kutega kamera ile ya siri mara akasikia vishindo vya mtu haraka haraka akaenda kujificha chini ya meza.Mlango

wa ofisi ya Jenerali Willium ukagongwa Nawal mwili ukamtetemeka.Mtu aliyegonga mlango akakiminya kitasa na kuufungua mlango akachungulia ndani halafu akaufunga mlango ule akaondoka zake.Haraka haraka Nawal akamalizia kutega kamera ile ya siri halafu akatoka kwa tahadhari kubwa akarejea mahala ambako aliachwa apumzike.Akachukua simu na kumpigia simu Ruby akamjulisha kwamba tayari amekwisha tega kamera na kile kifaa cha kunasa

maongezi.Tayari Ruby alikwisha anza kupata picha za kamera kutoka katika ile kamera aliyoitega Nawal.

Dakika tano toka Nawal atoke katika ofisi ya Jenerali William akasikia vishindo vya hatua za mtu na akajitokeza Jenerali William

“Samahani Chloe kwa kukuacha peke yako” akasema Jenerali William na kuketi sofani

“Bila samahani Jenerali William” akasema Nawal

“Mimi ndiye mkuu wa vikosi vyote vya Marekani

vilivyopo hapa Tanzania hivyo ninakuwa na mambo mengi ya kushughulikia” akasema Jenerali William

“Kwa kuwa hapa kambini ni sehemu yenye shughuli nyingi,utapelekwa katika nyumba ninakoishi mimi na utaishi nasi hapo hadi pale mambo yatakapotulia.Ubalozi wetu hapa Dar es salaam umelipuliwa hivyo sina sehemu nyingine ya kukupeleka zaidi ya mahala ninapoishi.Usihofu ni sehemu salama sana” akasema Jenerali William

“Ninashukuru sana Jenerali William kwa msaada huu mkubwa” akasema Nawal na Jeneral William akasimama

“Pale kambini utapatiwa kila utakachokihitaji.Mimi nitakuja jioni baada ya kumaliza shughuli zangu na tutapata wasaa wa kuzungumza zaidi” akasema Jenerali William akamuaga Nawal akaondoka.

Dakika chache baada ya Jenerali William kuondoka akaingia mwanajeshi mmoja akajitamblisha kwa Nawal kwamba ametumwa na

Jenerali William kumpeleka mahala anakoishi.Nawal akavaa begi lake la mgongoni kisha akaongozana na Yule mwanajeshi hadi katika gari la jeshi akaingia wakaondoka kuelekea anakoishi Jenerali William

****

Nawal alifikishwa katika makazi ya maofisa wa vikosi vya Marekani waliokuwa wakiishi katika mojawapo ya nyumba za wageni muhimu wa serikali.Alipokewa na

wahudumu ambao ni wanajeshi pia na tayari taarifa zake walikwisha zipata hivyo basi wakamuhudumia kwa chakula halafu akaenda kupumzika.Ilikuwa ni nyumba ya kifahari sana.Nawal akasimama dirishani akatazama nje kulikuwa na ulinzi mkali karibu kila kona ya jumba lile kulikuwa na mlinzi mwenye silaha,juu ya paa vile vile kulikuwa na wanajeshi wakilinda na katika geti la kuingilia ndani ya nyumba ile kulikuwa na ulinzi mkali na kila gari lililoingia

lilikaguliwa kama limebeba mlipuko

“Jumba la kifahari sana hili na lenye ulinzi mkali mno hata hivyo ulinzi huu hauwezi kunizuia kutekeleza jukumu langu.Lazima tukimbizane na muda na kuhakikisha tunafahamu mahala kilipo kirusi.Mpaka mapambazuko ya kesho lazima tayari tuwe na kirusi mkononi” akawaza Nawal halafu akachukua simu na kumpigia Ruby akamjulisha kuwa tayari amefika katika makazi ya maofisa wa jeshi la Marekani.

“Tumekuwa tunafuatilia ile kamera uliyoifunga katika ofisi ya Jenerali William lakini toka wakati ule hajarejea katika ofisi yake.Tunaendelea kumfuatilia na kama kuna kitu chochote tutakipata nitakujulisha mara moja.Hakikisha unachunguza kila kinachoendelea katika nyumba hiyo na kama ikiwezekana tega kamera na kifaa cha kunasa maongezi ili tujue William anawasiliana na nani na wanaongea nini.Nina uhakika mkubwa lazima anafahamu kinachoendelea

kuhusiana na kirusi alichokileta Sattar”

“Sawa nitajitahidi kufanya hivyo Ruby” akasema Nawal

“Kumbuka kuwa makini sana kwani wakikugundua hao jamaa lazima watakuua” Ruby akasisitiza

“Ninalifahamu hilo Ruby na mpaka hapa bado hakuna tatizo lolote” akasema Nawal

“Kwa kutumia simu yako tayari tumefahamu mahala ulipo hivyo tunarusha drone yetu mahala hapo ili kuichunguza zaidi na kujua kila kinachoendelea kwa nje”

akasema Ruby na kuagana na Nawal.

TEHRAN - IRAN

Zimekwisha pita saa tisa toka Mathew Mulumbi na wenzake sita walipoiteka ndege iliyokuwa inawapeleka nchini Marekani.Ndani ya ndege ilikuwa ni furaha tupu.Raia wale wa Iran waliimba na kucheza kwa furaha wakifurahia kurejea nyumbani baada ya miaka kadhaa ya kuishi katika mateso makubwa.Ilikuwa ni kama

muujiza kwao pale ndege ilipobadili uelekeo na kuelekea nchini Iran.Hawakutegemea kama jambo hili lingewezekana siku moja waweze kurejea nyumbani.

Wakati ndege ikiendelea kupasua anga kuelekea nchini Iran,Mathew akachukua zamu ya kuwalinda mateka wao waliokuwa wamefungwa pingu zile ambazo Mathew na wenzake walikuwa wamefungwa.

“Mnatupeleka wapi?akauliza mmoja wa

mateka ambaye ni rubani wa ndege

“Mnakwenda nchini Iran ambako mtakabidhiwa kwa mamlaka husika na yawezekana hamtaweza kuziona tena familia zenu” akasema Mathew huku akiichezea bastora yake.Mmoja wa wale marubani akainamisha kichwa na kumwaga machozi

“Tafadhali msitupeleke Iran watatuua.Uhasama wa Iran na Marekani ni mkubwa na watu wale ni makatili wanaweza kubwa watatukata

vichwa ! akasema mmoja wa walinzi wale

“Taifa lenu ndiyo taifa katili kabisa duniani kuliko yote.Hawa raia wa Iran ambao bado hawaamini kama wanarejea tena nyumbani kwao walikamatwa na kufungwa bila kuwa na hatia.Wameteswa sana na kilichokuwa kinafuata ni kupelekwa Marekani kuuawa.Huu ni ukatili uliopitiliza.Machafuko yanayoendelea eneo la Afrika Mashariki hivi sasa ni nchi yenu ndiyo imeyaratibu kwa

lengo la kujipatia mafuta kutoka Uganda.Wakati damu ya watu ikimwagika kila uchao,tani na tani za mafuta zinamiminika Marekani.Huu ni zaidi ya ukatili.Marekani na wamarekani wanastahili adhabu kali ! akasema Mathew kwa ukali

“Wewe ni gaidi na umelipua ubalozi wa Marekani jijini Dar es salaam unadhani kwa hiki ulichokifanya utakuwa salama? Akauliza mmoja wa walinzi akimtazama Mathew kwa hasira

“Nakuhakikishia hautakuwa salama.Marekani haijawahi kushindwa na gaidi yeyote.Utasakwa kwa maisha yako yote hadi tuhakikishe umekamatwa na kupata adhabu unayostahili kwa unyama ulioufanya ! akasema yulemlinzi lakini Mathew hakumjibu kitu

Ndege ilikaribia kuingia katika anga la Iran na Abdu Razaq aliyekuwa anaiongoza ndege ile akawaita wenzake na kuwajulisha kuwa wanakaribia kuingia katika anga la Iran.Abdu Razaq akabonyeza

kifaa ambacho walikizima pale walipobadili uelekeo wa ndege ambacho kingewawezesha kuwasiliana na waongoza ndege na vile vile kuonekana katika rada za Iran.

Ndege iliingia katika anga la Iran na kuanza kuonekana katika rada za Iran. Abdu Razaq akajitambulisha kuwa wao ni raia wa Iran lakini walikuwa na ndege ya Marekani.Halikuwa jambo jepesi kuwaamini na ndani ya muda mfupi wakajikuta wamezingirwa na ndege nane na kivita za Iran

zikiwasindikiza kuelekea katika uwanja wa ndege wa kijeshi jijini Tehran.

Kwa kufuata maelekezo waliyopewa na waongoza ndege Abdu Razaq aliiongoza ndege hadi katika uwanja wa kijeshi uliopo nje kidogo ya jiji la Tehran huku ikiendelea kusindikizwa na ndege za kivita za Iran.Mara tu ndege ile iliposimama ilizingirwa na wanajeshi wenye silaha.Abdu Razaq na wenzake wakakumbatiana kwa furaha baada ya ndege kusimama.Walikuwa

nyumbani.Wote kwa pamoja wakamshukuru Mathew kwa ujasiri wake uliosababisha wao wakawa huru tena.

Mlango wa ndege ukafunguliwa na Yasser Wazir akawa ni mtu wa kwanza kushuka ndegeni.Akashuka ngazi haraka haraka na kukanyaga ardhi akainama akasujudu.Wenzake nao wakashuka na kufanya kama alivyofanya Yasser.Uwanjani pale alikuwepo Meja Jenerali Farhad Karvan mkuu wa majeshi wa Iran ambaye alifika kuwapokea raia wale wa Iran

ambao waliaminika tayari wamekwisha uawa.Ulikuwa ni mshangao kwa wote waliokuwepo pale uwanjani baada ya kuwaona tena wenzao wakishuka ndegeni wote wakiwa hai japo walikuwa wamedhoofika sana.Meja Jenerali Farhad akawakaribisha tena nyumbani

Wakati salamu zikiendelea katika mlango wa ndege akajitokeza Mathew Mulumbi na kuwafanya watu wote wageuke kumtazama.

“Na Yule ni nani?akauliza Meja Jenerali Farhad Karvan

“Yule ni mtu muhimu sana.Anaitwa Abu Zalawi ndiye ametuwezesha tukanyage tena katika ardhi ya nyumbani” akasema Yasser Wazir

“Huyu mbona kama……” akasema Meja Jenerali Farhad baada ya kumtazama Mathew kwa makini lakini Yasser akamkatisha

“Anaitwa Abu Zalawi ndiye aliyelipua ubalozi wa Marekani jijini Dar es salaam.Huyu ndiye aliyepambana na

kuhakikisha tunafanikiwa kuidhibiti ndege na kuibadili uelekeo kuja nyumbani.Naweza kusema kwamba bila yeye tusingefanikiwa kukanyaga tena ardhi ya nyumbani tulikuwa tunaelekea kuuawa.Ndani ya ndege kuna walinzi tumewashikilia mateka ambao wote ni raia wa Marekani ” akasema Yasser.

Meja Jenerali Farhad akatoa maelekezo Mathew Mulumbi akachukuliwa akaingizwa katika gari na kuondolewa haraka pale

uwanjani.Farhad akiwa ameongozana na Yasser wakaingia ndegeni na kuwashuhudia wale mateka waliokuwa wamefungwa pingu.Akatoa maelekezo na mateka wale wakafunguliwa pingu kisha wakashushwa ndegeni na kuingizwa katika gari la jeshi na kupelekewa mahala alikoelekeza.Yasser na wenzake nao pia wakaingizwa katika gari maalum na kupelekwa kwanza katika hospitali ya jeshi kwa ajili ya kuchuguzwa afya zao kabla ya kuruhusiwa kukutana na

familia zao.Hakuna aliyejua mahala alikopelekwa Mathew Mulumbi japo Meja Jenerali Farhad aliwahakikishia kwamba amepelekwa sehemu salama

WASHINGTON DC – MAREKANI

Kitendo cha Abdu Razaq kuwasha tena kifaa kilichowawezesha kuwasiliana na waongoza ndege wa Iran na vile vile kuiwezesha ndege kuanza kuonekana katika rada kiliwawezesha mamlaka za

Marekani waliokuwa wakiitafuta ndege hiyo kuiona na kufuatilia uelekeo wake na wakagundua ilikuwa inaelekea nchini Iran

Taarifa hiyo ya ndege iliyopotea kuonekana ikielekea nchini Iran iliwafikia G20 wakiwa katika kikao cha kujadili mapendekezo ya mkuu wa CIA Jason Washington ya kutaka Abu Zalawi auawe baada ya kujulikana kuwa si gaidi bali ni jasusi akitokea Tanzania na si Saudi Arabia kama walivyoelezwa na Habiba Jawad.Kikao kilikuwa kizito na

kilichukua muda mrefu kutokana na wengi wa wajumbe kutokukubaliana na wazo la kutaka kumuua Mathew Mulumbi kabla hajamaliza kazi aliyotumwa kuifanya.

David Walker aliyepigiwa simu na Jason Washington kumjulisha kwamba ndege tayari imeingia katika anga la Iran,aliwapa wenzake taarifa zile.

“Hizi si taarifa za kustusha wala kushangaza kwani tulitegemea jambo hilo kutokea kutokana na mipango

mizuri tuliyokuwa tumeiweka. Suala mezani bado ni kuhusiana na Abu Zalawi ambaye limetolewa pendekezo la kuuawa baada ya kujulikana kuwa si gaidi kama tulivyoaminishwa na Habiba Jawad.Tunatakiwa kupata muafaka katika jambo hili haraka" akasema David Walker

"Binafsi baada ya kuwasikiliza kwa muda mrefu sijaona bado sababu ya msingi ya kutaka kumuua Abu Zalawi hata kama tumegundua si gaidi.Mpaka hatua hii

hajaonyesha dalili zozote mbaya na amevumilia mateso makali kwa ajili ya kuitekeleza misheni hii aliyopewa.Nashauri tumuache aendelee na misheni yake kwani mahala alipofika ni muhimu sana.Pale atakapokuwa amekamilisha misheni yake ndipo tumuue lakini kwa sasa tutafanya kosa kubwa kumuua” akasema Willie Simmons ambaye alikuwa kimya kwa muda mrefu wa kikao kile.Wajumbe wengine wakaonekana kumuunga mkono

“Kuna tatizo hapa ambalo wengi hamtaki kuliona.Huyu Abu Zalawi au Mathew Mulumbi ambaye tumemtuma akatekeleze kazi yetu nchini Iran anatokea Tanzania na tayari anafahamu kuwa ni sisi tunaohusika na vurugu zile za kidini zilizotokea nchini Tanzania kwa lengo la kuchukua mafuta kutoka nchini Uganda.Kama mtakumbuka wakati tunamueleza kuhusu sisi tulimueleza sehemu mbali mbali ambazo tumetengeneza machafuko na mojawapo ikiwa

ni Tanzania.Kwa namna yoyote ile huyu mtu lazima atakuwa na hasira na sisi.Hatuwezi kujua moyoni mwake anawaza nini lakini Abu Zalawi ni mtu hatari sana kuendelea kumtumia kwa sasa katika misheni zetu" akasema David walker

"Amefikaje kwa Habiba Jawad hadi wakajenga mashirikiano ya karibu? Yawezekana akawa amebadilika kutoka kuwa jasusi hadi kuwa gaidi hivyo hatakuwa na madhara yoyote

kwetu hata kama akifahamu siri zetu” akasema Eric Wood.

“Niliwaeleza awali kwa kirefu namna Mossad walivyombadili Mathew Mulumbi kutoka kwenye ujasusi hadi kuwa gaidi Abu Zalawi na lengo kubwa likiwa ni kumuua Habiba Jawad ambaye hadi leo hii Mossad hawajui kama tunashirikiana naye.Swali la kujiuliza hapa ni je kama aliandaliwa kwa ajili ya kumuua Habiba Jawad kwa nini baada ya kuonana naye hakufanya hivyo na badala yake akaanza kushirikiana

naye? Kuna nini kati ya Abu Zalawi na Habiba Jawad hadi akaamua kumleta kwetu mtu huyu ili tumtumie?
Tukiangalia mtiririko huo wote tunaona ni namna gani misheni yetu ilivyoingia dosari.Hata kama tukikubaliana kwamba tumuache amalizie misheni tuliyomtuma tutakuwa tunajidanganya tu kwani hatujui kuna nini kati yake na Habiba Jawad? Upo uwezekano mkubwa huyu jamaa akabadilika na kuwa mwiba kwetu ndiyo maana

lazima tumuwahi kumuua kabla hajafanya chochote nchini Iran” David Walker akaendelea kuwashawishi wenzake wakubali mpango wa kumuua Mathew Mulumbi

“Vipi kuhusu Mossad ambao wanataka tuwape taarifa za mahala alipo Habiba Jawad? Akauliza Michael Torres.

“Hatutaweza kuwapa taarifa za mahala alipo Habiba Jawad badala yake Habiba tutamuua sisi wenyewe baada ya kumuhoji kujua kuhusu Mathew Mulumbi.Ni yeye

ambaye ametufikisha hapa tulipofika hivyo si mtu ambaye tunaweza kumuanini na kuendelea kushirikiana naye tena.Lazima tumuue lakini tutafanya hivyo pale tu ambako Mossad watafanikiwa kumuua Mathew Mulumbi" akasema David Walker.

Baada ya mjadala mzito hatimaye wakafikia makubaliano ya kumuua haraka Mathew Mulumbi kwa kuwatumia majasusi wa Mossad walioko nchini Iran.Baada ya kumaliza kikao kile David Walker akaondoka

kwenda kuonana na mkurugenzi mkuu wa CIA Jason Washington

“Dah ! siamini kama misheni ambayo tumetumia gharama kubwa ya fedha na damu kumwagika imeishia sehemu nzuri kiasi hiki.Tayari Abu Zalawi amekwisha ingia nchini Iran kwa ajili ya kuianza kazi tuliyomtuma.Itatuchukua muda mrefu kuandaa tena operesheni nyingine na kufikia hatua kubwa kama hii ya kupandikiza mtu nchini Iran.Tulifanya makosa sisi

wenyewe hatukuwa makini toka mwanzo na zoezi hili hadi tukajikuta tukimtumia mtu ambaye si sahihi.Imeniuma sana kwani hivi sasa Abu Zalawi tayari amekwisha ingia nchini Iran.Kuna wakati ninasikia sauti ambayo inakataa tusifanye hiki tunachotaka lakini ninaisikia tena sauti nyingine ikinionya kuwa Abu Zalawi ni mtu hatari sana kwetu ambaye anapaswa kudhibitiwa haraka sana.Ngoja tukubali kushindwa na tujipange vizuri zaidi ili misheni ijayo iwe na mafanikio

makubwa” akaendelea kuwaza David.

****

“Imekuwa vyema umefika kwa wakati David kwani tunakwenda kuonana na makamu wa Rais amenitaka nifike ofisini kwake” akasema Jason Washington mkurugenzi mkuu wa CIA baada ya David Walker kufika ofisini kwake.

Bila kupoteza muda wakaingia katika gari la Jason na kuondoka kwenda kuonana

na Mark Piller makamu wa Rais

“Nini kimejiri huko katika kikao? Akauliza Jason na David akamweleza kila kitu walichokubaliana katika kikao

“Vizuri sana.Nilimdokeza Mark Piller kuhusiana na mpango wetu wa kumuondoa Abu Zalawi.Mark amestushwa sana na jambo hili ndiyo maana amenitaka nikaonanye naye kwani tusingeweza kuzungumza kwa kirefu katika simu.Haamini kile nilichomweleza kuhusu Abu

Zalawi” akasema Jason Washington

“Suala hili la Abu Zalawi linaumiza vichwa sana.Kila mtu anashangaa kuhusu jambo hili limetokeaje?

“Hatuna wa kumlaumu katika hili David.Tumekosea sisi wenyewe na lazima tuchukue hatua za haraka sana kuhakikisha jambo hili halitakuwa na madhara kwetu.Kama tungechukua tahadhari mapema haya yote yasingetoke ana misheni ingeendelea kama kawaida” akasema Jason

“Kuna kitu nimekuwa najiuliza vipi kuhusu wale jamaa wanasayansi tuliokuwa tunawashikilia kwa muda mrefu? Tunakubali tumewapoteza?akauliza David na Jason akatikisa kichwa akisikitika

“Watu wale japo hawajatupa taarifa tulizokuwa tunazihitaji lakini ni watu wa muhimu sana kwa Iran.Katika hili tumewapa Iran ushindi mwepesi lakini lazima tuhakikishe nao pia wanauawa pamoja na Abu Zalawi.” akasema Jason

Walifika katika ofisi ya makamu wa Rais ambaye alikuwa anawasubiri na bila kupoteza muda wakaingia katika chumba cha maongezi ya faragha na kikao kikaanza.

“Jason nimevuruga ratiba yangu ya siku ya leo ili niweze kuzungumza nanyi.Nataka kufahamu kwa kina kuhusiana na hiki kinachoendelea” akasema makamu wa Rais Mark Piller

Jason akamuelezea Mark Piller kila kitu hadi walipogundua kuhusu Abu Zalawi kuwa si gaidi bali ni

jasusi pamoja na maamuzi waliyoyachukua ya kumuua

“Jason jambo hili limetokeaje? Kwa nini haukufanyika uchunguzi wa kina kuhusiana na huyu mtu Abu Zalawi hadi tumefika hapa tulpofika? Akauliza Mark Piller

“Katika hili Mark hatuna wa kumlaumu mtu bali tunapaswa kujilaumu sisi wenyewe.Tulifanya uzembe wa kutokufanya uchunguzi wa kina kuhusiana na Abu Zalawi” akasema Jason

“Lakini yote haya ameyasababisha Habiba

Jawad ambaye tulimuamini kwa asilimia mia moja na hivyo tukamuamini yule mtu aliyetuletea.Hata mara moja hajawahi kutuangusha na katika kila operesheni tuliyomshirikisha hakujawahi kutokea matatizo.Hii ni mara ya kwanza Habiba anatufanyia kitu cha namna hii" akasema David Walker

"Mnadhani Habiba alikuwa na lengo lake binafsi la kumleta kwetu Abu Zalawi?akaliza Mark Piller

"Hatuna uhakika bado ndiyo maana tunataka

kulifanyia uchunguzi suala hilo lakini wakati uchunguzi huo ukiendelea tunataka kumuondoa kwanza Abu Zalawi pamoja na wale wanasayansi tuliokuwa tunawashikilia” akasema Jason.Baada ya tafakari ya muda mfupi Mark akauliza

“Kutakuwa na athari gani kama tukimuacha Abu Zalawi akaendelea na misheni lakini tukimfuatilia kwa ukaribu mkubwa kujua kila anachokifanya kwa kuwatumia hao majasusi wa Mossad ambao mnataka kuwatumia

kumuua?akauliza Mark Piller na Jason akampa maelezo aliyopewa na Moshe Levine mkuu wa Mossad kuhusu Abu Zalawi na Mark akazidi kuchoka.

“Mark hatuna namna lazima tumuondoe Abu Zalawi haraka sana ili kujihakikishia usalama wetu.Endapo tukishindwa kumuondoa Abu haraka itatugharimu baadae” akasema Jason.Waliendelea na majadiliano kwa muda halafu Mark Piller akasema

“Jason na David nimekubalianba na

mapendekezo yenu juu ya suala hili lakini nina ushauri.Hatuwezi kumuua Habiba Jawad nchini kwao Saudi Arabia.Habiba Jawad ana ukaribu mkubwa na mfalme wa Saudi Arabia ambaye ni mshirika mkubwa wa Marekani hivyo lazima tujihadhari tusivuruge mahusiano mazuri kati yetu na serikali ya Saudi Arabia.Habiba aitwe Marekani na akifika huku ndipo atakapouawa" akashauri Mark Piller

“Ushauri mzuri tutauzingatia” akasema Jason

“Angalizo.Habiba asiuawe kama Mossad hawajamuua Abu Zalawi.Pale ambapo Abu Zalawi atakuwa ameuawa ndipo Habiba auawe kwani tunaweza kumuua Habiba halafu Mossad wakashindwa kumuua Abu Zalawi.Kama kuna jambo wawili hawa wanalipanga lazima tuwaondoe wote wawili akiondolewa mmoja na mwingine akabaki hatutakuwa tumefanya kitu” akasisitiza Mark Piller.Baada ya

majadiliano Jason na David wakaondoka .Mark Piller hakupoteza muda akainua simu na kumpigia Rais William Washington

“Mheshimiwa Rais nahitaji kukuona sasa hivi” akasema Mark

“Njoo ofisini” akajibu Rais William na Mark Piller akatoka ofisini kwake kuelekea ofisini kwa Rais.

“Mark mpango wenu unakwenda vizuri.Nimefurahishwa na taarifa nilizozipata kwamba ndege ile iliyopotea

imeonekana ikielekea nchini Iran” akasema Rais William baada ya Mark kufika ofisini kwake

“Mheshimiwa Rais ni kweli mpango umekwenda vizuri sana na hivi tuzungumzavyo tayari mtu wetu amekwisha kanyaga ardhi ya Iran” akasema Mark Piller

“Vipi mna mawasiliano naye baada ya kuwasili Iran? Akauliza Rais William

“Mheshimiwa Rais mpango wetu wa kwanza ulikuwa ni kumuingiza Abu

Zalawi nchini Iran na mpango huo umefanikiwa vizuri lakini kuna tatizo limejitokeza” akasema Mark Piller na sura ya Rais William aikabadilika

“Kumetokea tatizo gani tena” akauliza William

“Baada ya Abu Zalawi kufika salama Iran tulihitaji kumpa msaada na kwa vile hatuna wetu wetu kule Iran ilitulazimu kuomba msaada kutoka kwa wenzetu wa Mossad ambao wana majasusi wao Iran na hapo ndipo lilipoibuka jambo ambalo hatukuwa tukilifahamu”

akasema Mark Piler na kumueleza Rais William kila kitu walichokifahamu kutoka kwa Mossad kuhusiana na Abu Zalawi.Zilikuwa ni taarifa zilizomstua sana William

“Mark kwa nini haya yote yametokea?Kwa nini hamkuchukua tahadhari mapema kuhakikisha mnamfahamu vyema mtu ambaye mnataka kumtumia katika misheni kubwa kama hii? Akauliza William

“Mheshimiwa Rais katika hilo tunakiri tulikosea na ndiyo maana tunataka

kuchukua hatua za haraka za kurekebisha kwa kumuondoa Abu Zalawi haraka sana kabla hajaendelea na misheni aliyotumwa nchini Iran”

“Kumuua Abu Zalawi ni suluhisho la jambo hili?akauliza William akionekana kukasirika

“Mheshimiwa Rais huyu mtu ni hatari kwetu kama tukiendelea kumuacha hai.Tayari anafahamu kila kitu kuhusu sisi na baya zaidi anafahamu ni sisi tulio nyuma ya kile kilichotokea Tanzania na Afrika mashariki na

anafahamu kwa nini tulifanya vile....”

“Pamoja na kufahamu ! akasema kwa ukali Rais William na kumkatisha Mark Piller

“Pamoja na kufahamu hayo yote lakini bado Abu Zalawi au vyovyote vile anavyofahamika amekubali kuifanya kazi aliyotumwa na kwa sasa tayari amefika nchini Iran.Anafahamu kabisa kwamba kazi aliyotumwa kuifanya Iran ni kazi ya hatari kubwa na kama akijulikana kuwa ni pandikizi la Marekani

anaweza akauawa muda wowote ule lakini bado yuko tayari kufanya.Kumuua Abu Zalawi ni kosa kubwaMark ! akasema Rais William

“Mheshimiwa Rais pamoja na Abu Zalawi kukubali kuifanya kazi aliyotumwa aifanye lakini hakuna anayejua moyoni mwake nini anakiwaza,hatujui ana mipango gani dhidi yetu.Kwa taarifa tuliyoipata kutoka kwa Mossad ni kwamba Abu Zalawi ameyatoa maisha yake katika kupambana na ugaidi hasa kundi la IS linaloendelea

kuotesha mizizi katika eneo la Afrika Mashariki.Abu Zalawi ni bilionea na ana familia inaishi Paris Ufaransa lakini ameacha hivyo vyote akajielekeza katika kupamba na na magaidi.Jaribu kupata picha mtu kama huyu anakuja kugundua kwamba tunashirikiana na magaidi wa IS na kibaya zaidi kuchochea machafuko katika nchi anakotoka na kusababisha vifo vya watu na sisi tukiendelea kubeba tani na tani za mafuta unadhani mtu kama huyu atafanya nini?Lazima atakuwa

na chuki kubwa sana dhidi yetu na hatujui nini anakifikiria lakini ni wazi jambo hili hataweza kulivumilia" akasema Mark Piller

"Mark nimekuelewa lakini maamuzi ya kumuua mtu kama huyu si sahihi.Mtu kama huyu bado anaweza akawa upande wetu.Tunaweza kuzungumza naye na kumfanya atuelewe na hata kama alikuwa na kitu moyoni mwake tukakiondoa.Sisi ni taifa kubwa na hatuwezi kukubali kushindwa kirahisi

namna hii.Hebu fikiria Mark,nini kingine mtakifanya kitakachowawezesha kupandikiza mtu nchini Iran? Kwa kuwatumia wale mateka wa Iran imekuwa rahisi kwetu kuweza kupenyeza mtu ndani ya Iran na kama mkiharibu msheni hii itachukua miaka mingi kuweza kufanikisha jambo kama hili na pengine lisiwezekane tena.Kwa kuwa tayari Abu Zalawi amekwisha ingia Iran,itafutwe namna ya kuzungumza naye na kumuweka sawa aendelee na jukumu lake badala ya

kufikiria kumuua” akasema Rais William

“Mheshimiwa Rais.....” Mark Piller akataka kusema kitu lakini Rais William akamzuia

“Mark sitaki kuendelea na mjadala huu.Hatuwezi kuipa Iran ushindi kirahisi namna hii lazima kwa namna yoyote ile misheni hii iendelee.Iran ni taifa tishio kwa Marekani kwa sasa na lazima tufahamu uwezo wake wa silaha hivyo lazima misheni iendelee.Abu Zalawi hapaswi kuuawa !

akasema kwa sauti ya msisitizo kisha wakabaki wanatazamana

“Mheshimiwa Rais sidhani kama unaiona hatari iliyoko mbele yetu kama tukiendelea kumtumia huyu Abu Zalawi ! akasema Mark

“Mark sijali chochote, ninachohitaji ni Abu Zalawi aendelee na misheni aliyotumwa nchini Iran.Endapo Abu akiuawa na misheni ikashindwa kuendelea ninaapa nitakifuta hiki kikundi chenu kwani hakitakuwa na maana tena.Sijali kama nitauawa ama nini kitatokea

lakini lazima nikifute !
akasema Rais William

“Mheshimiwa Rais nilipokuja kukueleza kuhusiana na kikundi hiki na mambo yake nilikupa angalizo kwamba unatakiwa usiri mkubwa kwani Rais wa nchi hapaswi kufahamu chochote kuhusu uwepo wa kikundi hiki.Utayaweka maisha yetu sote katika hatari kubwa.Nakuomba mheshimiwa Rais usifikirie kufanya hicho hicho unachotaka kukifanya”
akasema Mark Piller

“Mark mimi siogopi chochote na ninakuhakikishia kwamba nitafanya hivyo na wamarekani watajua kuwa nchi yao inashirikiana na magaidi”

“Mheshimiwa Rais ! akasema Mark

“Mark fanya ninavyokuelekeza.Ukitaka kundi lenu liendelee kuwepo.Nataka Abu zalawi aendelee na misheni yake nchini Iran.Sitaki auawe.Fanya kila linalowezekana kuhakikisha misheni yake inafanikiwa.Tunaihitaji sana

misheni hii ama sivyo Iran itaendelea kutoa vitisho vya kusishambulia Marekani! Siwezi kuzivumilia kauli chafu za vitisho zinazotolewa na Rais wa Iran dhidi ya Marekani ! akasema Rais William

“Mheshimiwa Rais kufanya hicho unachotaka nikifanye ni usaliti mkubwa kwa wenzangu na…..”

“Mark kumbuka kwamba sisi ndio tunao ongoza nchi hii na dhamana ya usalama wa watu wetu tumeibeba sisi na kwa sasa watu wetu wana hofu kufuatia vitisho vya Iran kuwa

anao uwezo wa kuishambulia na kuiharibu Marekani hivyo basi lazima tufanye kila lililo ndani ya uwezo wetu kuhakikisha tunaiweka nchi yetu salama pamoja na watu wake ndiyo maana ninasema kwamba tunaihitaji sana misheni hii kwa ajili ya kufahamu wezo wa silaha za Iran na baada ya hapo tutaichakaza vibaya sana.Ikitokea Iran imeshambulia Marekani watakaobeba mzigo wa lawama ni sisi na si hao ambao unaogopa kuwasaliti.Mark

fanya kila linalowezekana hata kama ni kwa kuwasaliti wenzako hakikisha Abu Zalawi anakuwa salama na anaendelea na misheni yake nchini Iran.Vuruga mpango wa kumuua ! akasema Rais William na Mark Piller akainamisha kichwa akitafakari

“Umenielewa Mark Piller?akauliza Rais William

“Nimekuelewa mheshimiwa Rais.Nitafanya kama ulivyoelekeza lakini naomba ufahamu kwamba ni jambo la hatari kubwa”

“Usihofu kuhusu hilo Mark.Kama kuna hatari yoyote unaihisi nijulishe na mimi nitakulinda.Tunayafanya haya kwa maslahi ya nchi yetu” akasema Rais William na Mark Piller akaondoka akarejea ofisini kwake na kujiegemeza kitini

“Hili jambo linaendelea kubadilika kila wakati.Rais anataka niwasaliti wenzangu na kuvuruga mipango ya kumuua Abu Zalawi ! akawaza Mark

“Lakini ukilitazama jambo hili kwa kina zaidi,Rais yuko

sahihi.Hatupaswi kumuua Abu Zalawi badala yake tunapaswa kufanya kila liwezekanalo kumuweka upande wetu.Kwa hiyo kwa mara ya kwanza nitalazimika kuwasaliti wenzangu na kuvuruga mpango wa kumuua Abu Zalawi.Kuna mtu mmoja tu ambaye ninatakiwa kuzungumza naye" akawaza na kufungua mkoba wake akatoa simu iliyokuwa na namba kumi na mbili tu ambazo ni namba za watu muhimu akaelekeza kidole chake katika namba ya sita ambayo ilikuwa

ni namba ya Habiba Jawad akampigia baada ya sekunde kadhaa simu ikapokelewa.

“Mark Piller ! akasema Habiba Jawad akionekana kushangaa

“Habiba Jawad unaendeleaje? Akasema Mark

“Ninaendelea vizuri Mark.Nimeshangaa kidogo leo umenipigia simu.Sikutegemea kabisa kupata simu yako” akasema Habiba Jawad

“Habiba nimelazimika kukupigia simu kuna mambo ya muhimu sana ya

kuzungumza mimi nawe na ninakuomba tafadhali yale tutakayoyazungumza hapa yawe ni baina yetu sisi wawili.Mtu mwingine yeyote kutoka G20 hatakiwi kufahamu kama nimekupigia simu.Umenielewa Habiba?akauliza Mark Piller

“Nimekuelewa Mark.Nini unataka kuzungumza nami?akauliza Habiba

“Kwanza kabisa ninataka kukupa taarifa kuwa mpango wetu umekwenda vizuri na hivi tuzungumzavyo tayari Abu

Zalawi amekwisha ingia nchini Iran” akasema Mark Piller

“Hizo ni taarifa njema sana.Nimefurahi kusikia matokeo mazuri ya mpango huu.Ninakuhakikishia Mark kuwa kama tayari Abu amefanikiwa kuingia nchini Iran lazima atafanikisha kila kitu alichotumwa kukifanya.Kitu cha msingi kwa sasa ni kujitahidi kutafuta namna ya kuwasiliana naye na kujua maendeleo yake” akasema Habiba

“Tayari tumelifanya hilo Habiba ila kuna tatizo limejitokeza”

“Tatizo gani Mark?akauliza Habiba

“Baada ya kuhakikisha Abu Zalawi ameingia Iran ilitulazimu kuomba msaada kutoka kwa wenzetu wa Mossad ambao wana watu wao kule Iran kwa ajili ya kumpa msaada na hapo ndipo tulipofahamu kila kitu kuhusu Abu Zalawi” akasema Mark na kumueleza Habiba kila kitu walichokigundua kuhusu Abu Zalawi.Kupitia spika za simu

Habiba Jawad akasikika akivuta pumzi ndefu

“Habiba unaweza ukazungumza chochote kuhusiana na jambo hili?akauliza Mark

“Sina cha kuzungumza Mark lakini kila kitu mlichoelezwa kuhusu Abu Zalawi ni cha kweli” akasema Habiba na Mark Piller akahisi mwili unamtetemeka

“Kwa nini Habiba kama ulifahamu kuwa Abu Zalawi ni jasusi tena anatokea Tanzania ukamleta kwetu tukampa

misheni kubwa kama hii? Akauliza Mark Piller

“Kwa sababu Abu Zalawi ndiye pekee anayeweza kuifanya kazi hii.Hakuna gaidi ambaye ana uwezo wa kuingia Iran na kufanya jambo la hatari la kuichunguza Iran zaidi ya Abu Zalawi.Mark hii si misheni ya kigaidi hii ni misheni ya kijasusi na mtu niliyewaletea ndiye anayefaa” akasema Habiba Jawad

“Habiba sisi tulihitaji gaidi lakini wewe ukatuletea jasusi tena anatokea Tanzania nchi ambayo kwa kushirikiana na

magaidi wa IS tumechochea machafuko ya kidini na kusababisha waumini kushambuliana na damu nyingi kumwagika na kama haitoshi bado tunaendelea na mpango wa kusambaza kirusi hatari kwa lengo la kuendelea kuchota utajiri mkubwa ulioko Afrika Mashariki.Kwa nini ukatufanyia hivi? Akauliza Mark

“Mark kama nilivyokueleza kwamba huyu ndiye mtu pekee anayefaa kwa misheni hii” akajibu Habiba

“Habiba japokuwa una uhakika kuwa mtu huyu ndiye anayefaa lakini tayari ana kasoro.Hatujui ni kitu gani anakiwaza baada ya kugundua kwamba sisi tuko nyuma ya kile kinachoendelea Afrika Mashariki.Hii ni kasoro kubwa na tayari imetia doa misheni nzima” akasema Mark

“Mark nataka nikuhakikishie kwamba Abu Zalawi hana tatizo lolote na msiwe na wasiwasi wowote naye.Anakwenda kutekeleza kile alichotumwa kukifanya Iran na uwezo wa kufanya

hivyo anao.Abu Zalawi japo ni jasusi lakini nimembadilisha na anafanya kazi kwangu.Nimembadili kutoka Jasusi kuwa Gaidi.Ni mimi pekee anayenisikiliza kila ninachomuelekeza kukifanya kwani nimemfanya kuwa mwanangu,amemuoa mwanangu Najma hivyo Abu Zalawi ni sehemu ya familia yangu" akasema Habiba

"Habiba kama nilivyokueleza kuwa tayari misheni imeingia dosari.Baada ya kugundua kuwa Abu Zalawi si Yule uliyetuaminisha kuwa

ni gaidi bali ni jasusi tena anatokea Tanzania,kuna maamuzi yamefanyika” akasema Mark Piller na kunyamaza kidogo

“Mmefanya maamuzi gani Mark?akauliza Habiba

“Tumekubaliana kumuua Abu Zalawi na misheni itakuwa imeishiahapo” akasema Mark na ukimya ukapita

“Mark Piller hilo ni kosa kubwa sana ambalo mtalijutia kwani hamtapata tena nafasi nyingine ya kumuingiza mtu wa kuwafanyia ujasusi nchini

Iran.Hii ni nafasi pekee mmeipata na mkishindwa kuitumia vyema ni juu yenu” akasema Habiba

“Habiba misheni tayari imevurugika na aliyeivuruga misheni hii ni wewe kwa kutuletea mtu ambaye hakuwa sahihi kwa misheni hii.Tulikuamini sana Habiba na ndiyo maana hatukuwa na wasi wasi wowote na Abu Zalawi lakini baada ya kumfahamu vyema Abu Zalawi umevunja uaminifu na maamuzi yaliyopitishwa ni wewe kuuawa pia” akasema

Mark Piller na ukimya ukawala.

“Mark ! akaita Habiba Jawad

“Unasemaje Habiba?

“Mnakwenda kufanya kosa kubwa sana kwa hiyo mipango yenu mliyoipanga” akasema Habiba

“Ninafahamu Habiba”

“Kwa nini ukanipigia kunijulisha kuhusu mipango yenu?akauliza Habiba

“Nimekupigia kwa sababu baada ya kutafakari kwa kina nimegundua kwamba tutafanya kosa

kubwa.Tunaihitaji mno misheni hii ifanikiwe hivyo nimekupigia kuomba msaada wako” akasema Mark na ukimya ukatawala tena.Habiba Jawad akavuta pumzi na kusema

“Nini unahitaji tena kutoka kwangu Mark wakati tayari mmekwisha panga mipango ya kuniua? Akauliza Habiba

“Nimeamua kuwasaliti wenzangu na kukueleza ukweli kuhusu mipango yetu,kwanza ili uchukue tahadhari na kujificha na pili ni kutafuta

namna ya kumfikishia Abu Zalawi taarifa za kumtaka achukue tahadhari kwani kuna watu wanaotaka kumuua.Nataka Abu aendelee na misheni hii hadi atakapoikamilisha” akasema Mark Piller

“Mark nimekuwa mtumwa wenu kwa miaka mingi,nimewafanyia kazi nyingi kwa manufaa ya nchi yenu lakini hata baada ya kuwafanyia hayo yote ninachoambulia ni kutaka kuuawa.Mmenisikitisha sana Mark”

“Habiba ndiyo maana nimekupa siri hii ili uweze kuchukua tahadhari na ikiwezekana uondoke Saudi Arabia ukajifiche mahala” akasema Mark

“Siwezi kukimbia Mark.Siwezi kukimbia.Kama mnataka kuniua njooni mtanikuta hapa ninawasubiri lakini fahamuni ya kwamba damu yangu haitawaacha salama ! akasema Habiba Jawad

“Habiba tafadhali naomba tusilifanye jambo hili liwe gumu.Wewe mwenyewe

unafahamu namna misheni hii ilivyo muhimu.Wengine wote hawalioni hilo lakini mimi ninafahamu umuhimu wake.Habiba tafadhali nakuhitaji sana.Naomba tushirikiane kuhakikisha misheni hii inaendelea na inafanikiwa.Naomba tafuta namna ya kumlinda Abu Zalawi dhidi ya wale wote watakaotumwa kumuua na aendelee na kazi aliyotumwa kuifanya.Habiba nakuahidi nitakulinda dhidi ya mipango yoyote mibaya inayopangwa juu yako” akasema Mark Piller

“Mark….. !

“Habiba tafadhali ! Sisi nawe tumetoka mbali sana na umetusaidia mambo mengi naomba mashirikiano yetu yaendelee kama kawaida na ninakuahidi kukulinda hata kama ni kwenda kinyume na wenzangu wote niko tayari kufanya hivyo.Tafadhali Habiba” akasema Mark

“Mark nimekuelewa lakini nataka kufahamu jambo moja.Nataka kufahamu namna mlivyopanga mipango ya kutuua mimi na Abu Zalawi” akasema Habiba na Mark

akamueleza mipango yote namna ilivyopangwa ya kuwaua yeye na Mathew

“Mark Piller unadhani nini kitakutokea pale wenzako watakapobaini kuwa umewasaliti?akauliza Habiba

“Ninafahamu nitakuwa matatizoni lakini niko tayari kukabiliana na chochote kitakachonitokea.Misheni hii ni muhimu mno kwa nchi yangu na kwa namna yoyote ile lazima ifanikiwe” akasema Mark Piller

“Sawa Mark nimekuelewa.Nitashirikiana

nawe kuhakikisha misheni hii inafanikiwa.Nitajitahidi kuhakikisha Abu Zalawi anapata taarifa mapema kabla ya watu wa Mossad hawajamfikia.Ninachotaka ukifanye ni kuendelea kunipa taarifa za mipango yenu yote mnayoipanga ili na mimi nitafute namna ya kumsaidia Abu Zalawi" akasema Habiba

"Nitakujulisha kila kitu Habiba Jawad lakini nakuomba nawe uchukue tahadhari kuanzia sasa.Pale utakapoitwa uje Marekani toa kisingizio kwamba hautaweza

kwa sasa kuna mambo ya msingi unayashughulikia na mimi nitaongeza nguvu.Ongeza ulinzi na mtu yeyote asiyefahamika asikaribishwe katika makazi yako” akasemaMark Piller

“Nakushukuru Mark.Mimi nitahakikisha Abu Zalawi anakuwa salama na anaendelea na mipango yake yote kama alivyotumwa nchini Iran” akasema Habiba wakaendelea na mazungumzo kidogo wakapeana mikakati namna watakavyokuwa

wakiwasiliana kwa siri kisha wakaagana.

“Nilijua tu lazima watagundua kuhusu Mathew lakini sikutegemea iwe mapema namna hii.Nilifahamu watakapogundua kuhusu Mathew mzigo wote wa lawama nitaubeba mimi na nilikwisha jiandaa kwa jambo hilo.Kwa sasa baada ya kuifahamu mipango yao natakiwa kuhakikisha Mathew anakuwa salama ili aweze kuikamilisha misheni yake” akawaza Habiba Jawad na

kuchukua simu nyingine akazitafuta namba Fulani na kupiga kisha simu ikapokelewa

“Habiba” akasema mtu aliyepokea simu upande wa pili

“Vahid unaendeleaje?akauliza Habiba Jawad

“Siwezi kusema naendelea vizuri Habiba.Bado kifo cha mwanangu Najma kinaniumiza mno.Ninajuta kwa nini nilimruhusu aje Riyadh.Kama ningeendelea kukaa naye hapa Tehran yasingemkuta haya

yaliyomkuta.Kwa ujumla bado siko sawa na itanichukua muda mrefu kulizoea jambo hili” akasema Vahid Ghorbani baba mzazi wa Najma.Vahid na Habiba waliwahi kuwa na mahusiano na wakamzaa Najma lakini hawakufunga ndoa na kila mmoja akaendelea na maisha yake.

“Vahid suala hili linatuumiza sote.Huwezi kujua niko katika hali gani kwa sasa baada ya kuwapoteza wanangu wawili ndani ya kipindi kifupi.Ni wakati mgumu sana huu kwetu sote hivyo

tusaidiane kufarijiana badala ya kulaumiana” akasema Habiba

“Sikulaumu Habiba nafahamu ulivyompenda Najma.Tuachane na hayo vipi maendeleo yako?

“Kama nilivyokwambia Vahdi kwamba siko sawa.Nimewapoteza watoto wawili ndani ya kipindi kifupi ni suala zito kulibeba lakini ninajitahidi.Hata hivyo sijakupigia simu kwa suala hilo.Vahdi kuna jambo nataka unisaidie”

“Sema chochote Habiba.Unataka nikusaidie nini?akauliza Vahid

“Kuna wanasayansi sita wa Iran waliokuwa wamepotea lakini leo hii wamerejea nyumbani”akasema Habiba

“Nimepata taarifa hizo kwamba wale watu wetu waliokuwa wamepotea wamerejea nyumbani leo hii lakini haijatolewa taarifa rasmi kwamba walikuwa wapi muda huu wote” akasema Vahid

“Aliyewakomboa watu hao na kuwarejesha nyumbani anaitwa Abu Zalawi”

“Abu Zalawi?! Vahdi akauliza

“Ndiyo.Anaitwa Abu Zalawi”

“Ni mtu wa wapi huyo Abu Zalawi?

“Ni Raia wa Saudi Arabia”

“Hatujafahamishwa jambo hilo.Nini unataka nikusaidie Habiba? Akauliza Vahid

“Ninataka ufanye kila lililo ndani ya uwezo wako uweze kuonana na huyu Abu Zalawi”

“Nionane na Abu Zalawi? Vahid akauliza

“Ndiyo.Kuna ujumbe wa muhimu sana ambao nataka umfikishie”akasema Habiba

“Habiba sifahamu alipo huyo Abu Zalawi na wala sijui ni jinsi gani nitaweza kumpata” akasema Vahid

“Vahid unatakiwa ufanye kila linalowezekana kuhakikisha unampata Abu Zalawi”

“Habiba sidhani kama mimi ni mtu sahihi wa kukusaidia kwenye jambo hilo” akasema Vahid

“Vahid ni muhimu sana ukaonana na Abu Zalawi.Huyo ndiye mume wa Najma”

“Mume wa Najma?! Vahidi akastuka

“Ndiyo ni mume wa Najma”

“Najma alikuwa na mume?Kwa nini hujawahi kuniambia jambo hili?

“Najma mwenyewe ndiye aliyetaka iwe siri na tusikujulishe.Kama unavyofahamu kuwa Najma hakuwahi kuwa na mpenzi lakini alipokutana na Abu Zalawi akajikuta akimpenda na

kufunga naye ndoa ya kimya kimya na alitoa maelekezo ya kutokufahamisha jambo hili.Alitaka yeye mwenyewe akujulishe pale atakapokuwa tayari lakini kwa bahati mbaya hakuwahi kufanya hivyo mauti yakamkuta” akasema Habiba

“Habiba ulikosea sana kukubali kunificha kuhusu Najma kuolewa wakati mimi ndiye baba yake mzazi.Hukunitendea haki katika hili”akasema Vahid

“Nakubali Vahid kwamba nilikosea lakini nilifanya hivyo kuheshimu matakwa ya

mtoto.Alitaka akueleze jambo hili yeye mwenyewe muda utakapofika.Tusameheane katika hilo”

“Nilipokuja msibani kwa nini huku nijlisha kuwa Najma alikuwa na mume hadi leo hii?

“Nilikuwa nimechanganyikiwa Vahid ndiyo maana sikukueleza chochote.Tafadhali naomba sana unisamehe kwa hilo” akajibu Habiba.Baada ya muda Vahid akauliza

“Unataka kumfikishia ujumbe gani huyo Abu Zalawi?akauliza Vahid

“Nataka uonane naye ana kwa ana na umpe simu nizungumze naye”

“Habiba umenipa mtihani mgumu sana.Kwanza ni nani huyo Abu Zalawi?Kwa nini yuko hapa? Akauliza Vahid

“Vahid naomba unisaidie hilo ninalokuomba ni muhimu sana”

“Habiba niko tayari kukusaidia lakini lazima nifahamu huyu mtu ni nani na kwa nini yuko hapa Iran?

“Abu Zalawi anataka kuuawa na Mossad hivyo nataka niongee naye nimpe

angalizo awe makini” akasema Habiba

“Anataka kuuawa na Mossad?akauliza Vahid

“Ndiyo.Kuna majasusi wanatumwa kuja Tehran kwa lengo la kumuua.Anatakiwa aipate haraka sana taarifa hiyo”akasema Habiba

“Kwani huyu Abu Zalawi ni nani hadi Mossad watake kumuua? Akauliza Vahid

“Vahid nitakueleza kila kitu hapo baadae kuhusiana na Abu Zalawi lakini kwanza naomba unisaidie kufanya kila uwezalo uonane naye na

umpatie simu nizungumze naye.Unaweza ukanisadia kwa hilo? Akauliza Habiba

“Sawa Habiba.Nitajitahidi kumtafuta huyo Abu Zalawi”

“Jitahidi Vahid wewe ni mfanya biashara mkubwa nchini Iran unafahamiana na watu wengi hata viongozi wa serikali naamini haitakuwa kazi ngumu kwako kufahamu mahala alipo Abu Zalawi” akasema Habiba Jawad na kuagana na Vahid.

****

Baada ya kutoka kuzungumza na makamu wa Rais,Jason na David walirejea katika ofisi ya Jason ambaye bila kupoteza muda akampigia simu Moshe Levine mkurugenzi wa Mossad

“Jason Washington” akasema Moshe baada ya kupokea simu

“Habari za muda huu Moshe.Nimekupigia kufuatia mazungumzo yetu ya awali” akasema Jason

“Ndiyo Jason.Umefikia wapi kuhusiana na yale

tuliyoyazungumza?akauliza Moshe Levine

“Kama nilivyokueleza asubuhi kwamba tunataka kumuua Abu Zalawi.Bado mpango huo unaendelea na kama nilivyokudokeza tunataka kuwatumia watu wako wa Mossad walioko nchini Iran” akasema Jason

“Jason nina watu wangu Tehran ambao wanaweza wakaifanya hiyo kazi muda wowote watakapopewa maelekezo lakini nilitoa masharti asubuhi ya kama mkitaka tuwasaidie kumuua

Abu Zalawi basi na nyinyi mtupe taarifa za mahala alipo Habiba Jawad.Mmefikia wapi katika suala hilo?akauliza Moshe Levine

“Tumejadiliana na tumekubaliana jambo moja.Habiba Jawad tutamuua sisi wenyewe pale ambapo nanyi mtakuwa mmemuua Abu Zalawi”

“Jason hatukukubaliana hivyo.Ninataka mtupe taarifa za mahala alipo Habiba Jawad na tutamkamata sisi wenyewe.Hatutaki kumuua kuna mambo mengi tunahitaji

kuyafahamu kuhusiana na mtandao wake kabla ya kumuua hivyo tupeni taarifa za mahala alipo sisi tutamkamata hatuhitaji msaada wa kumuua” akasema Moshe Levine

“Moshe sisi tuko tayari kutoa aina yoyote ya ushirikiano kwenu.Kama hamtaki kumuua Habiba hatuna tatizo na hilo.Sisi tutamkamata Habiba na tutamkabidhi kwenu lakini lazima kwanza tuhakikishe Abu Zalawi ameuawa ndipo tutawakabidhi Habiba

Jawad.Tunakubaliana katika hilo?akauliza Jason

“Jason tunamtaka Habiba Jawad kwanza ndipo tuwafanyie kazi yenu ! Kuna ugumu gani wa kutupa taarifa za mahala alipo Habiba ? akauliza Moshe Levine

“Moshe sisi na ninyi ni washirika wakubwa tena wa miaka mingi tunapaswa kuaminiana.Tuna sababu za msingi kwa nini hatuwezi kuwapa taarifa za mahala alipo Habiba Jawad.Naomba uniamini Moshe kwamba tutamkabidhi kwenu Habiba

Jawad pale tutakapokuwa na uhakika kwamba Abu Zalawi ameuawa.Hivi tuzungumzavyo tayari timu inaandaliwa kwa ajili ya kwenda kumkamata Habiba Jawad.Tutamuhifadhi hadi pale ambapo mtakuwa mmekamilisha zoezi la kumuua Abu Zalawi”

“Jason kutakuwa na ugumu katika jambo hilo.Tupeni Habiba Jawad na sisi tumuue Abu Zalawi”

“Moshe nakuhakikishia kwamba hata dakika hii mkimtaka Habiba Jawad mtampata lakini hatuwezi

kumkabidhi Habiba kwenu wakati bado hamjatekeleza kazi yetu.Muondoeni Abu Zalawi kwanza ili mumpate Habiba

“Tufanye hivi.Tudhihirishieni kwanza kama kweli mnaye Habiba Jawad na tutaelekeza apelekwe katika ubalozi wenu Jerusalem na baada ya kumuua Abu Zalawi mtamkabidhi kwetu.Tunakubaliana katika hilo”

“Hakuna tatizo katika hilo.Tutafanya hivyo”

“Vizuri.Nashukuru kama tumekubaliana hivyo Jason basi na sisi tunaanza mara moja mpango wa kumuua Abu Zalawi.Tutaendelea kufahamishana kila hatua tunayopiga” akasema Moshe Levine wakaagana

“Mambo yanazidi kuwa magumu David” Jason akamwambia David na kumuelezea kila kitu walichozungmza na Moshe Levine

“Nini maamuzi yako katika jambo hili? akauliza David Walker

“Hatuna ujanja lazima tumkamate Habiba Jawad na kumuandaa kwa ajili ya kuwakabidhi Mossad pale watakapokuwa wamemuua Abu Zalawi”

“Jason huo ni mpango wa hatari sana.Ni vipi kama wakimchunguza na kugundua kuwa tumekuwa tunashirikiana naye?akauliza David

“Tutamuweka Habiba Jawad katika ubalozi wetu jijini Jerusalem na baada ya wao kumuua Abu Zalawi sisi pia tutamuua Habiba Jawad

na kuwakabidhi maiti yake.Hatuwezi kuwakabidhi Habiba akiwa mzima” akasema Jason wakaendelea kujadiliana kuhusiana na mpango ule halafu Jason akainua simu na kumjulisha Mark Piller kuhusu mazungumzo yake na Moshe Levine pamoja na mpango waliouandaa.

Mark Piller baada ya kumaliza maongezi na Jason akampigia simu Habiba Jawad

“Mark karibu tena” akasema Habiba

“Habiba nimerejea tena kama nilivyokueleza awali kwamba nitakuwa ninakupa taarifa mipango yote inayopangwa dhidi yako” akasema Mark na kumueleza Habiba kuhusiana na mpango ule wa kutuma kikosi kwenda kumteka na kumpeleka katika ubalozi wa Marekani jijini Jerusalem tayari kwa kukabidhiwa kwa Mossad pale watakapokuwa wamefanikisha mpango wa kumuua Abu Zalawi.

“Ahsante sana Mark Piller kwa angalizo hilo.Tayari

nimekwisha anza taratibu za kumtafuta Abu Zalawi na kujua mahala alipo ili niweze kumuonya kuhusiana na mpango wa kumuua.Nategemea kabla ya watu hao wa CIA waliotumwa kuja kunikamata hawajafika hapa tayari nitakuwa nimekwisha mpata Abu Zalawi” akasema Habiba

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Kiza tayari kilikwishatanda katika jiji la Dar es salaam,Nawal alitoka chumbani kwake na kwenda kukaa sehemu ya kupumzikia iliyo mbele ya nyumba ile wanakoishi viongozi wa vikosi vya jeshi la Marekani vilivyopo Dar es salaam.Taa zilikuwa zinawaka katika nyumba hii kwani walikuwa wanatumia jenereta .Ulinzi pia ulikuwa mkali karibu kila pembe ya nyumba hii kulikuwa na

walinzi.Akiwa amejipumzisha mbele ya nyumba muhudumu akamfuata na kumuuliza kama angependa kutumia kinywaji chochote na Nawal akamuagiza amtengenezee kahawa

“Nilipowasiliana na Ruby saa kumi na mbili jioni,bado Jenerali William hakuwa amerejea ofisini kwake na hadi giza limeingia hatujui mahala alipo Sattar.Kwa namna yoyote ile lazima usiku wa leo tujue mahala kilipo kirusi.Nitamvamia Jenerali William usiku wa leo

chumbani kwake na lazima ataeleza alipo Sattar na kirusi.Kitu kikubwa ninachohitaji kufahamu ni watu wangapi wanaoishi ndani ya nyumba hii ili nijue namna ninavyoweza kukabiliana nao na kama nikiona sintaweza basi nitaomba msaada kutoka SNSA.Nitakaa hapa hapa hadi jenerali William atakaporejea” akawaza Nawal na kutolewa mawazoni baada ya kahawa yake kuletwa.

“Ahsante sana.Jina lako nani nimelisahau” akauliza Nawal

“Naitwa Brenda”

“Ouh Brenda .Naitwa Chloe” akasema Nawal na kumtaka Yule muhudumu kukaa kwa ajili ya mazungumzo lakini Brenda akamjulisha kwamba watazungumza pale atakapokuwa amekamilisha majukumu yake

“Huyu Brenda anaweza akanipa taarifa za kutosha kuhusu mahala hapa.Ngoja nimsubiri amalize majukumu yake” akawaza Nawal akiendelea kunywa kahawa yake taratibu

Akiwa ameyaelekeza macho yake katika geti mara akawaona wanajeshi waliokuwa wakilinda geti wakiwa katika heka heka akakaza macho zaidi ili kujua kinachoendelea.Geti likafunguliwa na gari nne zikaingia mle ndani.Tatu zikiwa ni gari za doria za jeshi la Marekani na moja ikiwa ni aina ya Prado.Kutoka katika mojawapo ya gari akashuka Jenerali William na na makamanda wengine wawili na kutoka katika ile Prado wakashuka watu wanne ambao

hawakuwa wanajeshi.Nawal alihisi mapigo ya moyo wake yakibadilika na kwenda haraka haraka baada ya kuziona sura za wale jamaa walioshuka katika Prado

“Sattar ! Assad ! akasema kwa sauti ndogo ya mshangao

Jenerali William akiwa ameongozana na wale jamaa wengine wanne na wanajeshi wawili wakaanza kupiga hatua kuelekea ndani ya ile nyumba.

“Chloe ! akasema Jenerali William baada ya kumkuta Nawal amekaa nje

“Jenerali William” akasema Nawal na kusimama

“Habari za toka mchana?Umeshinda salama? Akauliza Jenerali William

“Niko salama kabisa Jenerali William.Nimepata huduma nzuri”

“Nafurahi kusikia hivyo Chloe.Hawa ni wenzangu Meja Greg na Meja Thomas” akasema Jenerali William na kufanya utambulisho.

“Huyu ni mmarekani mwenzetu ambaye alikuwa hapa Tanzania katika shughuli zake za upigaji picha lakini

alijikuta amenasa katika machafuko na jana amekombolewa na vikosi vya jeshi la Tanzania akaletwa Dar es salaam na leo mchana Rais akanikabidhi.Chloe ataishi na sisi hapa hadi pale hali ya amani itakapokuwa nzuri” akasema Jenerali William na kumtaka Nawal waingie ndani.Miguu ya Nawal ilikuwa inagongana kwa kile alichokuwa amekishuhudia.Katika wale watu walioongozana na Jenerali William aliwashuhudia kwa macho

watu wawili waliokuwa wanawatafuta kwa jasho na damu.Assad Ismail na Sattar Sayf Al Din

“Siamini ninachokiona huu ni kama muujiza mkubwa.Watu wote hawa wawili Assad na Satter wote tunawatafuta kwa kila namna.Hadi mwili wangu unatetemeka sikuwa nimelitegemea kabisa jambo hili.Lakini mbona hawana yale masanduku ya kirusi?Wamekipeleka wapi? Au tayari wamekwisha anza kukisambaza?akajiuliza Nawal

“Usiku wa leo lazima kila kirusi kipatikane.Wamejileta wenyewe kwenye mdomo wa Mamba na hawatatoka salama” akawaza Nawal

Jenerali William akamuelezea Brenda kumpeleka Nawal katika chumba maalum cha mapumziko wakati yeye akiendelea na mazungumzo na wageni wake.Nawal hakwenda katika chumba cha mapumziko bali alielekea moja kwa moja chumbani kwake na kitu cha kwanza alichokifanya ni kuishika simu akampigia Ruby

“Hallo Ruby ! akasema Nawal

“Nawal kuna nini?Mbona unahema haraka haraka namna hiyo?Kuna tatizo? akauliza Ruby

“Ruby wako hapa ! akasema Nawal

“Akina nani Nawal?akauliza Ruby

“Assad na Sattar wote wako hapa.Wamekuja na Jenerali William” akasema Nawal

“Nawal una uhakika ni wenyewe?

“Nimewashuhudia mimi mwenyewe kwa macho yangu.Wamefika muda si mrefu wakiwa wameongozana na Jenerali William”

“Yale masanduku mawili aliyoshuka nayo Sattar ndegeni ambayo tunaamini yana kirusi yameletwa hapo?akauliza Ruby

“Hapana Ruby kirusi hakipo hapa.Yawezekana kuna mahala kimehifadhiwa au yawezekana tayari kimekwisha pelekwa kusambazwa” akasema Nawal

“Hapana bado hakijasambazwa kwani mtu pekee aliyeletwa kuja kusambaza kirusi hicho ni Sattar Sayf Al Din.Kama hayuko nacho hapo basi lazima kirusi hicho kimehifadhiwa sehemu Fulani wakisubiri muda ufike wakisambaze.Nawal usiku huu wa leo lazima tuhakikishe tunakipata kirusi hicho.Ni kufa na kupona leo lazima nyumba hiyo ivamiwe tuwachuku watu hao wote waliomo katika hiyo nyumba na watatuonyesha mahala kilipo kirusi.Nawal

endelea kufuatilia watu hao kama wataondoka au watalala hapo wakati tunaandaa kikosi kwa ajili ya kuvamia nyumba hiyo.Kuanzia mchana wa leo tumekuwa tukiichunguza nyumba hiyo na kuona namna walivyojipanga kiulinzi.Makomando wetu wako tayari na muda utakapowadia watavamia nyumba hiyo.Nawal tunakutegemea sana uweze kuwasaidia timu ya makomando watakapofika hapo" akasema Ruby

“Tayari nimekwisha yasoma mazingira ya hapa na ulinzi ulivyo hivyo hakuna tatizo nitasaidiana na timu itakayofika hapa” akasema Nawal na kumpa Ruby maelekezo kadhaa

Mara tu alipomaliza kuzunguma na Nawal Ruby akampigia Gosu Gosu akamtaka afike ofisini kwake mara moja akamueleza kuhusiana na kile alichoelezwa na Nawal

“Ruby mpaka hapo naamini tayari tumekwisha kipata kirusi.Usiku huu lazima

tuwapate hawa magaidi wote pamoja na kirusi.Nitaongozana na makomando wetu watakaokwenda kuvamia nyumba hiyo” akasema Gosu Gosu

“Hapana Gosu Gosu.Tuwaache makomando waende.Wewe utakuwa na kazi ya kuwahoji akina Assad kufahamu mahala kilipo kirusi pale watakapokuwa wameletwa hapa” akasema Ruby

“Ruby kwa nini hutaki nishiriki katika misheni siku

hizi? Kila ninapotaka kushiriki katika misheni unanizuia.You don’t trust me?akauliza Gosu Gosu

“Si hivyo Gosu Gosu.Sitaki kuyaweka hatarini maisha yako wakati tayari tunacho kikosi kinachoweza kupambana .Kumbuka huko wanakoenda kunalindwa na wanajeshi wa Marekani ambao wana mafunzo ya hali ya juu hivyo itakuwa ni nusu vita.Naamini kikosi chetu cha makomando kina uwezo mkubwa sana wa kuweza kufanikisha misheni hii.Kama

nilivyokuahidi kwamba wewe utafanya kazi ya kuwahoji akina assad watakapoletwa hapa” akasema Ruby

“Ruby imekuaje ukabadili mawazo leo na unataka niwahoji magaidi?akauliza Gosu Gosu

“Kwa namna yoyote ile tunahitaji kukipata kirusi hivyo basi kila aina ya mbinu lazima itumike wakati wa kuwahoji magaidi hao ili waweze kufunguka kirusi kiko wapi”

“Sawa Ruby nitaifanya kazi hiyo” akasema Gosu Gosu

kisha wakatoka kwenda kuanza maandalizi kwa ajili ya misheni ile

****

Kikosi cha makomando tisa wa SNSA kilikaribia kufika katika nyumba anakoishi mkuu wa vikosi vya wanajeshi wa Marekani walioko Tanzania.Wakati kikosi hicho kikiikaribia nyumba hiyo wenzao waliokuwa katika helkopta maalum wanayoitumia katika operesheni mbali mbali za

usiku tayari walikwisha fika usawa wa ile nyumba na walikuwa wanasubiri kupewa taarifa kuwa kila kitu tayari ili helkopta iweze kushuka chini na kushusha kikosi cha makomando ambacho kitadhibiti eneo la juu la nyumba ile.

Nawal ambaye alikuwa ndani ya ile nyumba akapewa taarifa kuhusu vikosi vile kuikaribia nyumba ile.Bado Jenerali William na akina Assad walikuwa wanaendelea na mazungumzo katika sebule ya chini.

Nawal akatoka chumbani kwake taratibu akaenda jikoni ambako hakukuwa na mtu.Ni sauti za maongezi ya akina William ndizo zilisikika.Nawal akiwa na vifaa vyake katika begi akakata waya unaopeleka umeme katika jiko kubwa la kupikia halafu akafanya utundu wa kuunganisha nyaya na shoti kubwa ya umeme ikatokea iliyosababisha umeme kukatika ghafla jumba lote likawa giza.Haraka haraka akarejea chumbani kwake na kuwajulisha akina Ruby

kwamba tayari umeme umekatika.

Baada ya kupewa taarifa ya umeme kukatika,helkopta ya makomando ambayo inatumia teknolojia ya hali ya juu ambayo haina mlio ikaanza kushuka taratibu na ilipofika usawa Fulani makomando wakaanza kushuka kwa kutumia miavuli.Tayari walikuwa wanafahamu upande ule wa juu kulikuwa na wadunguaji sita.Kutokana na giza wadunguaji wale hawakuweza kuwaona makomando wa SNSA

walipokuwa wakishuka na hawakuwa na wazo lolote la kuvamiwa.Waliendelea kuzungumza wakati wakisubiri umeme uwake.

Makomando wa SNSA wote walikuwa wamevaa miwani ya kuwawezesha kuona sehemu za giza na waliweza kuwaona vizuri namna wadunguaji wale waliokuwa juu ya ile nyumba walivyokaa na baada ya kupewa amri risasi kama mvua zilitoka katika bunduki zao zilizofungwa viwambo vya kuzuia sauti.Kufumba na

kufumbua wadunguaji wote walikuwa chini.Makomando wa SNSA wakatua taratibu na kulidhibiti eneo la juu la nyumba ile na kila mmoja akachukua nafasi yake.Baada ya kulidhibiti eneo la juu kazi iliyoifuata ni kuwasafishia njia kikosi cha chini ambao walikuwa mita chache kutoka katika jumba lile.Kwa msaada wa miwani ile waliyokuwa wameivaa ya kuona kwenye giza makomando waliokuwa wametawanyika katika sehemu ya juu ya ile nyumba wakajipanga tayari kwa ajili ya

kuanza kuwaondoa wanajeshi waliokuwa wakilinda upande wa chini.

Ndani ya nyumba bado zoezi la kufuatilia chanzo cha hitilafu iliyopelekea umeme kukatika liliendelea.Wanajeshi walikuwa wanapita chumba kimoja kimoja kuchunguza.Nawal akafungua mlango wa chumba chake akatoka na kuanza kushuka chini akakutana na wanajeshi wale waliokuwa wanafuatilia kujua chanzo cha hitilafu ile ya umeme.Wanajeshi wale wakamtaka radhi kwa hitilafu

ile kutokea wakamuahidi kuwa ndani ya muda mfupi umeme utarejea.

Nawal akapita sebuleni ambako Jenerali William na akina Assad walikuwa wanaendelea na maongezi.Walikuwa wanatumia taa maalum inayotumia betri

“Chloe” akaita Jenerali William baaada ya kumuona Nawal akipita pale sebueleni

“Kumetokea hitilafu ya umeme hapa ndani lakini tatizo hilo linashughulikiwa na muda si mrefu umeme

utarejea” akasema Jenerali William

“Nimeshindwa kukaa ndani kuna joto kali sana ngoja nipunge upepo hapo nje hadi umeme utakaporejea” akasema Nawal na kutoka nje akaenda kujibanza sehemu na kutuma ujumbe kwa Ruby akimjulisha kuwa Assad na Sattar bado wapo mle ndani akawahimiza kufanya hima kwani tayari wamekwisha anza kufuatilia kujua hitilafu ile ya umeme imetokea wapi.

Mara tu baada ya Ruby kupokea ujumbe ule kutoka

kwa Nawal,akampa taarifa mkuu makomando waliokuwa upande wa juu.Tayari kila komando alikuwa amelenga mwanajeshi na amri ikatolewa ya kuwafagia.Mvua ya risasi kutoka katika bunduki zilizofungwa viwambo vya sauti ikaanza kunyesha na baada ya sekunde kadhaa wanajeshi wote walikuwa wakilinda sehemu ya chini ya nyumba ile walikuwa chini.Bila kukawia kikosi cha makomando waliokuwa nje kikafika kwa haraka na kuvuka geti kisha wakachukua nafasi

ili kuhakikisha hakuna hatari yoyote.Nawal akapewa maelekezo kwamba aende akaungane na kikosi kile cha makomando akawafuata na kujitambulisha kwao akawajulisha kuwa watu wanaowatafuta wapo sehemu ya chini ya nyumba ile.Makomando wale wakajipanga vyema na kuanza kusogelea mlango mkubwa wa kuingilia ndani huku wale waliokuwa upande wa juu wa nyumba ile wakishuka chini

Wakati wakiendelea na maongezi Jenerali William

akastushwa na mlio wa kitu akawataka akina Assad wanyamaze kimya

“Kuna nini Jenerali?akauliza Assad na Jenerali William akamfanyia ishara ya kukaa kimya.Zilipita sekunde kadhaa Jenerali William akaupeleka mkono wake wa kulia kifuani kwake akabonyeza kidude katika redio yake ya mawasiliano na kuita

“Charles ! Charles ! Unanisoma?

Hakupata jibu lolote

“Alpha ! Alpha unanisoma?akaita tena lakini hakujibiwa.Akasimama na kutoa bastora yake

“Kuna kitu hakiko sawa hapa ! akasema akionekana kuwa na wasiwasi

“Kuna nin……” Assad akataka kuuliza lakini sauti kali ikawaamuru wasimame kama walivyo.Walivamiwa na watu waliokuwa wamefunika nyuso zao.Kwa kasi ya aina yake Assad akataka kuinyakua bastora yake iliyokuwa mezani lakini kabla mkono wake

haujaifikia akapigwa risasi ya bega akaanguka chini..

“Wekeni silaha zenu chini taratibu” Sauti ikawaamuru Jenerali William na Sattar.Taratibu Jenerali William akaiweka bastora yake chini,Sattar naye akachomoa bastora yake na kuiweka chini wakainua mikono juu.Haraka haraka wakafungwa pingu na kupandishwa sehemu ya juu ya nyumba ile.Assad akapewa huduma ya haraka ya kuzuia damu kuvuja kwa wingi kisha naye akafungwa pingu na kupandishwa juu ambako

tayari helkopta ilikuwa imetua akaingizwa katika helkopta pamoja na akina Sattar.Upekuzi uliendelea ndani ya nyumba ile na baada ya muda wanawake wawili waliokuwa wahudumu wakatolewa na kuingizwa katika helkopta kisha ikapaa na kuondoka.

Ruby na makomando wengine wakaingia katika magari yao mawili na kuondoka eneo lile.

“Hii ni moja ya operesheni tamu sana ambayo nimewahi kushiriki.Wanajeshi wale

hawakujua kama wanaweza kuvamiwa hivyo hawakuwa wamejiandaa.Sifahamu Marekani watatoa tamko gani kesho asubuhi pale watakapokuta miili ya wanajeshi wao wakiwa wameuawa.Lakini haya yote ni malipo ya udhalimu wao.Usiku wa leo hakuna kulala hadi kirusi kipatikane.Haijalishi damu kiasi gani itamwagika lakini lazima kirusi kipatikane” akawaza Nawal akiwa garini wakielekea makao makuu ya SNSA.

****

Helikopta ilitua ofisi kuu za SNSA ,mtu wa kwanza kushushwa alikuwa Assad aliyekuwa amepigwa risasi ya bega akakimbizwa katika kitengo cha afya ili kupatiwa matibabu.Wakashushwa Jenerali William na Sattar wakiwa wamefungwa pingu na kufunikwa na mifuko vichwani Gosu Gosu akaelekeza wapelekwe katika chumba cha chini ya ardhi.Mwisho wakashushwa wale wahudumu

wawili wakapelekwa katika chumba kingine

“Ahsanteni sana kwa kazi nzuri” akasema Ruby baada ya kupewa taarifa ya namna operesheni ile ilivyokwenda

“Makomando wameimaliza kazi yao sasa mpira umekuja kwetu” akasema Gosu Gosu

“Gosu Gosu leo nakuachia uhuru fanya kila uwezalo kuwafungua hawa watu.Kipaumbele cha kwanza ni kujua mahala kilipo kirusi na baada ya hapo tutaendelea kuwahoji mambo mengine

yanayohusiana na machafuko yaliyotokea lakini angalizo Gosu Gosu jitahidi kudhibiti hasira” akasema Ruby

“Usihofu Ruby kabla ya mapambazuko lazima tuwe tumekipata kirusi” akasema Gosu Gosu na kumsubiri Nawal ili kazi ya kuwahoji watu wale waliokamatwa ianze mara moja.

TEHRAN – IRAN

Saa nne za usiku kwa saa za Iran,waziri wa ulinzi wa Iran brigedi Jenerali Ahsan

Javad aliwasili katika makazi ya bilionea Vahid Ghorbani.Alipokewa na Vahid mwenyewe na kumkaribisha ndani.Vahid ni mmoja wa wafanya biashara wakubwa na wanaoheshimika sana nchini Iran.

“Karibu sana Ahsan” akasema Vahid

“Nashukuru Vahid na samahani kwa kuchelewa kuja.Nilikuwa na mambo mengi sana siku ya leo” akasema Brigedia Jenerali Ahsan.

“Usijali Ahsan.Ninafahamu majukumu yako mengi” akasema Vahid na baada ya maongezi mafupi ya utangulizi Ahsan akasema

“Vahid nimepita kwako mara moja kukusikilza kama ulivyoniomba.Nikitoka hapa kuna sehemu ninaelekea hivyo sintachukua muda mrefu hapa kwako” akasema Ahsan

“Ahsan nimekuita hapa ninahitaji msaada wako”

“Unahitaji nikusaidie nini Vahid?

“Kuna raia wetu waliokuwa wamepotea wamerejea leo” akasema Vahid

“Ndiyo wamerejea leo.Umekuwa ni kama mujiza kwetu kwani tayari tulikwisha hisi wameuawa.Hatukuwa na tegemeo la kuwaona tena wakiwa hai.Tumefurahi sana kuwaona tena ndugu zetu wale” akasema Ahsan

“Kuna mtu mmoja alikuwa ameongozana nao ambaye si raia wa Iran anaitwa Abu Zal…….” akasema Vahidi lakini Ahsan akamkatisha

“Abu Zalawi.Kwa taarifa tuliyoipata ni raia wa Saudi Arabia na anajishughulisha na ugaidi.Abu Zalawi ndiye aliyelipua ubalozi wa Marekani jijini Dar es salaam siku chache zilizopita” akasema Ahsan na kumstua sana Vahid

“Ni gaidi?! Vahid akauliza kwa mshangao

“Ndiyo ni gaidi !

“Hii inashangaza”akasema Vahid

“Ni jambo linalomshangaza kila mtu lakini tutawafanyia mahojiano na kujua nini hasa kimetokea

hadi watu wetu wakajikuta wakiwa na huyu gaidi” akasema

“Nini mipango yenu kuhusiana na huyu mtu?Hamuoni kama anaweza kuongeza matatizo na Marekani endapo wakifahamu kuwa mtu aliyelipua ubalozi wake yuko hapa nchini kwetu? Akauliza Vahid

“Kwa sasa ni mapema sana kusema chochote kuhusu huyu mtu hadi pale tutakapowahoji watu wetu na kufahamu kwa undani nini hasa kilichotokea na imekuaje wakajikuta

wakiwa na huyu gaidi.Baada ya hapo tutafanya maamuzi” akasema Ahsan na ukimya mfupi ukapita

“Mbona umeuliza kuhusu huyu jamaa? Akauliza Ahsan

“Ahsan kuna jambo nataka kuliomba.Yawezekana ni jambo kubwa na hukulitegemea lakini nakuomba unisaidie”

“Sema unachohitaji Vahdi nitakusaidia,wewe ni zaidi ya rafiki” akasema Ahsan

“Ninataka kuonana na Abu Zalawi” akasema Vahid na

mstuko mkubwa ukaonekana usoni kwa Ahsan

“Unataka kuonana na Abu Zalawi? Akauliza Ahsan akiwa bado anashangaa.Hakutegemea kama Vahid angeweza kumuomba kitu kama kile

“Ndiyo Ahsan ninataka kuonana na Abu Zalawi”

Ahsan akavuta pumzi ndefu na kuuliza

“Vahid mimi nawe tumefahamiana muda mrefu sana toka tukiwa vijana wadogo masomoni na tumeendelea kuwa marafiki

wakubwa hata sasa.Nini sababu ya kutaka kuonana na huyu mtu? Naomba unieleze bila kunificha tafadhali” akasema Ahsan

“Nilikueleza kuhusiana na kifo cha mwanangu Najma”

“Ndiyo ulinieleza”

“Kuna jambo ambalo sikuwa nikilifahamu kuhusiana na Najma ambalo nimelifahamu leo hii” akasema Vahid na kunyamaza kidogo halafu akaendelea

“Najma alikuwa ameolewa lakini alifanya siri hakutaka nifahamu”

“Alikuwa ameolewa?

“Ndiyo lakini kwa siri na hakutaka nifahamu.Kwa mujibu wa mama yake alitaka kunipa taarifa hizo yeye mwenyewe lakini hakufanya hivyo hadi mauti yalipomkuta.Kwa bahati mbaya aliyekuwa mume wake ni Abu Zalawi”

“Abu Zalawi?! Ahsan akazidi kushangaa

“Ndiyo.Nimeambiwa kwamba ndiye aliyekuwa mume wa Najma”

“Najma ametoka wapi na huyu gaidi? Binti yako alikuwa

ni msomi mzuri na mwenye sura ya kimalaika inawezekanaje hadi akajikuta akiingia katika mahusiano na huyu jamaa?akauliza Ahsan

“Ahsan hata mimi sifahamu nini kilitokea lakini nilichoelezwa ni hicho kwamba aliolewa na Abu Zalawi” akasema Vahid

“Vahid yawezekana si Abu Zalawi huyu gaidi.Yawezekana kuna Abu Zalawi mwingine” akasema Ahsan

“Ahsan ninaomba msaada wako niweze kuonana na huyu Abu Zalawi na kuzungumza

naye japo kwa dakika tano tu ili niweze kupata uhakika kama kweli ni yeye aliyemuoa mwanangu Najma” akasema Vahid

“Sawa nitakusaidia Vahid.Nilikueleza kuwa nikitoka hapa ninaelekea sehemu Fulani.Ninakwenda kuwatembelea mashujaa wetu waliorejea leo kujua maendeleo yao na kwa kuwa umeniomba basi baada ya kutoka hapo hospitali tutaelekea mahala alikopelekwa Abu Zalawi ukaonane naye” akasema

Ahsan.Hakukuwa na muda wa kupoteza wakaingia katika gari la Ahsan na kuondoka kuelekea hospitali.

****

Saa tano za usiku waziri wa ulinzi wa Iran Brigedia Jenerali Ahsan Javad aliwasili katika hospitali ya jeshi walikopelekwa Yasser Wazir na wenzake baada ya kurejea nyumbani wakitokea mahala kusikojulikana.Mpaka muda huu hawakuwa wamehojiwa chochote kuhusiana na mahala

walikokuwa kwa muda wote waliokuwa wamepotea.Brigedia Jenerali Ahsan Javad hakuwa peke yake alikuwa ameongozana na Sassan Mahmoud anayeongoza wizara ya ujasusi ya Iran MOIS na vile vile alikuwa na Vahid Ghorbani mfanyabiasha mkubwa nchini Iran na rafiki yake wa karibu.

Waliwatembelea na kukagua maendeleo ya akina Yasser na kujiridhisha kuwa wanapatiwa huduma ya afya ya hali ya juu.Baada ya hapo wakaondoka kuelekea mahala

alikopelekwa Abu Zalawi.Baada ya mwendo wa dakika kadhaa wakafika katika nyumba moja kubwa yenye ulinzi mkali inayotumiwa na MOIS kwa shughuli zake na kubwa zaidi ikiwa ni kuhifadhi watu mbali mbali wanaohojiwa na idara hiyo.

Geti la nyumba likafunguliwa magari yakaingia,milango ikafunguliwa haraka haraka na msimamizi mkuu wa nyumba ile akatoka kuja kuwapokea wageni akawakaribisha ndani

“Anaendeleaje mgeni wetu? Akauliza Sassan Mahmoud mkuu wa MOIS

“Anaendelea vizuri.Kabla ya kumleta hapa tulimpeleka kwanza katika hospitali yetu akaangaliwa afya yake na kupatiwa matibabu ndipo tukamleta hapa.Anaendelea vizuri” akasema Yule msimamizi wa ile nyumba kisha Ahsan akamtaka Sassan wazungumze pembeni.Baada ya mazungumzo yaliyochukua dakika zipatazo tano Sassan akamtaka Yule msimamizi wa ile nyumba kuzima kamera

zote kwa muda halafu akamtaka awapeleke katika chumba alimowekwa Abu Zalawi.Mlango wa chumba ukafunguliwa wakaingia ndani na kumkuta Mathew akiwa amejilaza kitandani akiwa amefungwa bandeji sehemu mbali mbali za mwili wake zilizokuwa na vidonda.Mathew hakuwa na wasiwasi hata chembe akainua kichwa chake akawatazama watu wale waliokuwa wanamtazama kwa woga

“Abu Zalawi unaendeleaje?akauliza Ahsan

“Ninaendelea vizuri” akajibu Mathew

“Karibu sana Iran.Mimi naitwa Brigedia Jenerali Ahsan Javad waziri wa ulinzi wa Iran.Nimekuja kukutazama kujua maendeleo yako”

“Ahsante mheshimiwa waziri ninaendelea vyema”

“Sawa Abu ninashukuru kama unaendelea vyema.Mimi nawe tutakuta tena pale afya yako itakapokuwa imekaa vizuri.Kwa sasa endelea kupumzika na ninakuhakikishia uko salama

hivyo siwe na hofu yoyote” akasema Ahsan

“Nashukuru sana mheshimiwa waziri” akasema Mathew

“Kabla sijaondoka kuna mtu ambaye anahitaji kuonana nawe” akasema Ahsan na Vahid akaitwa mle chumbani.Watu wote wakatoka na kuufunga mlango akabaki Mathew na Vahid.

“Karibu” akasema Mathew akimshangaa Vahid namna alivyokuwa akimtazama

“Abu Zalawi” akasema Vahid kwa sauti ndogo

“Ndiyo ni mimi karibu.Wewe ni nani? Akauliza Mathew ambaye aliinuka na kukaa kitandani

“Naitwa Vahid Ghorbani”

“Karibu Ghorbani.Nikusaidie nini? Akauliza Mathew.Vahid akatoa simu na kuzitafuta namba za Habiba akapiga

“Kabla sijazungumza nawe chochote kuna mtu ambaye unatakiwa uzungumze naye simuni” akasema Vahid na kumpatia Mathew ile simu

“Hallow” ikasema sauti ya mwanamke upande wa pili

sauti ambayo haikuwa ngeni masikioni mwa Mathew

“Hallow” akasema Mathew

“Mathew Mulumbi.Nimefurahi tena kuisikia sauti yako.Unazungumza na Habiba” akasema Habiba Jawad akitumia lugha ya kiswahili

“Mama Habiba.! Akasema Mathew naye akishangaa

“Mathew sina muda mwingi wa kuzungumza nawe.Kuna jambo ambalo nataka nikufahamishe” akasema Habiba

“Nakusikiliza mama”

“G20 tayari wamefahamu kila kitu kuhusu wewe kuwa si gaidi bali ni jasusi” akasema Habiba na Mathew akastuka sana

“wamefahamuje?akauliza Mathew

“Wamepata taarifa zote kutoka Mossad”

“Bastard ! akasema Mathew kwa hasira

“Usihofu Mathew japokuwa wamefahamu kila kitu kuhusu wewe lakini kila kitu kinaendelea kama kawaida.Misheni yako

inaendelea kama kawaida kwani tayari ndani ya G20 wamekwisha gawanyika.” akasema Habiba na kumueleza Mathew kila kitu kinachoendelea

“Kwa hiyo Mathew nimekupigia kukupa tahadhari kuhusiana na mpango huu wa kukuua kwa kuwatumia majasusi wa Mossad” akasema Habiba

“Mama nakushukuru sana kwa kunipa tahadhari kuhusiana na mpango huo wa kuniua.Ninakuahidi sintaishia

njiani nitahakikisha ninalimaliza hili kundi la G20”

“Nakutakia kila la heri Mathew.Kila nitakapokuwa nikipata taarifa zozote nitajitahidi nikufikishie lakini ukiona kimya kwa muda wa wiki moja kuanzia sasa ujue tayari nimekwisha kufa”

“Mama Habiba tafadhali endel……”

“Kwa heri Mathew.Kuwa makini” akasema Habiba na kukata simu.

“Tayari umeupata ujumbe wako? Akauliza Vahid

“Ndiyo nimeupata ninashukuru sana” akasema Mathew na kumrejeshea Vahid simu yake

“Abu Zalawi nimepewa muda mfupi wa kuzungumza nawe.Naamini mimi hunifahamu na hujawahi kuniona”

“Ni kweli sikufahamu” akasema Mathew

“Mimi ni……” akasema Vahid na kusita

“Karibu Iran Abu Zalawi” akasema Vahid na kugonga mlango ukafunguliwa Mathew akabaki anashangaa

“Alitaka kunieleza nini huyu jamaa halafu akasita?akajiuliza Mathew na kuinuka akaketi kitandani.

“Kazi imekuwa kubwa zaidi ya nilivyodhani.Kama hawa jamaa tayari wamekwisha nifahamu mimi ni nani na wanataka kuniua natakiwa kutumia akili kubwa ili waweze kuniamini tena.Kwa namna yoyote ile lazima nirejee tena Marekani kumaliza kazi niliyoianza.Siwezi kuishia njiani lazima nifike mwisho na kukifutilia mbali kikundi cha

G20.Namshukuru Habiba kwa kunipa taarifa za mpango wao wa kutaka kuniua.Nina wasiwasi sana kama wakati nitakapomaliza misheni yangu Habiba ataendelea kuwa hai kwani hawa jamaa tayari wanadai amewasaliti.Naomba Mungu amsaidie huyu mama awe hai na ashuhudie kwa macho yake namna kundi la G20 linavyosambaratishwa” akawaza Mathew

“Kama wanataka kuniua mimi na kusitisha ile misheni waliyonituma,ninapata picha kwamba hata wale jamaa

niliowaokoa watakuwa mashakani.Naamini nao pia watakuwa katika mpango wa kuuawa ili isijulikane kama walikuwa wametekwa na Marekani.Lazima niwasadie kwani wale ndio kinga yangu” akawaza Mathew

Baada ya kutoka katika chumba cha Mathew,Vahid alipelekwa katika gari ambako Brigedia Jenerali Ahsan alikuwa anamsubiri,kisha wakaondoka

“Nimeshindwa kumwambia Abu Zalawi kuwa mimi ndiye baba yake

Najma.Nimejikuta nikimuonea huruma ghafla Yule kijana baada ya kumuona namna mwili wake ulivyo na vidonda vingi.Kwa nini kijana Yule akaamua kujiingiza katika masuala ya ugaidi.Kwa nini Mossad wanataka kumuua?Ninahitaji kupata tena wasaa mwingine nizungumze naye kwa kirefu zaidi" akawaza Vahid wakiwa garini baada ya kuondoka mahala alikopelekwa Mathew

Wakati Ahsan na Vahid wakiondoka katika nyumba alikopelekwa Mathew,katika

moja ya mtaa jijini Tehran watu watatu walikuwa wamekaa juu ya nyumba Fulani wakizungumza.Wawili miongoni mwa watu hao walikuwa majasusi kutoka Mossad walioko jijini Tehran

“Nawaahidi hadi kufika kesho mchana tayari nitakuwa nimepata taarifa za mahala alipo Abu Zalawi pamoja na wale raia wengine waliokuwa wamepotea” akasema Zana Behnam ambaye anafanya kazi katika wizara ya ujasusi na usalama wa taifa ya Iran.

“Tunashukuru Zana.Tunaamini hautatuangusha” akasema Avner jasusi kutoka Mossad

“Siwezi kuwaangusha.Mimi nanyi tumekwisha shirikiana katika mambo mengi” akasema Zana.Avner akatoa bahasha kutoka katika mfuko wa koti na kumpatia Zana

“Hiki ni nusu ya kiasi cha fedha ulichokihitaji kwa ajili ya kazi hii.Pale utakapokuwa umekamilisha jukumu lako basi utamaliziwa kiasi kilichobaki” akasema Avner na

bila kuhesabu Zana akaiweka bahasha mfukoni wakaagana

DAR ES SALAAM – TANZANIA

“Nawal hongera sana umefanya kazi nzuri” akasema Ruby baada ya Nawal kuwasili na gari la makomando

“Ahsante Ruby lakini tutapata muda wa kuzungumza na kupongezana hapo baadae kwa sasa tunatakiwa kuitumia vyema kila dakika tuliyonayo kabla ya mapambazuko ili kufahamu

mahala kilipo kirusi na kukichukua kwani ikifika asubuhi itagundulika kile tulichokifanya na yawezekana tusikipate tena kirusi hicho hivyo kufa au kupona lazima usiku huu kirusi kipatikane.Tunao watu wanaofahamu mahala kirusi kilipo hivyo hakuna kuwaonea huruma lazima tutumie kila mbinu hadi waonyeshe walipokificha kirusi hicho” akasema Nawal na mkuu wa kikosi cha makomando akatokea na kumkabidhi Ruby vazi Fulani

“Hili ni moja ya vazi tumelikuta katika nyumba ile baada ya kufanya upekuzi.Yapo mengine kumi na sita na vazi hili ni maalum kwa ajili ya kujikinga na hewa ya sumu au maambukizi ya virusi”akasema

“Washenzi hawa walikwisha jiandaa kujikinga na virusi wakati sisi tukiteketea” akasema Ruby

“Mtu wa kwanza kumuhoji ambaye anafahamu kilipo kirusi ni Jenerali William.Huyu nitamuhoji mimi mwenyewe” akasema

Gosu Gosu kisha maandalizi kwa ajili ya kuanza kumuhoji Jenerali William yakaanza.Maandalizi yalipokamilika Jenerali William akaingizwa katika chumba maalum kwa ajili ya mahojiano.Gosu Gosu Ruby na Nawal walimtazama katika kioo kikubwa wakiwa katika chumba kingine .Gosu Gosu akavuta pumzi ndefu na kutoka ndani ya kile chumba akaingia katka chumba cha mahojiano akavuta kiti na kuketi

“Habari yako Jenerali William” akasema Gosu Gosu lakini Jenerali William hakujibu kitu akamtazama Gosu Gosu kwa macho ya dharau

“Naitwa Papi Gosu Gosu,ni mwanajeshi.Kwa miaka zaidi ya ishrini nimeishi msituni nikipigana vita hivyo nataka tuzungumze kama wanajeshi” akasema Gosu Gosu na Jenerali William akacheka kidogo

“Nini maana ya mchezo huu mlioufanya?akauliza Janerali William

“Huu ni mchezo wa kijinga sana mmeufanya.Sisi tuko hapa kwa ajili ya kuwasaidia kutafuta amani katika nchi yenu halafu ninyi mnatufanyia hivi ! Ninawahakikishia kwamba hiki mlichokifanya kitakuwa na athari kubwa sana kwenu.Hamtabaki salama hata kidogo ! akasema Jenerali William

“Huna hata aibu ya kusema mmekuja kutusaidia ! Akasema Gosu Gosu akionekana kuanza kupandwa na hasira

“Ndiyo tumekuja kukusaidieni kutafuta amani baada ya kuanza kuuana wenyewe kwa wenyewe lakini malipo yake ndiyo haya.Mnafanya jambo bay asana kuteka na kuua walinda amani ! akafoka Jenerali William

“Jenerali William sisi si watoto wadogo wa kushindwa kutambua mambo.Karibu vurugu nyingi zinazotokea barani Afrika nchi zilizoendelea zina mkono wake.Mnatengeneza machafuko kwa malengo

mnayoyajua wenyewe halafu mnaleta vikosi vyenu mkijidai mnakuja kutusaidia kutafuta amani kumbe mna ajenda zenu za siri.Tunafahamu kila kitu mnachokifanya Afrika na sasa mwisho wenu umefika ! akasema Gosu Gosu

“Sisi hatuna sababu yoyote ya kuleta machafuko kwa bara masikioni kama hili.Sisi ni taifa kubwa lenye uchumi mkubwa kuliko yote duniani.Ni taifa lenye nguvu kubwa kijeshi kuliko yote duniani kwa nini tusumbuke na watu masikini kama

waafrika? Hizo ni dhana potofu mnazojenga kwamba vikosi vya Marekani au nchi nyingine kubwa vikija kulinda amani Afrika vinakuwa na ajenda zao za siri wakati si kweli.Sisi ni taifa linaloheshimu haki za binadamu na hatuko tayari kuona haki za binadamu zikivunjwa na watu kuuawa ndiyo maana tuko mstari wa mbele katika kuhakikisha tunapeleka vikosi vyetu haraka sana sehemu yoyote ile ambako kuna kuwa na uvunjifu mkubwa wa haki za

binadamu.Tazama hivi majuzi vurugu zilizotokea hapa nchini kwenu mkaanza kuuana wenyewe kwa wenyewe kwa sababu ya dini hivyo kwa sababu ya dini,tumeleta vikosi vyetu kuja kuwasaidia kutafuta amani !

“Mwongo mkubwa wewe ! akasema Gosu Gosu kwa ukali huku akigonga meza

“Nilikwambia tunafahamu kila kitu mlichokifanya na mipango yenu yote tunaifahamu hivyo usijaribu kunidanganya.Unadhani hatujui mnachokifanya kule

Tanga? Tunafahamu namna mnavyopora tani na tani za mafuta ya kutoka Uganda.Tunafahamu machafuko haya yote yaliyotokea mmeyatengeneza ninyi kwa ajili ya kujipatia mafuta.Tunafahamu kila kitu Jenerali na msituone tuko kimya mkajua kuwa hatufahamu chochote ! akasema Gosu Gosu kwa ukali

“Hiki ni kichekesho wewe kijana.Marekani haina haja ya kuja kuchukua mafuta huku Afrika.Tuna akiba kubwa ya mafuta na tunaendelea

kutengeneza mafuta ya kutosha kutoka katika mimea na tumewekeza sana katika teknolojia rahisi ya kutengeneza magari na mitambo isiyotumia mafuta mengi hivyo basi hatuna haja na mafuta machafu kutoka Uganda ! akasema Jenerali William kwa dharau

“Gosu Gosu kompyuta yetu inatuonyesha William amepatwa na mstuko mkubwa ulipomtajia suala hilo la kuchukua mafuta kule Tanga.Endelea kukazia hapo hapo ! Ruby akamjulisha Gosu

Gosu kupitia kifaa alichokuwa amekivaa sikioni.

“Tunafahamu kila kitu Jenerali William kuhusiana na mipango yenu yote mnayoipanga na magaidi wa IS.Bado muda kidogo tu dunia yote itafahamu kila kitu ambacho kinafanywa na taifa lako kwa siri.Itakuwa ni aibu kubwa kwa taifa kubwa kama Marekani pale tutakapoitangazia dunia namna inavyozinyonya nchi masikini ! akasema Gosu Gosu na Jenerali William

akaonekana kupandwa na hasira

“Huo ni upumbavu mkubwa ! akahamaki Jenerali William

“Marekani haiwezi kushirikiana na magaidi wa IS au kikundi chochote cha kigaidi.Tumekuwa mstari wa mbele katika kupambana ugaidi duniani na katu hatuwezi kushirikiana nao.Hiki unachokitamka ni kitu cha kijinga sana ! akasema kwa ukali Jenerali William huku akijaribu kuitikisa mikono yake lakini ilikuwa

imefungwa barabara kwa pingu zilizo katika kiti kile maalum.

Gosu Gosu akalifungua faili akatoa picha ya Assad Ismail

“Unamfahamu huyu? Akauliza Gosu Gosu

“Wewe kijana una upungufu wa akili,maswali gani hayo unaniuliza?

“Jenerali William hapa hauna nguvu ya kufanya chochote,tafadhali jibu kile unachoulizwa kwa ufasaha” akasema Gosu Gosu

“Kwa nini mmenileta hapa ninyi watu wenye akili finyu? Akafoka Jenerali William

“Sisi tuna akili finyu? Leo utafahamu watu wenye akili finyu ni watu wa aina gani ! akasema Gosu Gosu

“Unamfahamu huyu mtu pichani? Gosu Gosu akauliza

“Simfahamu mtu huyu ! akajibu Jenerali William

“Hujawahi kumuona sehemu yoyote? Akauliza Gosu Gosu

“Nimekwambia sijawahi kumuona na simfahamu ! akajibu Jenerali William

“Kama humfahamu ninakufahamisha kuwa huyu anaitwa Assad Ismail ni kiongozi wa kundi la kigaidi la IS ambaye ndiye mnayemtumia katika kuchochea vurugu za kidini hapa nchini.Yeye na kundi lake ndio wanaofanya mauaji ya viongozi wa dini na kushambulia nyumba za ibada ili kujenga chuki miongoni mwa waumini na kusababisha washambuliane na kuuana” akasema Gosu Gosu na sura ya Jenerali William ikabadilika.Gosu Gosu

hakumjali akatoa picha nyingine

“Nafahamu hata nikikuuliza huyu ni nani utakana kumfahamu lakini huyu anaitwa Sattar Sayf Al Din.Naye vile vile ni mfuasi wa IS” akasema Gosu Gosu.Jenerali William alikosa maneno ya kuongea akabaki anaikodolea macho picha ile.Gosu Gosu akatoa picha nyingine akaiweka mezani.

“Picha hii ni ya mchana wa leo.Hapa ni uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere Dar es salaam ambapo

Sattar aliwasili akitumia ndege aina ya Gulfstream G650ER na ndege hii hutumiwa na shirika la ujasusi la Marekani CIA” akasema Gosu Gosu na kumtazama Jenerali William ambaye macho yake aliyaelekeza katika ile picha mezani.Gosu Gosu akatoa picha nyingine

“Hapa Sattar akishuka ndegeni akiwa ameongozana na wanajeshi wa Marekani.Ukiitazama picha hii Sattar ana masanduku mawili.Tunafahamu masanduku haya mawili yana

kirusi ndani yake ambacho Sattar amekuja kukisambaza hapa Tanzania”

“Sielewi unachokizungumza wewe kijana ! akafoka Jenerali William

“Utanielewa tu Jenerali William” akasema Gosu Gosu

“Marekani baada ya kufanikiwa katika mpango wake wa kuchukua mafuta ya Uganda kupitia bandari ya Tanga wana hofu kwamba amani itarejea muda si mrefu na vikosi vya Marekani havitahitajika tena kuwepo

hapa Tanzania hivyo zoezi la uchukuaji wa mafuta litakoma.Mmetafuta namna ya kuviwezesha vikosi vyenu kuendelea kuwepo hapa nchini kwa muda mrefu zaidi na mmekuja na mpango wa kusambaza kirusi hatari cha maangamizi hapa Tanzania ili muweze kuongeza vikosi zaidi.Jenerali William sisi tuna akili finyu kama ulivyosema lakini tunafahamu kila kitu kuhusiana na mipango yenu na ninakuhakikishia kwamba mipango yenu haitaweza

kufanikiwa” akasema Gosu Gosu

“Huu ni upuuzi uliopitiliza ! akafoka Jenerali William

“Jenerali William kuna kitu kimoja tu ambacho ninataka kufahamu kutoka kwako ambacho ndicho kitakachokutoa salama humu ndani.Nataka kujua kirusi hiki alichokuja nacho Sattar kiko wapi? Akauliza Gosu Gosu na kumtazama Jenerali William

“Gosu Gosu usimuulize tena swali lingine muache kwanza atafakari njoo huku”

Ruby akamwambia Gosu Gosu ambaye aliinuka

“Ninakuacha utafakari baada ya muda nitarejea tuendelee na mazungumzo yetu.Nakupa angalizo Jenerali William mimi ni mtu mbaya mno na usiombe uingie katika anga zangu ! Nitarejea baada ya muda mfupi ! akasema Gosu Gosu na kuchukua faili lake akatoka ndani ya kile chumba akaingia katika chmba walichokuwamo akina Ruby

“Umemuanza vizuri na kompyuta yetu hapa inatuonyesha kwamba

amepatwa na mstuko mkubwa.Hakutegemea kama tungefahamu mipango yao ya siri.Pamoja na hayo kuna jambo lingine ambalo tumelipata.Tumeifahamu familia yake.Ana watoto wawili wa kike ambao majina yao ni Cynthia na Lisa.Vile vile ana mke anaitwa Deborah” akasema Ruby na kumpatia Gosu Gosu picha za familia ya Jenerali William

“Hii familia yake ni silaha ya mwisho ambayo tutaitumia katika kumfanya Jenerali William afunguke endapo njia

nyingine za kumfungua zitashindikana.Kabla ya kurejea kumuhoji Jenerali William tutamuhoji kwanza Sattar na zoezi hili mtalifanya wewe na Nawal.Wakati mkiendelea kumuhoji Sattar tutaendelea kumtesa Jenerali William kwa kufungua muziki mkubwa” akasema Ruby na bila kupoteza muda Nawal na Gosu Gosu wakaenda katika chumba kingine cha mahojiano alimo Sattar.Nawal akavuta kiti akaketi Gosu Gosu akasimama pembeni

“Sattar Sayf Al Din ndilo jina lako? Akauliza Nawal lakini Sattar hakujibu kitu.Gosu Gosu ambaye mikono yake ilikuwa myepesi akakishika kichwa cha Sattar na kukigongesha katika meza mara mbili

“Ukiulizwa kitu unajibu haraka ! akafoka Gosu Gosu

“Nakuuliza tena jina lako ni Sattar Seyf Al Din? Akauliza Nawal

“Ndiyo.Naitwa Sattar Sayf Al Din”

“Umetokea nchi gani?

“Mimi ni raia wa Syria”

“Umeingia Tanzania ukitokea Syria?akauliza Nawal

“Hapana nimetokea Marekani”

“Umekuja kufanya nini Tanzania? Akauliza Nawal na Sattar akawa kimya

“Nakuuliza Sattar Tanzania umekuja kufanya nini? akauliza tena Nawal lakini Sattar hakujibu

“Nawal hatuna muda wa kupoteza na hawa watu ! akasema Gosu Gosu na kwenda katika meza iliyokuwa na vifaa mbali mbali akachukua vifaa kadhaa na

kumfuata Sattar.Nawal naye akasimama na kumsogelea Sattar

“Sattar nakuuliza kwa mara ya mwisho umekuja kutafuta nini Tanzania? Akauliza Nawal lakini Sattar aliendelea kuwa kimya.Gosu Gosu hakumkawiza akamnasa kofi zito lililomfanya Sattar aone nyota nyota halafu Nawal akakikamata kichwa chake akakigandamiza katika kiti Gosu Gosu akaupanua mdomo na kuingiza kifaa mdomoni na kulishika jino moja akaling’oa kwa nguvu damu zikaaza

kumwagika huku Sattar akipiga makelele kwa maumivu makali aliyoyapata.

“Leo tutaelewana ! akasema Gosu Gosu

“Sattar nakuuliza umekuja kufanya nini Tanzania? Nataka ujibu ama sivyo mateso haya yataendelea na tutakuondoa kiungo kimoja kimoja ! akasema Nawal lakini Sattar aliendelea kupiga kelele.Nawal akamfanyia ishara Gosu Gosu wakamkamata tena na kuondoa jino lingine Sattar akapoteza fahamu.

“Ruby tunaomba watu wa afya waje haraka humu ndani wamuhudumie huyu mtu atakapozinduka zoezi litaendelea.Wakati tunamsubiri tunarejea kwa Jenerali William” akasema Gosu Gosu kisha wakatoka ndani ya kile chumba wakaelekea katika chumba alimo Jenerali William.Mara tu Gosu Gosu alipoingia mle ndani muziki ukazimwa.Macho ya Jenerali William yalikuwa yanatoa machozi

“Kwa nini mnanifanyia hivi?Nawaambia mmekosea sana kunifanyia haya” akasema Jenerali William

“Huu ni mwanzo tu Jenerali William bado mengi yanakuja.Marekani mlikuwa mkiwakamata watuhumiwa wa ugaidi na kuwapeleka katika gereza la Guantanamo kuwatesa na leo umefika katika Guantanamo ya Afrika.Utakutana na mateso kama mliyokuwa mkiwatesa wale magaidi hadi pale utakapofunguka na kusema ukweli” akasema Gosu Gosu

“Nani amewatuma mnifanyie haya? Hiki unachokifanya wewe kijana kitakuwa na athari kubwa sana kwa nchi yako ! akasema Jenerali William

“William tunaanzia pale tulipoishia katika awamu ya kwanza.Ninataka kufahamu kirusi alichokuja nacho Sattar Sayf Al Din kiko wapi? Akauliza Gosu Gosu

“Wewe kijana nimekwisha kwambia una akili pungufu.Sifahamu una maanisha nini

unapozungumzia kirusi ! akafoka Jenerali William

“Sattar Al Din ambaye hadi usiku huu ulikuwa naye katika makazi yako ameleta hapa nchini kirusi kwa lengo la kukisambaza.Nataka kufahamu kilipo kirusi hicho” akasema Gosu Gosu

“Sifahamu chochote kuhusiana na kirusi hicho unachokizungumzia” akasema Jenerali William

“Jenerali nitazame vizuri nimechafuka damu.Nimetoka kumuhoji Sattar Sayf Al Din ambaye ameleta kirusi hapa

nchini na amekiri kukukabidhi wewe kirusi hicho.Nataka uniambie kilipo kirusi hicho” akasema Gosu Gosu

“Sikuelewi unachokiongea wewe kijana.Tafadhali naomba mnifungue haraka sana kabla ya vikosi vya Marekani havijavamia mahala hapa ! akafoka Jenerali William

“Hakuna kikosi chochote kitakachothubutu kufika mahala hapa na hawatafahamu kamwe kama uko hapa hivyo juhudi za kutoka hapa ni zako wewe mwenyewe.Ninakuhakikishia

William kirusi tutakipata na tutakwenda kukisambaza Marekani” akasema Gosu Gosu na kufungua faili lake akatoa picha ya mke wa Jenerali William akaiweka mezani

“Mkeo Deborah” akasema Gosu Gosu na kutoa picha za watoto wa William akaziweka mezani

“Hiyo ni familia yako ambayo nina uhakika unaipenda kuliko kitu chochote.Utajisikiaje pale utakaposikia kuwa wameathiriwa na kirusi hiki ambacho mmekileta

mkisambaze hapa Tanzania? Watoto hawa wadogo watapoteza maisha na watakufa kifo chenye mateso makali.Hebu fikiria mwanamke mrembo kama huyu Debor……”
Akasema Gosu Gosu lakini Jenerali William akatoa ukelele wa hasira

“Aaagghhhh !! akapiga kelele Jenerali William huku akijitikisa katika kiti akijaribu kutaka kuking’oa lakini kilikuwa kiti imara

“Ninasema waacheni familia yangu katika hili ! akafoka Jenerali William

“Ninarudia tena kukuhakikishia Jenerali William kwamba tutakipata kirusi na baada ya kukipata tutakirejesha Marekani ambako tutakisambaza na tunaanzia katika familia yako na ukumbuke kwamba kirusi hiki hakina tiba wala kinga.Lakini usihofu nitakupa simu utazungumza nao na kuwaaga pale watakapokuwa wameanza kuumwa” akasema Gosu Gosu

“Nitakuua ! Nitakuua mkiigusa familia yangu ! akafoka Jenerali William

“Huwezi kufanya chochote Jenerali William.Kitu pekee ambacho kinaweza kukusaidia ni kutuonyesha mahala kilipo kirusi hicho ili kujiokoa wewe na familia yako ! akasema Gosu Gosu na Jenerali William akabaki kimya

“Jenerali William hakuna faida yoyote kuendelea kuficha kirusi hicho.Tuonyeshe mahala kilipo tutakichukua na kukihifadhi sehemu salama.Hakuna

atakayefahamu kuhusu mpango huo na nchi zetu zitaendelea kuwa salama” akasema Gosu Gosu

“Sifahamu chochote kuhusu hicho kirusi unachokizungumzia.Wewe ni mwanajeshi wa aina gani ambaye unashindwa kunielewa?Nitazame macho yangu kama ninakudanganya ! akafoka Jenerali William

“Gosu Gosu,Sattar amezinduka” Ruby akamfahamisha Gosu Gosu

“Ninakuja baada ya muda mfupi na safari hii utanielewa

mimi ni mwanajeshi wa namna gani ! akasema Gosu Gosu na kutoka akaingia katika chumba walimo akina Ruby

“Gosu Gosu inakuaje unashindwa kutumia nguvu kumfungua huyu jamaa?Muda unatukimbia na tunatakiwa hadi mapambazuko tuwe tumekwisha kipata kirusi” akasema Nawal

“Huyu mtu ni mwanajeshi na si kazi nyepesi kumfungua mwanajeshi lakini nawaahidi nitakaporejea tena anakwenda kueleza ukweli” akasema Gosu

Gosu halafu akaongozana na Nawal wakaelekea katika chumba alimo Sattar.Tayari alikwisha rejewa na fahamu na alikuwa amefungwa katika kiti.Baada ya kuingia wale watu wa kitengo cha afya wakatoka wakawaachia uwanja akina Gosu Gosu.

“Sattar tumerejea tena. Nakuhakikishia leo utapoteza fahamu hata mara kumi hadi utakapoamua kufunguka na kutueleza ukweli.Tumekuondoa meno mawili tutaendelea kuyaondoa moja baada ya lingine na kama

bado utakuwa kimya tutaendelea na viungo vingine.Ili mambo haya yasiendelee tueleze kweli tafadhali ! akasema Nawal.Sattar mdomo wake ulikuwa umevimba na bado alionekana kuwa katika maumivu makali.Gosu Gosu akaenda kuchukua vifaa vile vya kung'olea meno akaviweka mezani.Nawal akachukua picha moja akaiweka mezani

"Unaweza ukamtambua huyu mtu pichani? Akauliza Nawal.Sattar akaitazama picha ile na kwa taabu akatamka

“Huyu ni mimi ! akajibu kwa kiarabu

“Safi.Ahsante kwa kuamua kutoa ushirikiano.Picha hii ilipigwa mchana wa leo katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere pale ulipowasili.Sattar tunafahamu katika masanduku haya mawili ulibeba kirusi ambacho umetumwa kuja kukisambaza hapa Tanzania.Nataka kufahamu kirusi hicho kiko wapi?akauliza Nawal,Sattar hakujibu akabaki kimya

“Sattar nahitaji majibu ama sivyo zoezi litaanza upya !

akasema Nawal lakini bado Sattar hakufumbua mdomo wake.Nawal akasimama na Gosu Gosu akashika tena vile vifaa vyake

“Mara ya mwisho nakuuliza kirusi kiko wapi? Akauliza Nawal lakini Sattar bado alikuwa kimya.Gosu Gosu akamnasa makofi mawili mazito halafu kichwa chake kikagandamizwa katika kiti na jino la tatu likang’olewa.Sauti ya Sattar ilielekea kukauka kutokana na kulia kwa maumivu aliyoyapata.

“Kirusi kiko wapi Kirusi? Akauliza Nawal.

“Nawal huyu bado maumivu hayajamkolea ! akasema Gosu Gosu na kushika tena vile vifaa vyake lakini Sattar akatamka kitu Nawal akamtaka Gosu Gosu asubiri

“Unasemaje Sattar? Akauliza Nawal

“Nitawaeleza ! akasema Sattar.Gosu Gosu akachukua pamba akamimina dawa Fulani na kumuwekea Sattar pale mahala alipong’oa jino na baada ya sekunde kadhaa

damu ikaacha kutoka lakini bado Sattar aliendelea kuhisi maumivu makali mno.

“Kiko wapi kirusi? Akauliza Nawal

“Nili…aaaghh !akagugumia kwa maumivu

“Niliwakabidhi wamarekani wakihifadhi hadi kesho” akasema Sattar kwa taabu.

“Unafahamu mahala kirusi hicho kilipohifadhiwa? Akauliza Nawal

“Sifahamu ! akajibu Sattar

“Sattar eleza ukweli ama sivyo tutaendelea kukung’oa

jino moja baada ya lingine ! akafoka Nawal

“Nawaeleza ukweli sifahamu wamekiweka wapi ! akasema Sattar

“Anasemaje huyu? Akauliza Gosu Gosu ambaye hakuelewa kile alichokisema Nawal kwa kuwa hafahamu lugha ya kiarabu

Nawal akamwambia Gosu Gosu alichokisema Sattar

“Anaonekana anasema ukweli.Endelea naye taratibu aeleze mambo yote mimi ngoja nikaendelee na Jenerali William” akasema Gosu Gosu

na kutoka akarejea katika chumba alichokuwamo Jenerali William

“Jenerali William hii nimekuja ni mara ya mwisho nataka unieleze mahala kirusi kilikofichwa !

“Nenda kuzimu Bazazi wewe ! akafoka Jenerali William na kumpandisha hasira Gosu Gosu akamsogelea na kumtandika ngumi mbili za usoni na mdomo wa Jenerali William ukajaa damu

“Unanipiga !! akasema Jenerali William kwa ukali

“Muda wa mchezo umepita William sasa ni kazi moja tu.Aidha uonyeshe kilipo kirusi au nikuharibu haribu na kukuachia ulemavu wa kudumu ! akasema Gosu Gosu na Jenerali William akamtemea mate yenye damu

“Kamwe huwezi kunitisha nyani wewe ! akasema Jenerali William na Gopsu Gosu hakumjibu kitu akaanza kumvurumishia makonde mazito.Ndani ya sekunde chache uso mweupe wa Jenerali William ukabadilika na kuwa

mwekundu,ulichafuka kwa damu.

“Mimi ni muuaji lakini wewe sintakuua ninataka nikutese ili uwe mfano.Nitakukata ulimi wako hautaweza kuzungumza tena,nitakuondoa vidole vyako vya mikono na miguu na hautaweza kuandika wala kumsimulia mtu kilichokupata.Utateseka na utakufa taratibu.Kwa mara ya mwisho wapi kilipo kirusi? Akauliza Gosu Gosu lakini Jenerali William hakujibu kitu.

Gosu Gosu akatoka na kwenda kumchukua Sattar aliyekuwa anahojiwa na Nawal akaingia naye katika chumba alimo Jenerali William ambaye alistuka baada ya kuiona sura ya Sattar ilivyobadilika.

“Gosu Gosu anataka kufanya nini? Ruby akauliza kwa wasi wasi

“Subiri tuone anachotaka kukifanya” akajibu Nawal

“Japo ulikana kutomfahamu lakini huyu ni Sattar Sayf al Din ambaye amekiri kuleta kirusi hapa Tanzania na kuwakabidhi

ninyi mkakihifadhi.Nataka kujua mahala kirusi hicho kilipo ! akasema Gosu Gosu lakini bado Jenerali William aliendelea kubaki kimya

Ghafla Gosu Gosu kafanya kitu ambacho hakuna aliyekuwa amekitegemea.Alichomoa bastora yake kwa kasi ya ajabu na kumtandika risasi Sattar katika paji la uso akaanguka sakafuni na kufariki .Jenerali William akaingiwa na woga mkubwa

“Nini umefanya hiki wewe katili? Akauliza Jenerali William sauti yake ikitetemeka

“Tumefika mwisho William.Hatutaki mchezo tena.Huyu ndiye aliyetumwa kuja kusambaza kirusi hapa Tanzania.Nimemuua na hakuna tena mtu wa kukisambaza kirusi hicho.Huyu ndiye aliyekuwa na maelekezo yote ya namna ya kufanya.Una sekunde thelathini za kuamua aidha kuonyesha kilipo kirusi hicho au kumfuata huyu shetani

mwenzako ! akasema Gosu Gosu

“Gosu Gosu what have you done ?! Ruby akauliza na kutaka kutoka ndani ya kile chumba ili aweze kumfuata Gosu Gosu katika chumba cha mahojiano lakini Nawal akamzuia

“Subiri kidogo Ruby.Kuna kitu nimekiona ! akasema Nawal

“Umeona nini?

“Subiri kidogo” akasema Nawal akiwa ameyaelekeza macho yake akimtazama Jenerali William

“Mara ya mwisho William wapi kilipo Kirusi? Akauliza Gosu Gosu lakini Jenerali William akabaki akimtazama.Alionekana kuchanganyikiwa.Gosu Gosu akamnyooshea bastora

“Sekunde thelathini zimekwisha.Kwa heri William” akasema Gosu Gosu na William akafumba macho.Gosu Gosu akaachia risasi mbili zilizopita pembeni ya kichwa cha William

Sekunde kadhaa zikapita William akafumbua macho.Alikuwa anatokwa na

jasho usoni huku akihema haraka haraka

“Nimetaka kukuonyesha kwamba ninao uwezo wa kukutoa roho yako muda wowote William.Nimepitisha risasi pembeni makusudi kabisa lakini safari ijayo sintakosa.Nitaingiza risasi kati kati ya kichwa chako.Tuokoe muda nataka unieleze kilipo kirusi ! akasema Gosu Gosu na Jenerali William akafumba macho

“William uko tayari kufa kwa ajili ya kulinda kirusi? Hujui kamba kirusi hicho

kinaweza kuvuka mipaka na kusambaa hadi nchini kwenu Marekani na hata familia yako inaweza kuathirika? Usiwe mjinga kiasi hicho William.Hawa waliokutuma ufanye hivi ni kwa maslahi yao.Tusaidiane kuokoa watu wetu wasije wakaangamia.Yawezekana labda hujaelezwa kwa undani kuhusiana na kirusi hicho.Labda nikueleweshe William kwamba kirusi hicho ambacho hakina tiba wala kinga kinasambaa kwa njia ya hewa na endapo kikiachiwa

hapa Tanzania hakuna namna ya kukizuia kisivuke mipaka ya Tanzania na kusambaa katika nchi jirani hatimaye bara zima la Afrika na mwisho dunia nzima.Hata Marekani lazima kitafika.Utajisikiaje pale ndugu zako watakapoanza kuangamizwa na kirusi ambacho umesaidia kukisambaza? Akauliza Gosu Gosu na kumtazama Jenerali William

“Ninakupa nafasi nyingine William ya kuweza kuiokoa dunia dhidi ya maangamizi makubwa yatakayotokea

endapo kirusi hicho kitasambazwa.Nakubali endapo kirusi hicho kitasambaa mtafanikiwa kutimiza lengo lenu kwani mtaleta watu wenu wengi tu kwa lengo la kuja kutoa msaada kumbe mna ajenda ya siri nyuma yake.Mtachukua mali nyingi lakini damu za wale watakaokuwa wamefariki kutokana na kirusi hicho hazitawaacha salama.Zitawaandama usiku na mchana.William sitaki kuzungumza mambo mengi nataka ukatuonyeshe mahala

kilipo kirusi ! akasema Gosu Gosu.Jenerali William akainamisha kichwa akafikiri kwa muda halafu akainua kichwa na kusema

“Nini mtakifanya endapo nitawaonyesha mahala kilipo kirusi hicho? Mtakwenda kukisambaza Marekani kama ulivyoniambia? Akauliza Jenerali William

“Sisi si wakatili kama ninyi.Hatutaweza kukisambaza hicho kirusi tutakihifadhi sehemu salama ambako hakitakuwa tishio kwa

binadamu” akasema Gosu Gosu

Jenerali Wiliam akafikiri kwa muda halafu akasema

“Endapo nitawaonyesha mahala kilipo kirusi hicho kuna mambo mawili ninataka tukubaliane” akasema Jenerali William

“Nini unakitaka Jenerali William? Akauliza Gosu Gosu

“Kwanza kabisa mtaniacha huru na pili suala hili litabaki kati yetu na hakuna atakayefahamu kama kulikuwa na mpango wowote wa kusambaza kirusi hapa

Tanzania.Nataka tulimalize suala hili kimya kimya mchukue kirusi mkakihifadhi sehemu salama na suala hili lifike mwisho.Mko tayari kwa hilo? Akauliza Jenerali William na Gosu Gosu akacheka kidogo

“Gosu Gosu mkubalie hicho anachokitaka” Ruby akampa maelekezo Gosu Gosu

“Nini ?! Gosu Gosu akashangaa

“Ninahitaji kujadiliana na wenzangu kuhusiana na suala hili.Nitarejea ndani ya muda mfupi” akasema Gosu Gosu na

kutoka mle ndani akawafuata akina Ruby

“Ruby are you out of your mind ?! akauliza Gosu Gosu kwa ukali

“Gosu Gosu hatuna namna ya kufanya zaidi ya kukubaliana na ombi lake ili tuweze kukipata kirusi hicho.Tusiharibu mambo Gosu Gosu nenda mle ndani mwambie tunakubaliana na matakwa yake na atuonyeshe kilipo kirusi”

“Then we let him go? Akauliza Gosu Gosu

“Ruby hawa watu ni wanyama sana.Mambo waliyoyafanya katika ardhi yetu si ya kibinadamu.Watanzania wenzetu wengi wamepoteza maisha kwa sababu ya watu hawa.Hatuwezi kumuacha akaenda hivi hivi” akasema Gosu Gosu

“Anachokisema Gosu Gosu kina msingi.Hatuwezi kuwaacha watu hawa wakaendelea kuifanya kile wakitakacho lazima wafundishwe adabu ! akasema Nawal

“Nini mnashauri kifanyike ili tukipate kirusi hicho? Akauliza Ruby

“Tumkubalie ombi lake ili atuonyeshe kilipo kirusi.Tukisha kipata kirusi hicho hatutamuacha salama ! Marekani lazima waondoke hapa nchini kwa nguvu ! akasema Gosu Gosu

“Una maanisha tumuue Jenerali Wiliam? Ruby akauliza

“Hakuna haja ya kumuonea huruma.Huyu amekuwa akishirikiana na hata kuwalinda watu wa IS

wanaochochea vurugu za kidini hapa nchini na kusababisha vifo vya watu wengi.Lazima tupeleke vilio pia Marekani kama wao walivyosababisha vilio hapa nchini" akasema Gosu Gosu

"Gosu Gosu tusipoteze muda nenda kazungumze naye na atuonyeshe kilipo kirusi na baada ya kukipata tutajua nini cha kufanya" akasema Ruby na Gosu Gosu akarejea katika chumba cha mahojiano alimo Jenerali William.Sakafu ya chumba kile ilikuwa imetapakaa damu na Sattar

Sayf Al Din alikuwa amelalia dimbwi la damu.

“Tumeyakubali yale unayoyataka lakini tutatekeleza pale tutakapokuwa tumekipata kirusi.Hivyo bila kupoteza muda tuonyeshe mahala kilipo kirusi hicho” akasema Gosu Gosu

“Nitawapeleka mimi mwenyewe mahala hapo”

“Wewe utabaki hapa na sisi tutakwenda wenyewe kukichukua kirusi hicho na tutakapokihakiki kwamba ni chenyewe ndipo

tutakapokuachia uende zako lakini kabla ya kukitia kirusi hicho mikononi mwetu hautabandua mguu wako ndani ya chumba hiki ! akasema Gosu Gosu

“Kirusi hicho kiko mahala ambako ninyi hamuwezi kuingia,kama kweli mnakitaka niko tayari kwenda kuwakabidhi”

“Mahala pekee ambako hatuwezi kuingia ni mbinguni anakoishi muumba wetu lakini kwa hapa duniani sehemu yoyote sisi tunaingia.Unadhani ni Marekani pekee ambao mna

jeshi au makachero wenye uwezo mkubwa? Hata sisi tunao uwezo mkubwa sana wa kufanya yale mnayoyafanya ninyi na hata zaidi hivyo tuelekeze mahala kirusi kilipo na sisi tutakwenda kukichukua" akasema Gosu Gosu kwa kujiamini

"Kwa nini unashindwa kunielewa? Kirusi hakiko baa au shambani kiko sehemu nyeti sana ambako ninyi hamuwezi kufika" akasema Jenerali William

"Kiko wapi? Tupe maelekezo na sisi tutakwenda

kukichukua tena naomba ufanye hivyo haraka kabla sijabadilika.Nimekwisha kwambia hautabandua mguu wako humu ndani hadi pale tutakapokipata kirusi na kujiridhisha kuwa kweli ni chenyewe ndipo tutakapokuacha uende zako” akasema Gosu Gosu akimtazama William kwa macho makali

“Kwa mara ya mwisho wapi kilipo Kirusi? Akauliza Gosu Gosu na kuupeleka mkono wake ilipo bastora

“Kirusi kipo katika kambi ndogo ya wanajeshi wa Marekani iliyoko ufukweni” akasema Jenerali William

“Kiko sehemu gani ndani ya hiyo kambi? Gosu Gosu akauliza

“Kuna kontena ambalo hulitumia kwa ajili ya kuhifadhi miili ya wanajeshi wanapokuwa wamefariki dunia na humo ndimo kilimo kirusi” akasema Jenerali William

Gosu Gosu akafungua mlango akatoka na kuingia katika chumba walimo akina

Ruby bila kuwasemesha akachukua karatasi na kalamu akarejea katika chumba cha mahojiano na kuviweka mezani.

“Nataka uchore ramani ya namna ya kuweza kufika katika hilo kontena lenye kirusi” akasema Gosu Gosu na kumfungua mkono wa kulia. Jenerali William akaunyoosha mkono halafu akaanza kuchora ramani ya kambi ilivyo na namna ya kuweza kufika katika kontena ambalo kumehifadhiwa kirusi.

“Ahsante kwa ushirikiano wako.Utaendelea kubaki hapa hapa hadi pale tutakapokipata kirusi” akasema Gosu Gosu

“Mnajidanganya bure hamtaweza kufika mahala hapo” akasema Jenerali William

“Na wewe maisha yako yatakuwa yameishia humu ndani ! akasema Gosu Gosu na kutoka.

“Mambo yameiva ! akasema Gosu Gosu

“Tunakwenda kuvamia kambi ya jeshi la Marekani hii

si operesheni rahisi hata kidogo” akasema Ruby

“Ni operesheni nzito lakini lazima ifanyike usiku huu na lazima ifanikiwe kwa namna yoyote ile ! Akasema Gosu Gosu

“Nawal ulifanikiwa kuingia katika kambi hiyo anayoizungumzia William.Nini ulikiona hapo?

“Ni kambi ndogo na haina wanajeshi wengi hata vifaa vilivyoko pale ni vichache.Kambi yao kubwa iko katika uwanja wa Uhuru.Tusiogope jamani

tunaweza kuvamia kambi hiyo”

“Ruby kwa nini tusiombe msaada kutoka kwa Rais atupatie vikosi vya jeshi? Akauliza Gosu Gosu

“Operesheni hii ni ya kimya kimya na hawapaswi kujua nani aliyewashambulia.Tukitumia vikosi vya jeshi utakuwa ni mgogoro mwingine tumeuanzisha.Tunao makomando wetu tutawatumia wote na vile vile tunao makachero.Hakuna atakayebaki hapa leo wote

wanakwenda kupambana kuhakikisha wanakipata kirusi hicho.Wakusanye watu wote niwajulishe kile tunachokwenda kukifanya usiku huu” akasema Ruby na kabla Gosu Gosu hajatoka Nawal akasema

“Nina wazo moja.Katika ile nyumba alikokuwa akiishi huyu Jenerali William kulikuwa na gari la jeshi la Marekani.Ninafikiria kwa nini tusilichukue gari lile na kulitumia katika operesheni hii? Akasema Nawal

“Wazo zuri sana Nawal.Gari hilo linaweza kutusaidia kuingia katika hiyo kambi wakidhani sisi ni wenzao halafu tutawapa shambulizi la kushtukiza na watakapostuka wamevamiwa tayari tutakuwa tumekipata kirusi na kuondoka zetu” akasema Gosu Gosu halafu akatoka kwenda kuwakusanya makomando na makachero wengine wote wa SNSA kwa ajili ya kupanga namna ya kwenda kukichukua kirusi katika kambi ndogo ya wanajeshi wa Marekani.

Ilichukua saa mbili kufanya maandalizi kwa ajili ya operesheni ile ya kuvamia kambi ya wanajeshi wa Marekani.Baada ya Ruby kujiridhisha kuwa kila kitu kiko vizuri,akatoa ruhusa safari ianze.Msafara wa magari ya makomando na makachero wa SNSA wakiongozwa na gari la jeshi la Marekani ambalo lilikwenda kuchukuliwa mahala alikokuwa akiishi Jenerali William,uliondoka katika makao makuu ya SNSA kuelekea katika kambi ndogo ya jeshi la Marekani.Helkopta

maalum kwa ajili ya operesheni za usiku nayo haikubaki nyuma ilipaa angani ikiwa na makomando kuelekea katika kambi hiyo.

SAA MOJA BAADAE

Ukimya mkubwa ulitawala katika ofisi kuu za SNSA.Ndani ya chumba cha operesheni walikuwemo Ruby,Nawal na wafanyakazi wengine wa SNSA wakifuatilia kwa karibu kile kilichokuwa kinaendelea katika operesheni ya kuvamia kambi ndogo ya jeshi la

Marekani kwa ajili ya kuchukua kirusi kilichokuwa kimehifadhiwa hapo.Toka kikosi cha SNSA kilivyofika katika kambi hiyo na kuvamia wakiwa na silaha nzito walikuwa wakiwasiliana na ofisi kuu kuwajulisha kilichokuwa kinaendelea lakini baada ya muda mapambano yakawa makali na kilichobaki kinasikika ni milio ya risasi na sauti za maelekezo ya viongozi.Mapambano yalikuwa makali na hii iliwapa hofu kubwa sana watu waliobaki

ofisi kuu za SNSA kuhusu usalama wa wenzao.

Baada ya takribani saa moja ikisikika milio ya risasi na mabomu,hatimaye nyuso za akina Ruby zikachanua kwa tabasamu pale walipoisikia sauti ya Gosu Gosu akiwajulisha kuwa wamefanikiwa kukipata kirusi.

“SNSA tumemaliza kazi na tumekipata kirusi.Narudia tena tumefanikiwa kukipata kirusi” akasema Gosu Gosu na watu wote waliokuwamo ndani ya chumba kile wakashangilia kwa nguvu.

“Mapigano yamemalizika? Akauliza Ruby

“Hakuna kilichobaki hapa.Tumeiteketeza kambi yote.Hapa kinachoonekana kwa sasa ni moto unaoendelea kuwaka ! akasema Gosu Gosu

“Vipi kuhusu watu wetu wako salama?

“Tumepoteza watu saba lakini wote miili yao inarejeshwa hakuna hata mwili mmoja wa watu wetu uliobaki hapa.Tayari vikosi vya ardhini vimekwisha ondoka na sisi tunaondoka sasa hivi na helkopta tutazungumza

tukifika huko lakini kitengo cha afya wajiandae kwani watu wengi wameumia wengine vibaya sana” akasema Gosu Gosu

“Ahsante Gosu Gosu.Kazi nzuri” akasema Ruby na maandalizi ya kuwapokea wenzao yakaanza mara moja.

****

Helkopta ya SNSA ilitua katika sehemu yake na mtu wa kwanza kushuka alikuwa ni Papi Gosu Gosu aliyekuwa amebeba masanduku

mawili.Alikuwa ameloana damu.Wafanyakazi wa SNSA walikuwa wamejipanga tayari kuwapokea

“Hongereni sana kwa kazi hii kubwa” akasema Ruby na kuyapokea yale masanduku mawili kutoka kwa Gosu Gosu

“Ahsante sana Ruby.Lilikuwa ni shambulio la muda mfupi lakini kali sana ! akasema Gosu Gosu huku majeruhi wakishushwa kutoka katika ile helkopta na kukimbizwa katika kitengo cha afya kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

“Gosu Gosu umeumia sana unatakiwa kwenda kupatiwa huduma kwanza” akasema Ruby na Gosu Gosu akachukuliwa kwenda kupatiwa matibabu.

Dakika chache baadae msafara wa magari ukawasili.Majeruhi wakashushwa wakakimbizwa kupatiwa matibabu na miili ya wale waliopoteza maisha ikapelekwa katika chumba maalum kuhifadhiwa.Ruby akawashukuru watu wote kwa kazi kubwa waliyoifanya ya

kuhakikisha kirusi kile kinapatikana.

Wakati majeruhi wakiendelea kupatiwa matibabu,Nawal akatumia muda huo kuwasiliana na Habiba Jawad kumjulisha kuwa tayari wamekipata kirusi

“Hongera sana Nawal kwa kazi nzuri mliyoifanya wewe na wenzako.Sasa dunia iko salama.Nimefurahi mno kwa mpango huu mbaya wa kusambaza kirusi kushindwa kufanikiwa” akasema Habiba

“Kirusi hicho kiko wapi kwa sasa? Akauliza Habiba

“Kiko hapa SNSA hii ni idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi.Utafanyika utaratibu wa kukihifadhi sehemu salama” akasema Nawal

“Hongera sana Nawal kwa kazi hii iliyotukuka mliyoifanya” akasema Habiba

“Mama wewe ndiye unayestahili hongera kwani bila wewe jambo hili lisngefanikiwa.Vipi kuhusu Mathew Mulumbi una taarifa zake zozote? Akauliza Nawal na Habiba akasita kidogo

“Mama una taarifa zozote za Mathew? Akauliza tena Nawal

“Ndiyo Nawal.Tayari Mathew yuko Tehran lakini kuna tatizo limejitokeza” akasema Habiba na kumueleza Nawal kile kilichokuwa kimetokea na hatua alizochukua kwa ajili ya kumsaidia Mathew asiuawe.

“Mama umenistua sana kwa taarifa hii.Maisha ya Mathew yako hatarini .Yuko peke yake kule Tehran na hawa jamaa wanaweza wakamzidi nguvu

wakamuua.Mama nataka niende huko Tehran haraka sana kumsaidia Mathew” akasema Nawal

“Unalosema ni jambo la kweli Nawal,Mathew anahitaji sana msaada.Hawa jamaa watafanya kila mbinu kuhakikisha wanamuua hasa watakapopata taarifa kuwa mpango wao wa kusambaza kirusi Tanzania umeshindwa kufanikiwa.Kwa kuwa hapo umekamilisha kazi fanya mpango uweze kuondoka mara moja kuja hapa Riyadh ili

tupange namna ya kumsaidia Mathew”

“Sawa mama nitafanya mipango ya kuondoka huku haraka na nitakujulisha” akasema Nawal

“Kwa mara nyingine tena Nawal hongereni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya.Naamini Marekani wakisikia mpango wao umeshindwa kufanikiwa watapasuka vichwa” akasema Habiba na kuagana na Nawal ambaye alirejea katika ofisi ya Ruby na kumkuta Gosu Gosu akiwa tayari amekwisha

gangwa jeraha lake la shingoni.

“Pole sana Gosu Gosu” akasema Nawal

“Ahsante Nawal.Ahsanteni nyote kwa msaada wenu.Ule mpango wako wa kutumia gari lao ulisaidia sana kwani walipoliona hawakuwa na wasi wasi wakajua ni wenzao.Mara tu walipofungua geti watu wetu hawakupoteza muda wakaanza mashambulizi na hapo ndipo shughuli ilipoanzia.Wengi wa wanajeshi waliokuwepo kambini walikuwa wamelala na

hawakutegemea kama wangevamiwa na wengine walikuwa wamekwenda doria.Ninakiri wanajeshi wale walikuwa wachache lakini mahiri sana.Baada ya kugundua wamevamiwa kwa haraka sana wakajipanga na tukaanza kushambuliana.Wana mbinu nyingi za kupigana lakini nawasifu makomando wetu nao wameiva barabara kwani waliweza kukabiliana nao na hatimaye tukalifikia lile kontena lenye kirusi tukalifungua na kukichukua na

hapo ndipo mapambano yalipozidi kwani tayari watu wetu kadhaa walikuwa wameuawa.

Kitu cha kwanza tulichokifanya baada ya kuvamia kambi ile tuliilipua nyumba iliyokuwa na mitambo ya mawasiliano hivyo hawakuweza kuwasiliana na wenzao kuomba msaada.Hata hivyo walijitahidi sana licha ya uchache wao na kama wangefanikiwa kuwajulisha wenzao walioko katika kambi kubwa uwanja wa uhuru sijui kama tungetoka salama.Wale

jamaa wako vizuri katika vita” akasema Gosu Gosu

“Poleni sana.Japokuwa tumewapoteza wenzetu lakini damu yao haijapotea bure.Wamekufa kishujaa wakilinda nchi yao na wameokoa maisha ya wengi ambao wangepoteza maisha endapo kirusi hicho kingesambazwa” akasema Ruby

“Tayari tumekipata kirusi.Nini kinafuata? Tunakihifadhi wapi? Mkumbuke vile vile kuwa tumeiteketeza kambi yao yote

na hii haitakuwa taarifa njema kwa Marekani” akasema Gosu Gosu

“Ni wakati muafaka wa kumjulisha Rais afahamu kilichotokea na kile kinachoendelea hapa nchini” akasema Ruby

“Vipi kuhusu Jenerali William? Akauliza Gosu Gosu

“Tulikubaliana tutamuachia huru pale tutakapokuwa tumekipata kirusi na kwa kuwa tumekipata lazima tuheshimu makubaliano yetu na

tumuachie huru”akasema Ruby

“Ruby niambie humaanishi hicho unachokisema ! akasema Gosu Gosu

“Gosu Gosu lazima tuheshimu makubaliano yetu! Akasema Ruby

“Ruby hawa watu si wa kuonea huruma hata kidogo.Hawa watu wamesababisha ndugu zetu wengi wakapoteza maisha.Hatuwezi kumsamehe mtu kama huyu.Kama tusingekuwa na taarifa za

mpango wao wa kusambaza kirusi hicho kingeanza kusambazwa kesho na hakuna anayejua yawezekana na sisi tungekuwa miongoni mwa wale ambao wangeathiriwa na kirusi hicho.Mamia kama si maelfu ya watu wengepoteza maisha.Huyu ndiye ambaye amekuwa akimlinda Assad Ismail mchochezi mkubwa wa machafuko yaliyopelekea watu wengi kupoteza maisha.Katu mtu kama huyu hatuwezi kumuachia.Hastahili huruma ya aina yoyote kwani yeye hakuona huruma wakati watu

wetu wanauana” akasema Gosu Gosu

“Gosu Gosu nadhani tutalijadili jambo hili baada ya kuzungumza kwanza na Rais” akasema Ruby na kuchukua simu akampigia Rais Dr Fabian lakini akataarifiwa kuwa simu ya Rais inatumika ikamlazimu kusubiri

“Kuna jambo nataka niwataarifu jamani” akasema Nawal

“Nimezungumza na Habiba Jawad nikamfahamisha kuwa tayari

tumekipata kirusi” akasema Nawal

“Ama kweli haya ni maajabu.Ni vigumu kuamini eti Habiba Jawad huyu ambaye tunamfahamu anafadhili makundi ya magaidi ndiye ambaye ameokoa taifa letu lisiingie katika maangamizi makubwa.Bila yeye tusingefahamu chochote kuhusiana na hiki kirusi.Nadhani hata hao wamarekani wenyewe watashangaa tumewezaje kugundua mpango wao uliokuiwa wa siri kubwa.

Tunapaswa kumshukuru sana huyu mama” akasema Gosu Gosu

“Uko sahihi Gosu Gosu.Habiba Jawad pamoja na mambo anayoyafanya lakini kwa hili anastahili shukran kwani bila yeye maelfu ya watu wangeangamia” akasema Ruby

“Kuna jambo lingine amenieleza Habiba la muhimu sana.Amenipa taarifa kwamba tayari Mathew Mulumbi amekwisha ingia Iran”

“Oh thank you Lord ! akasema Ruby

“Tunamshukuru Mungu kwa kumuwezesha Mathew kuingia salama nchini Iran lakini kuna tatizo limejitokeza.Maisha ya Mathew yako hatarini”

“Kivipi Nawal? Akauliza Ruby kwa wasi wasi.Nawal akawapa taarifa ile aliyopewa na Habiba

“Bastard ! Gosu Gosu akasema kwa hasira

“Japokuwa tayari Habiba amekwisha muonya kuhusiana na mpango wa kutaka kumuua lakini baada ya kutafakari nimeona bado maisha yake

yako hatarini.Wale jamaa wanaweza wakamshinda nguvu na kumuua kwani Mathew yuko ugenini na hana msaada wowote.Nimeamua nitakwenda Iran kumsaidia Mathew katika kufanikisha misheni yake”

“Unataka kwenda Iran? Akauliza Ruby

“Ndiyo.Nitapita kwanza Saudi Arabia kisha nitaelekea Iran.Nimeipenda sana Tanzania na nilitamani kuendelea kukaa hapa lakini kwa hili lililojitokeza lazima niondoke haraka sana kwenda

kumsaidia Mathew Mulumbi” akasema Nawal na Ruby akashusha pumzi

“Ni wazo zuri sana Nawal.Kwa namna yoyote ile lazima kwenda kumsaidia Mathew ikiwezekana kumuondoa asiendelee na hiyo misheni yake kwani kirusi tayari tumekipata na tutaendelea kuwasaka wote wanaohusika na vurugu hadi tutakapohakikisha wote wametiwa nguvuni.Tatizo ni namna ya kupata usafiri wa haraka wa kukupeleka Saudi Arabia” akasema Gosu Gosu.

“Nadhani ……..” Ruby akataka kuzungumza kitu lakini akanyamaza baada ya simu yake kuita.Alikuwa ni Rais Dr Fabian

“Imekuwa vyema Rais amepiga” akasema Ruby na kuipokea simu

“Mheshimiwa Rais” akasema Ruby

“Ruby ulinipigia simu lakini wakati unanipigia nilikuwa nazugumza na mkuu wa jeshi la polisi.Kuna tukio baya limetokea usiku huu.Moja ya kambi za wanajeshi wa Marekani

walioko hapa Dar es salaam imevamiwa na watu wasio julikana usiku huu na inasadikiwa wanajeshi wote waliokuwepo kambini wakati wa uvamizi huo wameuawa na kambi yote kuteketezwa vibaya sana kwa mabomu.Matukio haya yanataka kukipasua kichwa changu” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais nilikupigia ninaomba kuonana nawe”

“Usiku huu ?! akauliza Dr Fabian

“Ndiyo mheshimiwa Rais usiku huu.Ni muhimu sana”

“Haliwezi kusubiri hadi kesho?

“Hapana mheshimiwa Rais ni suala la kuzungumza usiku huu huu” akasema Ruby na Rais akakubali Ruby aende ikulu kuonana naye usiku ule.Aliingia katika gari lake akiongozana na walinzi wake kuelekea ikulu akiwaacha Gosu Gosu na Nawal

Mara tu Ruby alipoondoka Gosu Gosu akaenda katika chumba alimo Jenerali

William.Ujio wa Gosu Gosu ulimstua Jenerali William

“Nimerejea ! akasema Gosu Gosu akimtazama Jenerali William kwa macho yaliyojaa hasira

“Tumepoteza watu saba lakini kirusi tumekipata na kambi yote tumeiteketeza.Hakuna mwanajeshi wako hata mmoja aliyekuwapo kambini hapo usiku huu aliyepona wote tumewaua ! akasema Gosu Gosu na Jenerali William akapandwa na hasira

“Aaaagghhhh !! akasema kwa hasira Jenerali William huku akijaribu kujitikisa katika kiti alichokuwa amefungwa.

“Hakuna unachoweza kukifanya William ! Huu ni mwisho wako ! akasema Gosu Gosu

“Tuliweka makubaliano na nimetimiza upande wangu.Sasa ni upande wenu nataka mniachie huru niende zangu kama tulivyokuwa tumekubaliana ! akasema Jenerali William

“Siyo rahisi namna hiyo kama unavyodhani

William.Itakuchukua miaka kutoka humu na ikiwezekana hautaweza tena kutoka” akasema Gosu Gosu

“Tulikubaliana !! akafoka Jenerali William

“Sikiliza Jenerali William.Ninyi ni watu makatili msio na hata chembe ya huruma.Mmesababisha mamia ya watanzania wameuana kwa kujenga chuki baina yao.Kana kwamba damu mliyoimwaga haitoshi bado mkataka tena kusambaza kirusi ambacho kingesababisha maangamizi makubwa.Mungu analipenda

taifa hili na mpango wenu umeshindwa kufanikiwa.Hatuwezi kukuachia kirahisi namna hiyo Jenerali William.Kwa sasa endelea kupumzika tutazungumza vizuri hapo baadae hizi ni salamu tu nimekufikishia” akasema Gosu Gosu na kutoka

****

Ruby aliwasili ikulu na kumkuta Dr Fabian akimsubiri.

“Karibu Ruby” akasema Dr Fabian huku akimimina kinywaji katika glasi mbili akampatia moja Ruby.

“Ruby wewe ni mtu ambaye sikufichi jambo.Nataka nikuweke wazi kwamba sifikirii tena kuwania urais kwa kipindi cha pili pale kipindi changu cha kwanza kitakapomalizika.Hii si kazi nyepesi hata kidogo kuna nyakati ninajuta kwa nini niliingia katika siasa” akasema Dr Fabian

“Dr Fabian hayo ni masuala yako binafsi ambayo

sisi wengine hatustahili kuyafahamu lakini kwa sasa kwa kuwa bado umekalia kiti cha urais basi jielekeze katika kuwatumikia watanzania.Simama imara kuhakikisha nchi inakuwa salama na maisha ya watanzania yanarejea kuwa ya kawaida” akasema Ruby

“Ninachokupenda Ruby ni namna unavyoweza kunieleza ukweli.Wengine hawawezi kunitamkia maneno kama haya uliyonitamkia.Ahsante kwa kuwa mkweli kwangu na nitayaheshimu mawazo yako”

akasema Dr Fabian na kunywa funda la kinywaji

“Nimepigiwa simu usiku huu na mkuu wa jeshi la polisi akinijulisha kuwa kambi ndogo ya wanajeshi wa Marekani iliyoko kando mwa bahari imevamiwa na watu wasiojulikana waliokuwa wamejihami kwa silaha nzito na kuiteketeza kabisa pamoja na kuua wanajeshi wote waliokutwa hapo kambini.Taarifa hiyo imenichanganya sana kichwa changu ! akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais tuliweke kwanza hilo pembeni tutalizungumza baadae lakini nimekuja kukupa taarifa ya kile ambacho SNSA tumekuwa tunakichunguza tukianzia kwanza na vurugu zile kubwa zilizopelekea umwagaji mkubwa wa damu” akasema Ruby na kunyamaza kidogo

“Toka vurugu zilipoanza tulianza kuchunguza chanzo chake tukijaribu kuziunganisha na vurugu zilizoanzia nchini Uganda lakini napenda nikiri kwako kwamba tulifika mahala

tukakutana na giza nene mbele yetu.Hatukuwa na mwangaza ,tulikata tamaa.Mara akatokea Mathew Mulumbi ambaye ndiye aliyekuja kutufumbua macho na kutupa mwangaza" akasema Ruby na kunyamaza baada ya sura ya Dr Fabian kubadilika aliposikia jina la Mathew Mulumbi likitajwa

"Mheshimiwa Rais najua jina la Mathew linakuchefua lakini naomba uvumilie kwani litajitokeza mara nyingi katika mazungumzo haya" akasema Ruby

“Endelea usijali” akasema Dr Fabian

“Mathew alikutana nasi, mimi na Gosu Gosu na akatufahamisha kwamba amekuja nchini kwa misheni maalum ila hakutueleza ni misheni gani.Alichotueleza ni kwamba vurugu zile zilizotokea nchini na kupelekea waumini wa dini kushambuliana na kuuana zina nguvu kubwa kutoka nje ya nchi” akasema Ruby na kumueleza Dr Fabian kila kitu alichoelezwa na Mathew na sura ya Dr Fabian ikabadilika

kwa mshangao mkubwa alioupata.Ruby hakumjali akaendelea

“Tulifuata maelekezo ya Mathew na kuwakamata wale magaidi wote isipokuwa Assad Ismail ambaye ndiye aliyekuwa kiongozi wao.Wakati tukiendelea kumsaka Assad tukampokea mgeni anatokea Saudi Arabia ambaye ni Yule Chloe niliyekuja naye hapa jana nikakuomba utusaidiekumuunganisha na mkuu wa vikosi vya Marekani vilivyoko hapa nchini.Yule ni

Jasusi aliyekuwa anafanya kazi na shirika la ujasusi la CIA ambaye alikutana na Mathew huko Palestina katika kikundi kimoja cha wanamgambo wanaopambana na serikali ya Israel ambako Mathew alikuwa amejiunga nao akiwa katika misheni maalum" akanyamaza Ruby baada ya Dr Fabian kumfanyia ishara anyamaze

"Ruby mambo unayonieleza ni mazito sana lakini naona kama vile unanieleza juu juu.Ninataka unieleze kwa kina.Umesema huyu Chloe ni jasusi ambaye

alikutana na Mathew huko Palestina katika kikundi cha wanamgambo.Mathew alikuwa anafanya nini katika kikundi hicho cha wanamgambo? Ninataka kufahamu tafadhali” akasema Dr Fabian

“Ili ulifahamu jambo hili kwa undani zaidi nitakuanzia mbali kidogo” akasema Ruby na kuanza kumueleza Dr Fabian namna Mathew alivyopotea wakati wa operesheni ya kubadilishana mateka kati yao na magaidi wa IS.Ruby alimueleza Dr Fabian kila kitu toka Mathew

alipokamatwa na watu wa Mossad na kufungwa kwa miaka mitatu akiteswa na hadi alipojiunga na kundi la Ammar Nazari Brigades.Historia hii yote alielezwa na Nawal

Ruby akaendelea kumpa Rais maelezo ya kuhusiana na safari ya Mathew hadi alipokutana na Habiba Jawad

“Baada ya kufika kwa Habiba Jawad misheni ikabadilika na mipango ya kumuua haikuendelea tena badala yake akajiunga naye na kuwa sehemu ya familia kwa kumuoa mtoto wa Habiba”

“Dah ! Yaani akathubutu kumuoa mtoto wa mtu anayefadhili ugaidi duniani ! akasema Dr Fabian kwa mshangao

“Wote tulistuka tulipopata taarifa hizi lakini mstuko wetu ni kwa sababu hatukuwa tukimfahamu vyema Habiba Jawad ni nani.Mathew alipata bahati ya kumfahamu haraka ndiyo maana akajiunga naye.Nikukumbushe tu mheshimiwa Rais kwamba katika sakata lile la Melanie David na James Kasai wakishirikiana na magaidi wa

IS,ni Habiba Jawad ambaye alimuwezesha Mathew Mulumbi kulimaliza lile jambo kwa kumpa taarifa muhimu kuhusu James Kasai na mipango yao yote” akasema Ruby

“Are you sure? Akauliza Dr Fabian

“100% Mr President” akajibu Ruby

“Inashangaza sana.Kwa nini akafanya hivyo wakati yeye ndiye aliyekuwa akiwafadhili magaidi wale?

“Baada ya kukamilisha misheni ile Mathew Mulumbi

alirejea Saudi Arabia ambako tayari alikwisha kuwa raia na alijulikana kama Abu Zalawi na safari hii ndipo alipogundua siri kubwa aliyokuwa nayo Habiba Jawad” akasema Ruby na kumueleza Dr Fabian kuhusiana na kikundi kinachojulikana kama G20 kilicho ndani ya shirika la ujasusi la Marekani CIA ambacho ndicho kinamtumia Habiba Jawad katika kufadhili makundi ya kigaidi.Mshangao alioupata Dr Fabian ulikuwa mkubwa

“Ruby hiki unachokisema ni kitu kizito mno.Naomba uongee vitu ambavyo una uhakika navyo.Marekani kamwe haiwezi kushirikiana na magaidi wakati ni nchi inayoongoza katika kupiga vita ugaidi duniani.Inawezekanaje wakaihadaa dunia kuwa wao ni vinara katika kupambana na ugaidi halafu wakageuka upande wa pili na kushirikiana nao? Ruby naomba uwe makini mno na jambo hili” akasema Dr Fabian

“Usihofu mheshimiwa Rais,nina uhakika na hiki

ninachokueleza” akasema Ruby

“Kikundi hicho cha G20” Ruby akaendelea

“Kimekuwa kikishirikiana na makundi mbali mbali ya kigaidi katika mipango mbali mbali duniani yenye maslahi kwa nchi ya Marekani.Vurugu za kidini zilizotokea katika nchi za Afrika ya Mashariki zikianzia Uganda na kusambaa katika nchi nyingine Tanzania na kidogo nchini Kenya ni moja ya mikakati ya kikundi hicho”

“What ?! akauliza Dr Fabian

“Narudia tena mheshimiwa Rais kwamba vurugu hizi ambazo zimetokea Afrika Mashariki na kusababisha waumini wa dini kushambuliana hazikuibuka hivi hivi tu bali ni mipango ya kundi hili la G20 wakiwatumia magaidi wa IS katika kuchochea vurugu hizo”

“That’s not true ! akasema Dr Fabian na kusimama

“It is true Mr President ! akasema Ruby

“Wapi umeyatoa mambo haya Ruby? Kwa Mathew Mulumbi? Akauliza

“Mheshimiwa Rais haijalishi taarifa hizi tumezipata wapi lakini ni taarifa za kweli kabisa na ninaomba uniamini” akasema Ruby

“Hata mwendawazimu hawezi akakuamini Ruby kwa taarifa hiyo.Nimekwisha kutahadharisha kwamba taarifa hizi unazopewa na vyanzo vyako si taarifa sahihi na zina lengo la kuleta mgongano baina ya nchi zetu

na Marekani.Nchi ya Marekani ni marafiki zetu wa muda mrefu na wamekuwa wakitusaidia sana na hata machafuko haya yalipotokea ni wao waliotuma majeshi yao haraka kuja kutusaidia hakuna nchi nyingine iliyofanya hivyo”

“Nalifahamu hilo mheshimiwa Rais lakini naomba utulie nimalizie kile ambacho ninataka kukueleza” akasema Ruby na Dr Fabian akaketi.Ruby akamueleza kwa kirefu kile walichokigundua kutokana na vurugu zile za kidini zilizopelekea mamia ya

watu kupoteza maisha.Dr Fabian akabaki mdomo wazi

“Kwa hiyo mheshimiwa Rais vurugu hizi zote zilizotokea malengo yake ni kujipatia mafuta ya Uganda na ukitazama kwa makini utaamini kile ninachokwambia.Vurugu zilianzia Uganda na zikafika hadi hapa nchini na kwa hapa nchini vurugu zilianzia jijini Tanga.Kwa nini iwe Tanga na si Kilimanjaro? Jibu ni jepesi tu ni kwa sababu ili waweze kuyapata mafuta ya Uganda walilazimika kuudhibiti mji wa

Tanga kwani bomba la mafuta linatoka Uganda na kuishia Tanga na mara tu vurugu zilipoanza Marekani ikatuma vikosi vyake haraka sana kwa lengo la kusaidia kurejesha amani.Hivi sasa meli za Marekani zinapanga foleni zikijaza mafuta jijini Tanga" akasema Ruby na ukimya mfupi ukatanda mle ndani

"Ruby unachokizugumza kinaweza kuwa kweli.Sasa nimeanza kukuelewa" akasema Dr Fabian

"Baada ya mpango wao wa kuchukua mafuta

kufanikiwa,walihitaji kufanya kitu ambacho kitavifanya vikosi vya Marekani viwe na sababu ya kuendelea kuwepo hapa nchini kwa muda mrefu zaidi na ndipo walipokuja na mpango wa kusambaza kirusi hatari cha maangamizi” akasema Ruby na kumueleza Rais kuhusiana na mpango ule wa kusambaza kirusi hapa Tanzania.Dr Fabian akalazimika kufuta jasho usoni.Ruby akatoa faili katika mkoba wake akalifungua na kutoa picha akampatia Rais

“Anaitwa Sattar Seyf Al Din.Huyu ndiye aliyetumwa kuja nchini kusambaza kirusi hicho” akasema Ruby na kutoa picha nyingine

“Hapa ni wakati akishuka ndegeni katika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere akiwa ameambatana na wanajeshi wa Marekani.Haya masanduku mawili ndimo kilimo kirusi”akasema Ruby.Dr Fabian akazitazama picha zile kisha akasema

“Hebu subiri kidogo Ruby.Ninyi mlifahamuje kama kuna mpango huo wa

kusambazwa kwa kirusi hapa Tanzania na hadi mkafahamu mtu anayetumwa kuja kuifanya kazi hiyo? Akauliza Dr Fabian

“Chloe alitumwa kuja kutupa taarifa hiyo na Habiba Jawad.Kikundi hicho cha G20 walimtaka Habiba awatafutie mtu kutoka IS ambaye watamtumia katika mpango huo wa kusambaza kirusi hapa Tanzania na akamtafuta Sattar halafu akamtuma Chloe kutuletea taarifa” Akasema Ruby na kuendelea kumsimulia Dr Fabian

kilichoendelea baada ya Sattar kuwasili nchini na hadi walivyotumia mbinu ya kumkutanisha Nawal na Jenerali William

“Tunashukuru Chloe alipokewa vyema na Jenerali William na akampeleka katika makazi yake na saa mbili za usiku akatupa taarifa kwamba Jenerali William amefika katika makazi hayo akiwa ameongozana na Assad Ismali tuliekuwa tukimtafuta kwa udi na uvumba na vile vile alikuwa ameongozana na Sattar Sayf Al Din.Baada ya kupewa taarifa

hiyo tukaanza kujiandaa na kutuma kikosi caha makomando wetu wakavamia nyumba hiyo na kuwakamata Jenerali Wiliam,Sattar na Assad lakini kirusi kilikosekana.Tuliwafanyia mahojiano na Jenerali Wiliam akatuonyesha mahala kirusi hicho kilipohifadhiwa ambako ni katika kambi yao ndogo iliyoko ufukweni mwa bahari.Hatukuwa na namna nyingine ya kufanya zaidi ya kujipanga na kwenda kuivamia kambi hiyo”

“Wait..! ni ninyi mliovamia kambi ya wamarekani? Akauliza DrFabian kwa mshangao

“Ndiyo mhshimiwa Rais ni sisi.Tumepoteza watu saba na wengine wamejeruhiwa lakini tumefanikiwa kukipata kirusi ambacho kilitazamiwa kuanza kusambazwa siku ya kesho.Kwa sasa kirusi kimehifadhiwa SNSA na nchi iko salama” akasema Ruby na ukimya ukatawala mle ndani.Baada ya muda Dr Fabian akasema

“Nimekosa maneno ya kusema Ruby ! Sijui nitawashukuru vipi kwa jambo hili kubwa mlilolifanya la kuiokoa nchi yetu kutoka katika janga kubwa.Watu hawa ni wanyama wakubwa sikutegemea kabisa kama wanaweza wakatufanyia kitu kama hiki.Watu hawa ambao tunawaheshimu kama rafiki zetu kumbe wana sura mbili ! akasema Dr Fabian kwa hasira

“Kwa nini Habiba Jawad anafanya haya kwa nchi yetu? Akauliza Dr Fabian

“Ni kwa sababu amechoka kufanya hiki anachokifanya na kwa sasa anashirikiana na Mathew kuweza kukiondoa kikundi hicho cha G20 ambacho amekuwa akifanya kazi kwa niaba yao” akasema Ruby

“Hapo ndipo mnaponichanganya.Mathew Mulumbi anashikiliwa na Marekani kwa kulipua ubalozi wake hapa Dar es salaam.Atafanikiwa vipi kukiondoa kikundi hicho wakati ana tuhuma za ugaidi? Akauliza Dr Fabian

“Ule ulikuwa ni mpango maalum uliopangwa na hao G20” akasema Ruby

“Unataka kuniambia kwamba wamelipua ubalozi wao wenyewe? Akauliza Dr Fabian

“Ndiyo mheshimiwa Rais.Mpango huo uko hivi.Hivi sasa Marekani na Iran hazina maelewano mazuri na zimekuwa zikitoleana kauli za vitisho vya kushambuliana.Marekani wana hofu kwamba yawezekana kweli Iran akawa anamiliki silaha kali kama

inavyojitapa hivyo basi wakaamua kuja na mpango maalum wa kuweza kufahamu kuhusu silaha za Iran” akasema Ruby na kumweleza Dr Fabian mpango wote wa G20 kumuingiza Mathew nchini Iran kuchunguza silaha za Iran

“Hivi sasa Mathew yuko nchini Iran tayari kabisa kuanza kazi yake aliyotumwa” akasema Ruby

“Ruby kila unavyozidi kunieleza ninazidi kuchoka.Mambo haya ni makubwa mno.Mathew

Mulumbi ameingia katika misheni ya hatari sana”

“Ni misheni ya hatari mno na kama akifanikiwa kuimaliza salama basi itakuwa na mafanikio makubwa kwani lazima atakiondoa kikundi cha G20”

“Sikufahamu chochote kilichokuwa kinaendelea kuhusu Mathew ndiyo maana nikatamka maneno mengi mabaya na...”

“Usijilaumu mheshimiwa Rais hukufahamu chochote kilichokuwa kinaendelea ndiyo maana nilikushauri kuwa

usizungumze maneno mabaya kwani utafika wakati ambao utajilaumu kwa maneno yako” akasema Ruby na ukimya ukatanda

“Kwa hiyo mheshimiwa Rais hiyo kazi tuliyokuwa tunaifanya ambayo kila uliponiuliza nilikuomba unipe muda zaidi ni hiyo niliyokuleza na hapo ndipo tulipofika” akasema Ruby

“Ruby narudia tena sioni maneno mazuri ya kuwashukuruni kwa jambo hili kubwa mlilolifanya kwa taifa letu na dunia nzima kwa

ujumla kwani endapo kirusi hicho kingesambazwa hapa Tanzani lazima kingesambaa sehemu nyingine duniani”

“Mheshimiwa Rais pamoja na mafanikio haya makubwa tuliyoyapata lakini bado tuna kazi kubwa mbele yetu.Bado tunatakiwa kuufahamu mtandao wote ambao umeshiriki katika kuchochea vurugu zilizotokea hapa nchini na kuwakabidhi jeshi la polisi kwa hatua zaidi za kisheria.Tunaye Assad ambaye tunaamini atatueleza kila kitu kuhusu watu anaoshirikiana

nao.Jambo lingine tunacho kirusi hatari ambacho tunatakiwa kutafuta namna ya kukihifadhi na jambo la mwisho tumeua wanajeshi wa Marekani walioko hapa nchini na kwa hilo tumetengeneza mgogoro na Marekani.Tunahitaji msaada wako katika hili kuihakikishia serikali ya Marekani kwamba kilichofanyika ni shambulio la kigaidi”

“Hapana Ruby ! Hatuwezi kuwaogopa.Ni wao walioanza na sisi tunamaliza.Kuanzia kesho nitawaondoa wanajeshi

wote wa Marekani hapa nchini na nitawaeleza ukweli watanzania na dunia wafahamu ni kitu gani ambacho Marekani imekuwa inakifanya.Hili si suala la kufumbia macho ! akasema kwa ukali Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais wakati wa kuwatangazia watanzania na dunia juu ya jambo hili bado.Ukifanya hivyo utavuruga misheni ya Mathew kule Iran.Tuvute subira kidogo ili Mathew amalizie misheni yake na kisha akakimalize kile kikundi cha G20 na hapo

ndipo tutaitangazia dunia mambo yote waliyokuwa wanayafanya na hadi wakati huo tutakuwa tumekamilisha uchunguzi wetu kuwafahamu watu walioshiriki katika kuchochea machafuko”Ruby akamshauri Rais ambaye aliinama akafikiri halafu akasema

“Wazo zuri Ruby lakini hatuwezi kuendelea kuwaruhusu Marekani waendelee kuchukua tani na tani za mafuta ya Uganda.Lazima tuwaondoe bila ya vurugu.Kuna njia

nyepesi ya kuweza kuwaondoa hapa Afrika Mashariki.Watu hawa wamekuja kwa ajili ya mafuta hivyo basi pale watakapoyakosa mafuta hawatakuwa tena na ulazima wa kuwepo hapa.Tutalipua bomba la mafuta linalotoka Uganda na hiyo itapelekea mafuta kutokushuka tena Tanga.Wakikosa mafuta wataondoka zao" akasema Dr Fabian.

"Hilo ni wazo zuri pia mheshimiwa Rais.Tutajifanya hatujui chochote kuhusiana na mipango yao na hii itasaidia

kumpa Mathew nafasi ya kuweza kukamilisha misheni yake” akasema Ruby

Majadiliano yaliendelea kwa zaidi ya saa moja wakakubaliana mambo kadhaa ya kufanya halafu Ruby akasema

“Mheshimiwa Rais kuna suala lingine ambalo ninahitaji msaada wako”

“Sema Ruby nini unahitaji?

“Mathew Mulumbi yuko katika hatari kubwa ya kuuawa” akasema Ruby na kumueleza Dr Fabian

kuhusiana na mipango ya kumuua Mathew.

“Endapo wakifanikiwa mipango yao basi mpango wa kukisambaratisha kikundi cha G20 hautafanikiwa kwani mpango huo unamuhiaji mno Mathew.Kwa namna yoyote ile lazima tumsaidie ili aweze kuwa salama na afanikishe misheni yake” akasema Ruby

“Kama waliomtuma hawataki aendelee na misheni waliyomtuma na wanataka kumuua kuna ulazima gani wa kumsaidia afanikishe misheni aliyotumwa na hao jamaa?

Kitu cha msingi ni kumsaidia atoke Iran na kurejea nyumbani”Akasema Dr Fabian

“Kuna umuhimu mkubwa wa Mathew kuendelea na misheni yake na atakapoikamilisha itakuwa ni tiketi kwake ya kuingia tena Marekani na hapo ndipo atakapopata nafasi ya kukimaliza kikundi cha G20.Bila kukamilisha misheni aliyotumwa hataweza kurejea Marekani na G20 wataendelea kuwa tishio duniani” akasema Ruby

“Namna gani unataka kumsaidia? Una mawasiliano naye? Unafahamu mahala alipo?Akauliza Dr Fabian

“Sina mawasiliano naye lakini Habiba Jawad tayari amekwisha wasiliana naye na kumjulisha kuhusiana na hatari inayomkabili.Pamoja na kupewa taarifa za hatari hiyo lakini Mathew yuko ugenini na hana msaada wowote wale jamaa wanaweza wakamzidi nguvu na kumuua.Ikitokea bahati mbaya Mathew akauawa hizi juhudi zote tulizofanya zitakuwa bure na

hawa jamaa wanaweza wakajipanga na kurejea kivingine.Baada ya kujadiliana tumekubaliana kwamba Chloe atakwenda Tehran kumsaidia Mathew.Yeye itakuwa rahisi kuingia nchini Iran kwa kuwa ana uraia wa Saudi Arabia.Vile vile Habiba Jawad anafahamiana na watu wanaoweza kumsaidia Chloe kuingia kwa urahisi nchini Iran”

“Kama mna uhakika kwamba Chloe anaweza kuwa na msaada mkubwa kwa

Mathew basi aende mara moja” akasema Dr Fabian

“Kuna jambo limetukwamisha.Namna atakavyoweza kuondoka hapa kwa haraka kuelekea Riyadh” akasema Ruby na Dr Fabian akainamisha kichwa na kusema

“Hakuna tatizo la usafiri.Kwa jambo muhimu kama hili nitatoa hata ndege ya Rais impeleke haraka huko Riyadh.Lini anataka kuondoka?

“Hata sasa hivi akipata usafiri” akajibu Ruby

“Nitatoa maelekezo ndege yangu iandaliwe ili aweze kuondoka kesho asubuhi” akasema Dr Fabian

“Ahsante sana mheshimiwa Rais” akasema Ruby

Tayari imekwisha timu saa kumi za alfajiri,Ruby akaagana na Rais akaondoka kurejea ofisi za SNSA.

Baada ya Ruby kuondoka Dr Fabian akamimina mvinyo katika glasi akagugumia wote

“Mpaka sasa mwili unanisisimka kwa mambo aliyonieleza Ruby.Marekani

wamekuwa ni rafiki zetu kwa muda mrefu na wamekuwa wakitupa misaada mingi ya kimaendeleo na vile vile ni wachangiaji wa bajeti yetu ya serikali lakini kumbe ni chui mwenye ngozi ya Kondoo.Imeniumiza sana kwa kitendo hiki walichotufanyia.Huu ni uonevu na ukandamizaji uliovuka mipaka.Kama vijana wangu wasingesimama imara na kupambana kuhakikisha mipango yao haifanikiwi,wangeweza kusambaza kirusi hatari na

mamia ya watanzania wangeangamia.Huu ni unyama uliovuka kiwango! Akawaza Dr Fabian akiwa ameikunja sura yake kwa hasira akanywa funda lingine la kinywaji

“Sasa ninaanza kupata picha kumekuwa na magonjwa mbali mbali yanaibuka zama hizi bila kujua yametokea wapi na mengine mpaka leo hii hayana tiba,yawezekana virusi vinavyoeneza magonjwa haya vinatengenezwa na kuja kusambazwa huku kisha tunatumia gharama kubwa kununua dawa.Dah ! Matukio

haya yamenifundisha jambo kubwa sana.Ili kuepukana na haya yote nchi zetu zinapaswa kuachana kabisa na utegemezi wa mataifa makubwa.Nchi zetu za Afrika zinapaswa kuanza kujitegemea zenyewe bila kusubiri wafadhili.Kama tukiendelea kutegemea mataifa makubwa waje watuletee maendeleo matokeo yake ni kama haya yaliyotupata ! akaendelea kuwaza Dr Fabian halafu akawasha simu yake aliyokuwa ameizima ili azungumze na Ruby akatoa maelekezo ndege

yake iandaliwe kwa ajili ya safari ya nje ya nchi asubuhi.

****

Ruby alirejea SNSA.Ulinzi ulikuwa umeimarishwa sana.

“Vipi maendeleo ya hapa? Akauliza Ruby

“Hapa kila kitu kinaendelea vizuri.Vipi huko utokako? Akauliza Gosu Gosu na Ruby akawaeleza kila kitu kilichojiri ikulu.

“Ahsante sana Ruby kwa msaada huu mkubwa wa kupatikana usafiri kwenda

Riyadh.Inapendeza kama Rais mwenyewe amekubali kutoa ndege yake kwa ajili ya kunifikisha haraka Riyadh.Hii ina maanisha kwamba Tanzania inanituma kwenda kumsaidia mtoto wao ambaye ni Mathew Mulumbi na ninawaahidi kwamba nitafanya kila lililo ndani ya uwezo wangu kuhakikisha kwamba ninamsaidia Mathew na misheni yake inakamilika.Mathew atarejea nyumbani akiwa mzima kabisa” akasema Nawal

“Inakaribia saa kumi na moja za Alfajiri,nendeni mkapumzike kwa muda mfupi kwani si muda mrefu kutapambazuka” akasema Ruby.GoSu Gosu akamchukua Nawal wakaingia garini huku wakisindikizwa na walinzi kuelekea nyumbani kwa Gosu Gosu kwa ajili ya mapumziko mafupi kabla ya kuanza safari kuelekea Riyadh.

“Gosu Gosu tukifika nyumbani hakuna maongezi mengi.Nataka tutumie muda mfupi uliobaki kuagana kwani yawezekana nisirejee tena

Tanzania.Ninafahamu unachokitaka kwangu toka nimefika” akasema Nawal wakiwa ndani ya gari na kumfanya Gosu Gosu asisimkwe mwili kisha akatabasamu.

Mara tu baada ya kufika nyumbani, Gosu Gosu hakutaka kusubiri.Bila kujali maumivu aliyokuwa nayo kutokana na majeraha aliyoyapata,akambeba Nawal na kupanda naye ngazi hadi chumbani kwake ambako hakukuwa na muda wa kupoteza mpambano ukaanza

mara moja.Gosu Gosu aliumiliki uwanja vilivyo.

****

“Gosu Gosu ! Amka kumekucha tayari” akasema Nawal ambaye naye alistuliwa na mlio wa simu ya Gosu Gosu iliyokuwa ikiita mfululizo.Gosu Gosu akakurupuka kutoka usingizini na kuichukua simu yake.Mpigaji alikuwa ni Ruby

“Ruby habari za asubuhi ! akasema Gosu Gosu kwa sauti ya uchovu

“Nzuri Gosu Gosu,tayari nimekwisha anza kupatwa na wasiwasi.Si kawaida yako kuchelewa kupokea simu namna hii” akasema Nawal

“Ni uchovu wa jana.Mambo yanakwendaje?Uko salama? Akauliza

“Huku shwari kabisa kila kitu kinakwenda vizuri”

“Nawal anaendeleaje?

“Anaendelea vizuri.Ni yeye aliyeniamsha nilikuwa nimepitiwa na usingizi”

“GosuGosu ulikuwa umelala na Nawal? Akauliza Ruby na kumstua Gosu Gosu

“Oh no ! akasema Gosu Gosu

“Gosu Gosu nimetaarifiwa na Rais kwamba ndege iko tayari .Mwambie Nawal ajiandae kwa ajili ya safari.Ninakuja hapo kuwapitia tuelekee uwanja wa ndege” akasema Ruby na kukata simu

“Sikutaka Ruby afahamu kama nimelala na Nawal,hata hivyo hakuna kilichoharibika” akawaza Gosu Gosu na

kumfuata Nawal chumbani kwake na kumkuta akitoka kuoga.

“Ruby anasemaje? Akauliza Nawal

“Ndege iko tayari anatupitia muda si mrefu tuelekee uwanja wa ndege” akasema Gosu Gosu na kumkumbatia Nawal

“Tafadhali fanya kila uwezalo urejee Tanzania pindi mtakapokuwa mmekamilisha misheni yenu huko Iran”akasema Gosu Gosu

“Nimekwisha kuahidi Gosu Gosu kwamba nitarejea

Tanzania.Nimeipenda sana nchi hii” akasema Nawal na kuliachia taulo likaanguka chini

“Mama yangu ! akawaza Gosu Gosu baada ya kuushuhudia mwili mwororo wa Nawal

“Kama isingekuwa Ruby anakuja ningeanzisha kipute kingine hapa hapa.Lakini ngoja tujiandae kwa safari” akawaza Gosu Gosu

“Mbona unanitazama kwa tamaa namna hiyo kama Fisi mwenye njaa? Usijali nitarejea Dar es salaam kwa ajili yako”

akasema Nawal na kumfuata Gosu Gosu akambusu na kumtaka akajiandae.

“I’m not handsome like Mathew and others lakini nina bahati ya kukutana na kupendwa na warembo wenye uzuri wa kimalaika” akawaza Gosu Gosu akielekea chumbani kwake kujiandaa.

Dakika kumi na tano baadae Ruby akawasili na hakukuwa na muda wa kupoteza wakaingia garini wakaondoka kuelekea uwanja wa ndege wa Julius Nyerere.Asubuhi hii hali ya jiji

la Dar ilikuwa shwari na sehemu nyingi za jiji watu tayari walianza kuendelea na maisha yao ya kawaida licha ya kuwa na hofu bado kuwa machafuko yanaweza kuanza tena.Vikosi vya jeshi na polisi viliimarisha doria katika mitaa mbali mbali

Walifika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere ambako Ruby alikutana na wasaidizi wa Rais ambao tayari walikwisha fika uwanjani pale mapema wakawaongoza kuelekea ndani ya uwanja hadi katika ndege ya Rais.Kabla

hawajaingia ndegeni Ruby akamuita pembeni Nawal

“Nawal ukifanikiwa kuonana na Mathew mpe barua hii”akasema Ruby huku akilengwa na machozi

“Nitafikisha ujumbe wako usijali” akasema Nawal na kumkumbatia Ruby na Gosu Gosu halafu akapanda ndegeni.Mlango ukafungwa na taratibu ndege ikaondoka baada ya dakika chache ikapaa kuelekea Riyadh

“Tumuombee Nawal afike salama na amsaidie Mathew.Sisi huku bado

tunaendelea na mchaka mchaka wetu ! akasema Ruby wakaingia garini na kuondoka kurejea SNSA.

MPENZI MSOMAJI

- MPANGO WA KUMUUA MATHEW MULUMBI UTAFANIKIWA?
- NAWAL ATAFANIKIWA KUINGIA NCHINI IRAN KUMUOKOA MATHEW ?
- NINI KITAENDELEA NCHINI TANZANIA BAADA YA

WANAJESHI WA MAREKANI KUUAWA NA SNSA?

MAJIBU YA MASWALI HAYA NA MENGINE MENGI USIKOSE SEHEMU IJAYO YA SIMULIZI HII.

TUNAPOKARIBIA KUFIKA MWISHO WA SIMULIZI HII NDEFU YA SIRI,JIANDAE KWA BALAA LINGINE LA MATHEW MULUMBI KATIKA HADITHI MPYA

SCANDAL(KASHFA)